**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 28 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**MHE. MAULID SALEH ALI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Maulid Ali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki sehemu ya pili hujaisoma, umesoma sehemu moja tu ya bajeti, taarifa hujaisoma, Mheshimiwa Naibu Waziri, uko nayo au tukusaidie, Katibu msaidie hiyo nakala.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):**

Taarifa ya Mwaka ya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha kwa Mwaka 2022/2023. *(The Annual Report 2022/2023 of Arusha International Conference Centre for the Year 2022/2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali na tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 453

### Ujenzi wa Barabara ya Mshangano Legele – Mletele – Songea

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mshangano - Legele hadi Mletele kilometa 9.2?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022/2023 Serikali ilifanya matengenezo katika Barabara ya Mshangano - Legele hadi Mletele ikiwa ni pamoja na kuifungua kilometa 9.2, kung'oa miti, ujenzi wa mitaro meta 2600, ujenzi wa makalavati 12 na uwekaji wa changarawe kilometa 2.6 kwa gharama ya shilingi milioni 52. Aidha, katika mwaka 2023/2024 Serikali imeendelea kufanya matengenezo katika barabara hiyo kwa kuimarisha tuta, kuichonga na kuchimba mitaro ya kutolea maji ya mvua mita 1000 kwa gharama ya shilingi milioni 52.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imefanya usanifu wa barabara hiyo ya Mshangano - Legele hadi Mletele kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa tano ambapo shilingi bilioni 2.51 zinahitajika na ujenzi wake utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri kwamba barabara hii tayari iko kwenye mpango wa kutengewa fedha na kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha, maana huu mpango ni muda mrefu sana, kila mwaka itatengewa, itatengewa. Sasa nataka majibu ni lini Serikali inapeleka fedha kuanza kujenga kwa kiwango cha lami mara moja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi ni kwamba Serikali inatambua umuhimu wa barabara zetu za wilaya na ndio maana kila mwaka imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati na ujenzi. Kwa hiyo, nimhakikishie kama vile Serikali ambavyo tayari imeanza kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii, nimhakikishie kwamba Serikali itahakikisha fedha inapatikana kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan inakwenda kujenga uwanja wa mpira wa kimataifa wa kisasa kwa gharama ya shilingi bilioni 286, lakini hakuna barabara hata moja ya lami ambayo inakwenda kwenye eneo la uwanja. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya lami ikiwepo pamoja na Barabara ya Njolo ili kuleta maana kwenye uwanja wa *AFCON?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Mbunge ni la msingi sana na Serikali kwa kutambua umuhimu wa miundombinu mizuri ya barabara kuelekea katika uwanja huu wa *AFCON,* Serikali tayari imeshafanya utambuzi wa barabara hizo muhimu na imebaini kwamba kuna mtandao wa barabara za jumla ya kilometa 13 ambazo zimeshafanyiwa usanifu na imebainika kwamba zitahitaji shilingi bilioni 18 kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kuwa Serikali itahakikisha shilingi bilioni 18 zinapatikana kwa ajili ya kujenga barabara hizi ili ziweze kufanana na uwanja ule mzuri wa *AFCON* unaotaka kujengwa. Kwa hiyo, nimhakikishie kuwa zitajengwa barabara nzuri kwa ajili ya kiwanja hiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe kutoka Balangdalalu – Gidagunja - Gehandu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ina urefu wa kilometa 12 na tayari katika mwaka wa bajeti wa 2024/2025 imetengewa jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba barabara hii inakuja kujengwa na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 454

**Ujenzi wa Barabara ya Ilembo hadi Mpui - Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kujenga miundombinu ya barabara iliyoharibika kati ya Kijiji cha Ilembo na Makao Makuu Tarafa ya Mpui – Kwela?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022/2023 shilingi milioni 45 zilitumika katika barabara ya Ilembo hadi Mpui kwa ajili ya matengenezo ya kilometa tatu kwa kiwango cha changarawe.

Aidha, katika mwaka 2023/2024 kiasi cha shilingi milioni 55 kimetumika kutengeneza kilometa tatu zaidi kwa kiwango cha changarawe na kivuko na hivyo kuwa na jumla ya kilometa sita za changarawe katika barabara hii yenye urefu wa kilometa 10.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025 Serikali imepanga kuendelea kuimarisha kipande cha barabara kilichosalia chenye urefu wa kilometa nne kwa kukichonga na kuweka mifereji ya kuondoa maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhudumia mtandao wa barabara wa Jimbo la Kwela kwa kuzijenga, kuzikarabati na kuzifanyia matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; katika barabara hiyo anayotaja hitaji kubwa ni daraja kubwa ambalo tumeleta maombi ya fedha shilingi bilioni 1. 3. Je, ni lini Serikali italeta fedha hizo ili kujenga daraja hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Barabara ya Mititi – Mnokola - Mombo ni barabara ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Kata ya Mnokola na imeharibika sana. Je, lini Serikali mtaleta fedha kutengeneza barabara hii muhimu kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, katika Barabara ya Ilembo - Mpui tayari Serikali imeshafanya usanifu wa daraja ambapo imebaini kwamba litagharimu shilingi bilioni 1.35. Nimhakikishie kwamba Serikali inatafuta fedha ili kuhakikisha daraja hili linakamilika na Serikali inataka ifanye jitihada kuhakikisha kwamba miundombinu ya kudumu inajengwa. Kwa wakati huu, tayari Serikali imetengeneza kivuko cha miguu ambach kimejengwa chenye urefu wa meta 120. Kwa hiyo, kwa

kuwa Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara hizi na hasa kiuchumi na kijamii, Serikali itahakikisha inapata fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kudumu kwa maana ya daraja la kudumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; Barabara ya Mnokola – Mititi - Mombo yenye urefu wa kilometa 12 Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya kurekebisha maeneo yale yaliyo korofi ili wananchi waweze kupita kwa urahisi. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhudumia barabara hizi za wilaya katika jimbo lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 455

**Kanuni za Uchaguzi wa Makamu Wenyeviti wa Halmashauri**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza: -

Je, lini utaratibu wa Naibu Meya na Naibu Wenyeviti wa Halmashauri utarekebishwa ili wahudumu miaka mitano badala ya kuchaguliwa kila mwaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Halmashauri za Wilaya zinazoelezea Uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti zimetungwa chini ya kifungu cha 70(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 287 na Kanuni za Kudumu za Halmashauri za Miji zinazoelezea Uchaguzi wa Naibu Meya zimetungwa chini ya kifungu cha 42(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 288

ambapo Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri huchaguliwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa mabadiliko ya sheria, kanuni na taratibu ni sehemu muhimu ya utawala bora na maendeleo endelevu ya jamii. Hivyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikipokea hoja kutoka kwa wadau walio wengi kuhusu hitaji la mabadiliko ya kanuni hizi itazifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly James Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa sheria hii na kanuni hizi hamwoni kwamba zinawanyima hawa wasaidizi kushauri ipasavyo na kujiamini kwenye kutenda kazi kwa sababu anapotokea Meya ameenda kinyume Naibu Meya ataogopa kumshauri akijua baada ya mwaka atamshughulikia na kumwondoa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni lini Serikali mtaleta sheria hizo zibadilishwe ili haki iweze kutendeka kwa hawa wasaidizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa hoja hii. Nimhakikishie tu kwamba sheria zilizopo zinaelekeza uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, Naibu Meya kila mwaka. Halmashauri nyingi ambazo Manaibu Meya na Makamu Mwenyekiti wanakwenda kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba Naibu Meya anaweza kushughulikiwa na Mwenyekiti, anayechagua ni Baraza zima la Madiwani siyo Meya peke yake. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Naibu Meya, Makamu Mwenyekiti anachaguliwa kila mwaka haimnyimi fursa ya yeye kutoa mchango na ku-*exercise* shughuli zake za uongozi ipasavyo kwa sababu tu anachaguliwa kila mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, tunaona hoja ya msingi katika hoja yako na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumelichukua hili ili tukalifanyie tathmini tuweze kuona namna gani tunaweza tukaboresha kama itaonesha itakuwa na tija nzuri zaidi kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, baada ya hilo sasa ndio tutaona lini tunaleta kanuni hizo baada ya kujiridhisha na utaratibu huo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa hapa Bungeni Wabunge wa Viti Maalum wanaweza kuwa Wenyeviti wa Kamati za Bunge; je, Serikali haioni ipo haja kupitia sheria hii ili Madiwani wa Viti Maalum na wenyewe waweze kuwa Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri? Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge halafu tuweze kuona namna nzuri ya kulifanyia kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, sasa aulize swali lake. Haya Mbunge wa Tanga aliyeko Bungeni Mheshimiwa Omari Kigua kwa niaba yake.

Na. 456

**Hitaji la Magari ya Wagonjwa Vituo Vya Afya Mgombezi na Kwamsisi – Korogwe**

**MHE. OMARI M. KIGUA K.n.y. MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza: -

Je, lini Vituo vya Afya Mgombezi na Kwamsisi – Korogwe vitapewa magari ya wagonjwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali ilipeleka magari mawili ya kubebea wagonjwa katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe. Magari hayo yamepangwa kwenye Hospitali ya Magunga na Kituo cha Afya Majengo, lakini yanatoa huduma za rufaa kwa mfumo wa kaskedi kwenye vituo vingine vya huduma vikiwemo Kituo cha Afya cha Mgombezi na Kwamsisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma za rufaa kwa wagonjwa hususan kwa akinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, binafsi nishukuru kwa niaba ya Mheshimiwa Kimea kwa majibu mazuri ya Serikali na nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwenye Wilaya ya Kilindi tuna Vituo vya Afya vya Mwekiboma na Tunguri, lakini hatuna magari. Je, Serikali iko tayari kutuletea magari?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri nilishawahi kuuliza swali nikaomba fedha kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Afya cha Msagalu na akaahidi kwamba Serikali italeta shilingi milioni 100. Je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri utaleta fedha kwenye Kituo cha Afya cha Masagalu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi kubwa sana imefanywa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, kwa kununua magari ya wagonjwa 316 ndani ya mwaka huu na halmashauri zote zimepelekewa magari ya wagonjwa, pia magari 212 kwa ajili ya huduma za usimamizi wa huduma za afya. Kwa ujumla magari 618 yamenunuliwa na yamepelekwa ikiwemo katika Halmashauri ya Kilindi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutafanya tathmini kuona uwezekano wa kupata magari mengine ili yaende kusaidia kutoa huduma za rufaa katika vituo ambavyo amevitaja, ikiwezekana ya ndani ya halmashauri au hata yale ambayo tutayapeleka mengine.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kweli kwamba tunafahamu kituo hicho cha afya kinahitaji shilingi milioni 100 ili kikamilishwe na mimi nirudie tu kuhakikishia kwamba Serikali inatambua hilo na ina *commitment* hiyo. Tunatafuta fedha, fedha ikipatikana tutaleta katika Halmashauri ya Kilindi ili tuweze kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa.

Je, lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Soya, Wilaya ya Chemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali imeshapeleka magari ya wagonjwa katika halmashauri zetu zote 184, lakini kuna mpango wa awamu ya pili wa kupeleka magari mengine ya wagonjwa kwa halmashauri zile zenye vituo vingi vya afya na hasa ambavyo vipo mbali sana kutoka makao makuu ya halmashauri.

Kwa hiyo, naomba tuchukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge, Mama Toufiq kuhusiana na Kituo cha Afya cha Soya tuweze kufanya tathmini kuona kama kuna *ambulance* ambayo inaweza

ikafanya huduma za *casket* karibu kabisa na kituo hicho basi ile *ambulance* ambayo ipo halmashauri au na kituo cha afya cha jirani itaendelea kutoa huduma hizo, lakini kama ni mbali zaidi basi tutafanya utaratibu wa kupata gari lingine la wagonjwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 457

**Ahadi ya Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, lini ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano ya ujenzi wa hoteli ya nyota tano katika Mji wa Mpanda itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la idadi ya watalii nchini, Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu mbalimbali katika sekta ikiwemo huduma za malazi. Kwa upande wa Mkoa wa Katavi, Wizara kupitia *TANAPA* ilipata eneo lenye ukubwa wa hekta 15.37 katika Kitalu A, Kiwanja Na. 12 katika eneo la Magamba-Mpanda Mjini kwa ajili ya ujenzi wa hoteli ya nyota tano. Aidha, tayari hati ya eneo hilo imepatikana na *TANAPA* imechonga barabara pembezoni mwa eneo husika kwa ajili ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa shughuli za uendelezaji wa eneo hilo haukuweza kuanza kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, kwa sasa Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea kufanya

upembuzi yakinifu kuhusu mradi huo kabla ya kuanza utekelezaji wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, sambamba na maono ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano katika ujenzi wa hoteli hiyo, nini kauli ya Serikali katika kuunga mkono *Royal Tour* ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita katika ujenzi wa hoteli hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Wizara imejielekeza kwenye kuhakikisha tunafika mahali kwamba hoteli hii iwe imekamilika na mtazamo wetu katika kuibua sekta ya utalii kwenye ukanda ule tunatarajia kwamba baada ya kukamilisha ujenzi huu tushirikishe sekta binafsi kwenye kuendesha hoteli hii ili kujenga *confidence* ya wawekezaji wengine kuwekeza katika sehemu hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie fursa hii kupongeza uongozi wa Mkoa wa Katavi kwa sababu ni miongoni mwa mikoa ambayo imeandaa mkakati wa utalii wa mkoa wao na imebainisha maeneo ya vivutio vya utalii. Kwa hiyo, sisi Wizara ya Maliasili na Utalii tunachofanya ni kuoanisha vipaumbele vile walivyoviweka katika kutangaza utalii, kuunganisha na mkakati wetu wa utalii ili kutangaza kama *package* moja ya kuweza kuibua fursa za utalii kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kufanya hivyo, lakini sambamba na hilo tunajitahidi sana kuhakikisha tunaboresha miundombinu iliyopo kule kama barabara ili maeneo ya vivutio yaweze kufikika kwa urahisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 458

**Upatikanaji wa Mawasiliano ya Simu Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawezesha upatikanaji wa mawasiliano ya simu katika Vijiji vya Ikuka na Kitumbuka, Wilayani Kilolo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali kupitia *UCSAF* imekifanyia tathmini Kijiji cha Ikuka kilichopo katika Kata ya Uhambingeto na kuingizwa katika mradi ambao utatekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 mara baada ya Serikali kukamilisha taratibu za mkopo kutoka Benki ya Exim China. Kwa upande wa Kijiji cha Kitumbuka kilichopo Kata ya Irole, *UCSAF* itafanya tathmini ili kubaini mahitaji halisi ya mawasiliano ya simu na kuchukua hatua stahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru kwa majibu. Kipengele (b) cha Kijiji cha Kitumbuka baada ya wale wafanyakazi kusikia kuna swali nadhani tayari mawasiliano yapo. Kwa hiyo, usihangaike kufanya utafiti tayari umeshafanyika, lakini sasa nina maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ahadi ya minara ya *UCSAF* mingi tu katika kata mbalimbali ikiwemo Kata ya Masisiwe, Kata ya Kimala na kata nyingine, lakini ujenzi wake upo kwa taratibu

na mpaka sasa bado haujakamilika. Je, ni lini minara hiyo itakamilika ili wananchi wale waweze kupata huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kata ya Nyazwa na Mahenge na Kata ya Kising'a kuna minara ya Halotel ambayo nadhani inatumia *solar,* kwa hiyo, ikifika jioni mtu akituma *message* mpaka kesho asubuhi kwenye saa tatu.

Sasa je, ni lini Serikali itabadilisha mfumo wa minara ile *either* kwa kuwaomba *UCSAF* wakafunge minara mingine ili wananchi wapate *message* usiku huo huo na pia wapate mawasiliano usiku huo huo kama wanavyokusudia? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa ufuatiliaji na sisi baada ya kuona swali pia tukafanya kazi na niwaambie tu wananchi dhamira ya Wizara ni kuhakikisha mawasiliano na usikivu unakuwa muruwa. Kwa maswali haya ya kata uliyoitaja ni kweli *UCSAF* ina minara 758 ambavyo kwenye utekelezaji na eneo ulilolitaja Mheshimiwa Mbunge tayari tunaendelea na taratibu za kuona na lenyewe linafikiwa na kazi za ujenzi hazipo taratibu sasa hivi tupo kwenye asilimia kubwa kwa sababu kazi ni ya miezi 24.

Mheshimiwa Spika, katika kata hii nyingine uliyoitaja Mheshimiwa Mbunge mnara unaotumia *solar,* tayari tuna mawasiliano na wenzetu wa *REA* kuona kwamba tunapeleka umeme wa uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, wananchi wa Makete tunashukuru kwa kuboresha mawasiliano Kata ya Mang'oto, Kata ya Kitulo na Ipelele. Wanauliza Wana Makete, ni lini mtapeleka mawasiliano katika za Kata ya Luwumbu

na Kata ya Ukwama kwa sababu kuna changamoto kubwa ya mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze, kadiri tunavyoendelea kuwasiliana Mheshimiwa Sanga nikuhakikishie hizi kata ulizozitaja ya Ukwama pamoja na hizi nyingine tupo katika hatua za mwisho kuhakikisha tunaleta mawasiliano ya uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kata ya Qamtananat, Eshkesh na Gidardagaw haina mawasiliano ya umeme, je, lini Serikali inatuletea minara hiyo ya umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay.

Mheshimiwa Spika, hizi kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge na zenyewe zipo kwenye utaratibu wa kuhakikisha tunakuja kujenga minara na mawasiliano yaweze kupatikana kwa uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, sasa aulize swali lake.

Na. 459

**Kuimarisha Usikivu wa Redio ya Taifa *(TBC)* – Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaimarisha usikivu wa Redio ya Taifa *(TBC)* katika Wilaya ya Micheweni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, *TBC* imekamilisha ujenzi wa mitambo ya redio masafa ya *FM* katika Visiwa vya Unguja na Pemba. Upande wa Unguja na Pemba mitambo ya *TBC* Taifa na *Bongo FM* imefungwa katika minara ya *ZBC* na inapatikana kwa masafa ya *87.7 MHz* (*TBC* Taifa) na *89.7 MHz* (*Bongo FM*). Matangazo ya *TBC* kwa Pemba yanapatikana katika maeneo yote ikiwepo Micheweni, Mchanga wa Kware, Ziwani, Mzambarauni, Wete, Konde, Kongamasha, Wingwi, Mchangamdogo, *Pemba Airport*, Kichunjuu, Bandari ya Mkoani na kadhalika. Aidha, *TBC* itafanya utafiti kuona kama bado kuna eneo lina changamoto ili kuweza kutatua mapema iwezekanavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiukweli bado kuna changamoto juu ya usikivu wa redio *TBC*. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini utapeleka timu ya wataalamu kwenda kufanya utafiti juu ya usikivu wa redio hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema wamekamilisha kujenga mtambo wa masafa ya redio ya *FM,* sasa ni lini mitambo hii itaanza kufanya kazi katika Visiwa vya Unguja na Pemba ili wananchi wa visiwa hivyo waweze kusikia redio yao ya Taifa ya *TBC*? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya yongeza ya Mheshimiwa Omar Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto, Mheshimiwa Mbunge mimi nakupongeza kwa sababu unafuatilia sana na nikuhakikishie na naomba kutumia Bunge lako Tukufu kuwaagiza wataalamu wetu kwenda mara moja kuona kwamba ni kwa nini baadhi ya maeneo masafa hayajafika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lini itaanza kufanya kazi hii mitambo? Mheshimiwa Mbunge mitambo imeshaanza kufanya kazi, hapa cha kufanya ni kama hivyo wataalamu waende kuona changamoto ipo wapi ili maeneo ambayo hayajapata huduma yaweze kupata huduma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 460

**Hitaji la Kiwanda cha Nyavu Nchini**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kiwanda cha nyavu za uvuvi nchini?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunavyo jumla ya viwanda sita vya nyavu za uvuvi ambapo Ukanda wa Pwani (Dar es salaam) tunavyo viwanda vitatu ambavyo ni *Nyota Venture, Nyamagara Fish Net* na *Quality Nets* na Ukanda wa Ziwa Victoria (Mwanza)

tunavyo viwanda vitatu pia ambavyo ni *Fanaka Fish Net, CFN Mwanza Litimed* na *Ziwa Net Limited*. Aidha, viwanda hivi vinahudumia wavuvi nchi nzima ambapo vinazalisha nyavu za makila *(gillnets)* na nyavu za dagaa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo na idadi hii ya viwanda bado baadhi ya zana zinaagizwa kutoka nje ya nchi kutokana na mahitaji ya soko yaliyopo pamoja na masuala mengine ikiwemo baadhi ya zana kutozalishwa kabisa nchini. Vilevile mahitaji ya zana za uvuvi ni makubwa ukilinganisha na uzalishaji uliopo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea na jitihada za kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya nyavu za uvuvi ili kuweza kutatua changamoto zilizopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anijulishe kwamba hizi nyavu zinazoitwa makokoro zinafanya kazi na zinatia hasara sana wavuvi kwa vile kila wakati zinachomwa. Je, zinatengenezwa wapi na zinaruhusiwa na nani ziwepo nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa vile hiyo ni *CDF* ilikuwa tayari miaka karibu mitano/sita iliyopita kushirikiana na Serikai kuendeleza sekta ya uvuvi; je, ni kwa kiwango gani Serikali imeendeleza mahusiano na Shirika hili la Kimataifa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua makokoro yanatengenezwa wapi?

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hatuna taarifa sahihi kwamba makokoro yanatengenezwa wapi kwa sababu makokoro haya ni zana ambazo zimekuwa zikiingia nchini kinyume cha sheria. Kama kuna kiwanda ndani ya nchi kinatengeneza makokoro basi Serikali haina hiyo taarifa na kama Mheshimiwa Mbunge ana hizo taarifa basi aweze akatusaidia ili tuchukue hatua zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Shirika la Kimataifa, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaendelea na jitihada mbalimbali za kushirikiana na mashirika haya ya kimataifa ambayo yanahusiana na masuala ya uvuvi ili kuendeleza sekta hii ya uvuvi iwe na tija zaidi kwa wavuvi wetu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mbogwe ni wafugaji, waliahidiwa na aliyekuwa Mheshimiwa Waziri mwaka 2022 kuchimbiwa malambo ya kunyweshea mifugo yao na imekuwa ikiingia kwenye bajeti kila mwaka, lakini utekelezaji wake unakuwa haupo. Sasa ni lini Serikali itaenda kuwachimbia malambo wafugaji wa Mbogwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, uchimbaji wa malambo siyo sehemu ya swali la msingi wala majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo utalipeleka kama swali la msingi.

Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa kuwa waathirika wakubwa wa nyavu haramu wamekuwa ni watumiaji ambao ni wavuvi badala ya wafanyabiashara wanaoingiza nyavu hizi. Nini mkakati wa Serikali kuzuia uingizaji wa nyavu hizi haramu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumeendelea kudhibiti uingizaji wa nyavu haramu nchini, lakini kama tunavyofahamu wahalifu wanakuwa na mbinu zao wakati sisi tunajipanga hivi, nao wanajipanga hivi. Tayari tumeshabaini baadhi ya mbinu za wahalifu hawa kuingiza nyavu nchini kwa kutumia mbinu mbalimbali na Serikali imeendelea kuchukua hatua stahiki zinazodhibiti nyavu zisiingie nchini.

Mheshimiwa Spika, mbinu hizo zipo nyingi ambazo tumekuwa tukizitumia ambazo kwa namna hiyo siwezi kuzielezea sana hapa, lakini itoshe tu Mheshimiwa Mbunge aamini kwamba Serikali inafuatilia na kuchukua hatua stahiki ambazo tumekuwa tukichukua katika kudhibiti uingizaji wa nyavu haramu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, sasa aulize swali lake.

Na. 461

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Kibiti**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali kwa sasa inaendelea na utekelezaji wa azma ya kujenga chuo cha ufundi stadi katika kila mkoa na wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 64 kwa wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo vya ufundi stadi pamoja na chuo kimoja cha

Mkoa wa Songwe. Aidha, Wilaya ya Kibiti ni miongoni mwa wilaya hizo 64 ambazo zinajengewa vyuo vya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeshapeleka kiasi cha shilingi 324,694,243.00 pamoja na vifaa vya ujenzi ikiwemo nondo na simenti kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kibiti ambapo ujenzi wa chuo hiki upo katika hatua ya ujenzi wa kuta za boma na ufungaji wa *lintel* pamoja na ukamilishaji wa misingi, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza kabisa tunaipongeza Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inaendelea kufanya na tunakiri kupokea fedha hizo. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni lini sasa kituo hiki kinakwenda kukamilika? *(Makofi)*

Swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuambatana nami ili sasa tuweze kwenda kwenye eneo la tukio kuweza kuona mwendelezo wa mradi huo na Serikali iweze kutoa kauli? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mpembenwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi huu tunaufanya kwa awamu, kwa hiyo kwa awamu ya kwanza tunajenga majengo tisa ambayo ukamilishaji wa majengo haya tunatarajia mwezi Septemba, mwaka huu majengo yale tisa yatakuwa yamekamilika ili basi itakapofika mwezi wa kumi na moja zile *course* za muda mfupi zianze kutolewa.

Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wote kwenye yale majimbo 64 ambayo tunajenga vyuo hivi ifikapo mwezi wa tisa kwa awamu ya kwanza tutakuwa tumekamilisha.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwenye eneo la pili hili la kwenda, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo ndiyo shughuli yetu Wizara ya Elimu, baada ya shughuli hizi za Bunge ni lazima tutembelee miradi hii yote. Kwa hiyo, nipo tayari kufuatana na yeye mara baada ya Bunge hili ili tuweze kuona maendeleo ya mradi ule, lakini na kutatua changamoto zilizopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Mwibara unasuasua, je, chuo hiki kitakamilika lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Kajege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu maswali ya nyongeza ya Maheshimiwa Mpembenwe, ni kwamba ujenzi wa awamu ya kwanza kwa vyuo hivi tunataraji ukamilike mwezi wa tisa mwaka huu na yale mafunzo ya muda mfupi tunatarajia kuanza mwezi wa kumi na moja. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Kajege tutahakikisha kwamba itakapofika mwezi wa tisa Chuo hiki cha Mwibara kinakamilika ili mafunzo yaanze kutolewa mwezi wa kumi na moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa yuko tayari tutembelee Mradi wa *VETA* Kiteto ili tukague kwa siku ambazo siyo nyingi sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kufuatana na Mheshimiwa Olelekaita kwenda kule Kiteto kwa ajili ya kuona maendeleo ya mradi na kutatua changamoto zilizopo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilipewa Chuo cha *Kyela Polytechnic* zaidi ya miaka mitatu sasa, je, nini mpango wa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali dogo la Mheshimiwa Jumbe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulipokea hiki chuo na hivi sasa Mamlaka yetu ya Ufundi Stadi *(VETA)* inaratibu taratibu za makabidhiano ili basi kiweze kuendeshwa na Serikali haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Halmashauri ya Moshi Vijijini ina Majimbo mawili na majimbo haya mawili yana idadi ya watu zaidi ya 500,000, Jimbo la Vunjo liko mbali sana na Moshi Mjini ambako kuna kituo au kuna Shule ya *VETA*. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha *VETA* kwenye Mji Mdogo wa Himo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Kimei, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kujibu kwenye maswali ya msingi, vyuo hivi kwa awamu ya kwanza tulikuwa tunajenga katika ngazi ya Wilaya na awamu ya pili hivi vyuo 64

tumekwenda kujenga kwenye Wilaya ambazo zina Jimbo zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya ukamilishaji wa awamu hizi zote mbili kwa hatua inayofuata sasa tunaweza kuangalia yale maeneo ambayo yana idadi kubwa ya watu ili tuweze kusogeza huduma karibu ya maeneo hayo likiwemo na eneo hilo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Wilaya ya Kishapu ina Chuo cha *VETA* ambacho kimekamilika na kimeanza kufanya kazi, lakini hakina usafiri wowote maana yake gari kwa ajili ya Mkuu wa Chuo; ni lini Serikali italeta gari kwa ajili ya chuo chetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli katika Wilaya ya Kishapu katika ujenzi wa awamu ya kwanza ya Vyuo vya *VETA* tumeweza kujenga chuo pale katika vile vyuo 25 na vimeanza kutoa huduma. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kama tulivyofanya ujenzi kwa awamu, vilevile utekelezaji au uendeshaji wa majukumu wa vyuo hivi unakwenda kwa awamu.

Kwa hiyo, tumeweka bajeti katika mwaka ujao wa fedha wa 2024/2025 kwa ajili ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia yakiwemo magari. Tunaamini wakati wa utekelezaji wa bajeti hiyo ya mwakani tunakwenda kupeleka gari katika Wilaya hii ya Kishapu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, Chuo cha *VETA* Ulyankulu ndiyo chuo kinachotumika kama Chuo cha Wilaya ya Kaliua, lakini chuo hicho kimechakaa na hata hakina karakana za kutosha.

Je, ni lini sasa chuo chetu kitafanyiwa ukarabati angalau kiwe kina hadhi ya Chuo cha *VETA* kwani kwa sasa hadhi kiliyonayo hata *FDC* haifai? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Migilla, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Migilla, tunafahamu uwepo wa vyuo hivi ambavyo ni chakavu au ni vya muda mrefu na tumeendelea kuvifanyia ukarabati. Katika bajeti yetu ijayo ya mwaka 2024/2025 kama ukiipitia vizuri, tumeweka bajeti kwa ajili ya ukarabati, vilevile kuongeza majengo kwenye baadhi ya vyuo ikiwemo na chuo hiki cha Ulyankulu.

Mheshimiwa Spika, nikuondoe hofu na wasiwasi na niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge wote ambao wana Vyuo vya *VETA* vile vya zamani ambavyo vinahitaji ukarabati na kuongeza miundombinu tutakwenda kufanya hivyo. Mheshimiwa Rais tayari alishaagiza na sisi tulishaweka kwenye bajeti tutakwenda kufanya hivyo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 462

**Kupunguza Kodi kwenye Vifaa vya Mazoezi**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza kodi kwenye vifaa vya mazoezi kwa kuwa mazoezi ni tiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya mwaka 2014 kama ilivyofanyiwa marekebisho mbalimbali, imeainisha msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* katika kipengele cha 6(1) na Jedwali la Misamaha lililopo kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148. Bidhaa au huduma zilizopewa msamaha wa kodi ya *VAT* ni pamoja na vifaa vinavyotumiwa kwa ajili ya tiba.

Mheshimiwa Spika, msamaha kwenye vifaatiba vya mazoezi *(physiotherapy)* hutolewa kwa hosiptali zilizosajiliwa na kuidhinishwa na Waziri wa Afya ambapo hupatiwa msamaha wa kodi kwa lengo la kuboresha afya kupitia mazoezi ambayo ni njia bora ya kuzuia magonjwa na kuboresha ustawi wa jumla wa jamii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaonesha kabisa Serikali ime-*base* sana kwenye mazoezi ya tiba, lakini tunafahamu vifaa vya mazoezi viko vingi na mazoezi ni kinga ya magonjwa.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa vyote vya mazoezi hasa vifaa kinga?

Swali la pili, kwa kuwa Sheria ya Kodi imeainisha vifaa vya mazoezi na ime-*base* kwenye vifaatiba, je, Serikali haioni haja ya kufanyia marekebisho sheria hii ili iongeze vifaa vya mazoezi vingine ambavyo havipo kwenye vifaatiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili na kuhamasisha mazoezi kwa ajili ya afya zetu. Swali lake la kwanza na swali la pili naomba uniruhusu nijibu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba ushauri wake umechukuliwa na unaenda kufanyiwa kazi. Serikali sasa hivi ipo katika mchakato wa ukusanyaji wa maoni na hatimaye kutunga sheria baada ya kupelekwa Bungeni, ila nimwombe hofu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wenzangu kwamba kwa sasa tuangalie zaidi vyanzo vya ukusanyaji wa mapato kuliko kupunguza mapato ya nchi hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Ngorongoro swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Catherine Magige.

Na. 463

**Ujenzi wa Barabara ya Sale – Kigongoni**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE K.n.y. MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Sale – Kigongoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Sale – Mto wa Mbu, eneo la Kigongoni yenye urefu wa kilometa 168 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sasa maandalizi ya ujenzi

yanaendelea kwa sehemu ya Mto wa Mbu (Kigongoni) – Selela yenye urefu wa kilometa 23, Selela – Engaruka kilometa 27 na Engaruka – Ngaresero kilometa 25. Kwa sehemu zilizobaki za Engaruka – Ngaresero (kilometa 35) na Sale – Ngaresero (kilometa 58), Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesema kuwa barabara ipo kwenye matengenezo, lakini barabara hii ambayo iko kwenye matengenezo imeshaharibika kutokana na mvua kubwa ambayo imekuwa ikiendelea kunyesha.

Swali la pili, kwa kuwa uharibifu wa barabara ni kubwa sana kwa nchi nzima, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inaanza kujenga upya barabara hizo zilizoharibika kwa kiwango cha juu sana ili tatizo hili lisije likatokea tena? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni barabara ambayo imeharibika na inapita kwenye maporomoko mengi sana hasa eneo la Mlima Oldonyo Lengai kumekuwa na uharibifu mkubwa sana, lakini vipande vile tulivyovitaja ni kwamba vimeshapata kibali na tuko kwenye hatua za manunuzi kwa maeneo yale yote matatu ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami yale maeneo yote korofi na yalikuwa pia ni maelekezo ya viongozi wa kitaifa akiwepo Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo mengine ambayo yamebaki kwa kuwa mvua imeisha, tutaendelea kuyakarabati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara zingine zote nchini, tumelijibu hapa kwamba tulifanya kazi kwanza kurejesha mawasiliano na sasa hivi Serikali tumeshapata tathmini ya uharibifu wa barabara mikoa yote na Serikali inajipanga sasa kwenda kuijenga ili kuirudisha katika hali iliyokuwepo kama ilivyokuwa hapo awali, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nangurukulu - Liwale ni barabara iliyotajwa kwenye bajeti hii inayotekelezwa leo. Wananchi wa Liwale wanataka kujua barabara hii inaanza lini ujenzi wake kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hiyo ipo kwenye bajeti na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama tulivyoahidi tutaanza eneo ambalo ni eneo korofi kwa kujenga kwanza kwa lami kilometa 11, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nyakato - Sitiri mpaka *Igombe TX* kilometa 18 ina miaka saba sasa inajengwa na haijakamilika. Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni kweli imeanza kujengwa kwa muda mrefu, lakini barabara ambazo tunazijenga kwa awamu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuijenga ili kuikamilisha na bado mwaka ujao wa fedha tumetenga fedha kwa ajii ya kuendelea kuijenga ili tuweze kuikamilisha barabara yote hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Kolandoto – Munze kwenda Mwamngongo ipo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Je, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kesho tutasoma bajeti na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, barabara aliyotaja ni kati ya barabara kuu *(trunk roads)* ambazo zipo kwenye mpango kuanzia Kolandoto - Mwamngongo hadi Lalago ambayo tuna uhakika kwenye mpango wa bajeti huu tumeiingiza ili iweze kupata kibali na kuanza kujengwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ipogolo mpaka Kilolo inaunganisha majimbo matatu ya Iringa Mjini, Kalenga na Kilolo na mkandarasi yuko *site*. Ni kwa nini sasa barabara ya kutoka Kilolo - Kibaoni mpaka Kidabaga isijengwe pia kwa lami kwa sababu malori yamekuwa yakikwama kwa muda mrefu sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tu nikubali kwamba eneo alilolitaja la kuanzia Kilolo kwenda Kidabaga hii barabara bado ni ya changarawe. Ni kweli pia kwamba tumeshaanza kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Ipogolo hadi Kilolo ambayo pia ilikuwa ni kero sana. Sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kutoka Kilolo pia tuweze kuunganisha hadi Kidabaga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 464

**Changamoto ya Maji Kata ya Lipwidi - Mtwara Vijijini**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya maji katika Kata ya Lipwidi, Mtwara Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kata ya Lipwidi ina jumla ya wakazi 6,687 waishio katika vijiji vitatu vya Lipwidi, Mtama pamoja na Nambela. Katika kuboresha huduma ya maji katika kata hiyo, Serikali imekamilisha usanifu wa Mradi wa Maji Lipwidi utakaonufaisha wananchi wapatao 17,821 waishio katika vijiji 18 vya Wilaya ya Mtwara vikiwemo vijiji vyote vya Kata ya Lipwidi.

Mheshimiwa Spika, mradi huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 na kukamilika ndani ya miezi 24 ambapo utahusisha upanuzi wa mradi mkubwa wa maji wa Makonde kwa kutoa maji kwenye tanki la lita 1,000,000 linaloendelea kujengwa katika Kijiji cha Nyundo. Kazi zitakazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 400,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 121.2, ujenzi wa nyumba ya mitambo pamoja na ujenzi wa vioski 39 na vituo 19 vya kuchotea maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha inawatua ndoo kichwani akina mama wa Tanzania. Je, ni lini sasa Serikali mtafanya iwezekanavyo katika kutatua changamoto hii ya maji katika Kata ya Lipwidi kwa sababu ipo kwa muda mrefu?

Swali langu la pili, ni nini mkakati wa Serikali wa kutumia chanzo cha maji cha Bwawa la Kitere ambalo liko karibu kuhakikisha mnamaliza changamoto hii ya maji ambayo ipo kwa muda mrefu katika Kata hii ya Lipwidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwatumikia vema wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini na kwa kuendelea kutoa ushirikiano na kushirikiana na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba inamtua mama ndoo kichwani na ndio maana katika bajeti yetu ya Wizara ya Maji tulitoa visima 900 ambavyo vinaenda kujengwa nchi nzima na kila Mbunge anapata visima vitano, ni katika hizo harakati za kuhakikisha tunamtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika suala la bwawa ambalo ameliongelea, Serikali inapokea na tutaendelea kufanya tathmini kuangalia namna gani bwawa hilo litakuwa na msaada, kama tukiona kwamba litakuwa na msaada basi tutahakikisha kwamba tunatumia chanzo hicho ili tuhakikishe kwamba tunawaletea maji katika vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviongelea, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Umechanganya mambo hapo, nawaza Mheshimiwa Zungu akikusikia.

Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, je, ni lini Serikali itamaliza kabisa changamoto ya maji katika Kata ya Chitete na Kata ya Chilulumo katika Jimbo la Momba? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba Mheshimiwa Juliana Shonza amekuwa mstari wa mbele kuwapambania wanawake wa Mkoa wa Songwe hivyo na sisi tunaendelea kuhakikisha kwamba tunashirikiana naye kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, katika vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja tayari viko katika mpango wetu wa utekelezaji wa bajeti ya 2024/2025. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

Na. 465

**Changamoto ya Kubambikiwa Bili za Maji**

**MHE. AMINA ALI MZEE K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za kisheria kwa watumishi wa Mamlaka za Maji nchini wanaowabambikia wananchi bili kubwa za maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Jimbo la Chumbani, kama ifuatavyo:- *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kumradhi ni Jimbo la Chumbuni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji imeanzisha madawati na vituo vya huduma kwa wateja kwa Mamlaka zote za Maji na Usafi wa Mazingira nchini ambapo huwa na jukumu la kupokea taarifa za hali ya huduma, maoni, ushauri au malalamiko ikiwemo ya bili za maji kutoka kwa wateja na wadau mbalimbali. Baada ya malalamiko kupokelewa kupitia dawati hilo, huchunguzwa na ikibainika ni kweli basi wahusika huchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kupewa onyo, kusimamishwa au kufukuzwa kazi kwa mujibu ya sheria, kanuni na taratibu zilizopo kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika kukomesha kabisa changamoto ya ubambikiwaji wa bili za maji kwa wananchi, Serikali pia imebuni mfumo ambao pamoja na mambo mengine unahusika kusimamia ankara za maji zinazotolewa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini. Mfumo huo unafanya kazi kwa kumshirikisha mteja wakati wa usomaji wa dira za maji, kumtumia ujumbe mfupi wa maneno *(sms)* mara usomaji unapofanyika ukionesha usomaji wa sasa, usomaji wa mwezi uliopita na kiasi cha matumizi yake ya maji kwa mwezi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujumbe huo pia humtaka mteja kuhakiki usomaji huo kabla ya ankara yake kuandaliwa na ikiwa hajaridhika au kuhitaji ufafanuzi, basi huwasiliana na namba ya huduma kwa mteja kwa ajili ya ufafanuzi.

Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kuharakisha matumizi ya dira za malipo ya kabla *(pre-paid water meters)* ili kupunguza au kuondoa kabisa kadhia ya kuwabambikia wananchi bili za maji kwani watakuwa wakilipia kadiri wanavyotumia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kelele zimezidi nadhani hata ninyi mnajisikia. Narejea tena humu ndani wako wageni na watu waliokuja kujifunza kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge ambao mnapaswa kwanza kuliheshimu Bunge lenu kabla hamjamdai mtu mwingine heshima hiyo.

Mheshimiwa Amina Ali Mzee, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Serikali kwa wanaotumia *postpaid meter* kujipimia matumizi ya maji wenyewe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, ni gharama gani ambayo inatumika sehemu moja na sehemu nyingine juu ya kupima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeingia kwenye mkakati wa kufunga *prepaid water meter*. Pia mkakati huo unaendana sambamba na kuhakikisha kwamba *postpaid meters* ambazo ni *mechanical meters* tunaanza kuziondoa. Vilevile tunaziondoa kwa namna ambayo *postpaid meters* na *prepaid meters* ni *utilities property* ambazo zinakuwa na gharama zake. Pia tayari nyingine zimekwishakuwa *purchased* na nyingine zimekwishafungwa kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuwezi kwenda kufungua moja kwa moja na kuziondoa, ni lazima twende hatua kwa hatua wakati tunakwenda mbele, basi huku zinazoharibika kwa wengine tunazi-*replace,* lakini baadaye tunaamini kwamba kwa utaratibu huo tutakuja kukamilisha na kuhakikisha kuwa wananchi wote tumewafungia *prepaid water meter.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; gharama zinatofautiana, unaweza ukakuta kwamba Dar es Salaam *unit* au

*(M³)* ni shilingi 2,000; Dodoma, Turiani na Gairo inaweza ikawa tofauti. Haya yote yanatokana na njia ya uzalishaji wa zao la maji. Kama tumezalisha kwa umeme wa kutumia Gridi ya Taifa, umeme wa jua au tumetumia uzalishaji kwa kutumia maji ya mserereko gharama zake zitakuwa tofauti na ndiyo maana unaweza ukakuta kwamba gharama zinatofautiana kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 466

**Uhitaji wa Visima vya Maji Arumeru**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itachimba visima virefu vya maji maeneo ya Maruvango, Kituo cha Afya Mareu, Sakila, Ngyan na Nkoaranga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Programu ya Uchimbaji wa Visima 900 imekamilisha utafiti wa maji ardhini *(Hydrogeological Survey)* katika Vijiji vya Maruvango, Mareu, Sakila, Ngyan, Nkoaranga pamoja na Kituo cha Afya Mareu ambapo uchimbaji wa visima unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2024 na kukamilika mwishoni mwezi Agosti, 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushuru tena na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Naona kwenye majibu mmesema kazi hii itakamilika

mwishoni mwa mwezi Agosti. Ombi letu, hiyo ahadi itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mradi wa maji unaogusa Kata za Embaseni, Maji ya Chai, Kikatiti hadi Samaria unatekelezwa kwa kusuasua sana, je, ni lini mradi huo utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge Dkt. Pallangyo kwa kuendelea kushirikiana na kufuatilia mradi huu. Ni kweli mradi huu ni mkubwa wa shilingi bilioni 8.8 na ni mradi ambao unakwenda kugusa vijiji takribani vinane na tayari Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jumaa Aweso, ameelekeza kupeleka fedha shilingi milioni 200 katika Mamlaka ya Maji Arusha ili mzabuni apewe na aanze kusambaza mabomba katika mradi huo kwa vijiji viwili. Pia nakuhakikishia kwamba Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya vijiji vingine ambavyo vimebaki ili kuhakikisha kwamba Mradi huu unakamilika kwa wakati, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, ukakae kiti cha nyuma kidogo, kwa sababu nimesimama hapa kwa muda nawasubiri mkae.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali na sasa nitaleta matangazo.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na ...

Mheshimiwa Munira, nimesimama nisikilize.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika ndiyo tutakaoanza nao; wageni wa Mheshimiwa January Makamba - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Joseph Ntakarutimana - Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EALA);* Balozi Dkt. Samwel Shelukindo - Katibu Mkuu; Balozi Stephine Mbundi - Katibu Mkuu Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EALA);* Balozi Said Shaib Mussa - Naibu Katibu Mkuu na Balozi Yusuph Mndolwa - Mkuu wa Itifaki, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa hawa wengine wote wameandikwa Kiingereza na tafsiri yake itanipa wakati mgumu hapa.

Katibu wa Bunge, wakati mwingine waandikwe kwa Kiswahili ili tuweze kuwa tunatumia aidha Kiswahili au Kiingereza. Sasa hawa wengine watatajwa kwa Kiingereza kwa sababu ndiyo vyeo vilivyoandikwa hapa kwa sababu la sivyo itanichukua muda kutoa tafsiri.

*We have His Excellence Ricardo Ambrosio Sampaio Mtumbuida - High Commissioner of Mozambique; Her Excellence Chen Mengjian - Ambassador of Peoples Republic of China; His Excellence Isaac Njenga - High Commissioner Republic of Kenya; Mr. Mark Bryan Schereiner - Country Representative UNFPA; Ms. Epiphanie Buzizi - Charge d'Affairs of Rwanda; Mr. Manoj Verma - Charge d'Affairs of India; Ms. Shy- Rose Bhanji - Counsellor Agha Kan, Mr. Sergei Logachev - Minister Counsellor - Russia; Ms. Katherine Gifford - Deputy Representative UN Women; Mr. Amr Selim - Counsellor Arab Republic of Egypt; Mr. Kim Jong Jin - Counsellor - Democratic People of Republic of Korea, sounds like there is something wrong, but good to see you. (Makofi)*

*Ms. Godfrida Magubo - UK Head Office Dodoma.* Haya hawa wameandika Kiswahili, ahasante. *(Makofi)*

Ndugu Rabia Abdalla Hamid - Katibu wa CCM - *NEC* – Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi -

Mwenyekiti wa Bodi – Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, Balozi Aziz Mlima - Mwenyekiti wa Mabalozi Wastaafu, Balozi Luteni Jenerali Abdulrahaman Shimbo - Balozi Mstaafu, Bwana Joseph Kahama - Katibu wa Chama cha Kirafiki cha Tanzania na China, Balozi Bertha Semu Somi - Katibu wa Mabalozi Wastaafu na Balozi Began Taj - Mwenyekiti wa Bodi ya *AICC*. *(Makofi)*

Wapo pia Mheshimiwa Angela Kizigha - Mwenyekiti – *EALA Tanzania Chapter* (huyu ni Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki); Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Maghembe (Mbunge) - Katibu – *EALA Tanzania Chapter*; Mheshimiwa Ansar Kachwamba - Mbunge *EALA;* Mheshimiwa James Kinyasi Millya - Mbunge *EALA;* na Mheshimiwa Machano Ali Machano Mbunge *EALA*. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Salim Kikeke - Mhariri Mkuu *Crown Media*. *(Makofi)*

Haya hao walikuwa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Sasa tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine; tunao wageni 90 wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambaye ni Naibu Waziri…

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Felista Njau, Mheshimiwa Matiko, bado nimesimama natangaza.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 90 wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Taasisi ya Vijana ya Sisi Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Maxmilian Likombom, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wageni hawa ni viongozi wa *Tk Movement* kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 52 wa Mheshimiwa Stephen Byabato ambaye ni Naibu Waziri wa Afrika Mashariki na hawa ni Wenyeviti, Makatibu Wenezi wa Kata na Wajumbe wa Kamati ya Siasa wakiongozwa na Naibu Meya wa Manispaa kutoka Bukoba Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambaye ni Afisa Kilimo Wilaya ya Tarime. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambaye ni Kada wa CCM kutoka Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Asha Juma ambao ni ndugu zake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambao ni wapigakura wake kutoka Buchosa. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni Watendaji Kata kutoka Makete. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 13 wa Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ambao ni Shirika la Madawa Asili na Ulinzi wa Mazingira kutoka Jijini Dar es Salaam. Pia Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro anao wageni wengine watatu ambao ni Taasisi ya *Tanzania Diaspora Global Council* kutoka nchi za Australia, Uingereza na Ujerumani na wageni wengine watano wa Mheshimiwa Ruhoro ambao ni viongozi wa Shirika la *The Right Way* la Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Deus Sangu ambao ni Makada wa Chama kutoka Jimbo la Kwela, Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Makada wa CCM kutoka Mkoa wa Iringa na Dar es Salaam. Pia tunao wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kutoka *Venny Company Real Estate* ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza ni wanafunzi tisa wa *Masters in International Relations* kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 40 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi ya *The Southern Highlands School* kutoka Mafinga, Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao na wengine watakaopata nafasi ya kuingia humu ndani pia tutawatangaza.

Sasa tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninatumia Kanuni ya 76 kupata mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inajibu swali namba 455 ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate aliyetaka kujua ni kwa nini Serikali isilete mabadiliko ya kanuni ikionesha kwamba kila mwaka kunakuwa na uchaguzi wa Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa majibu ya Serikali ni kana kwamba hakuna tatizo, lakini mimi kama Mbunge na wenzangu naona kuna tatizo kwa sababu kila mwaka ukifanya uchaguzi wa Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti maana yake watu hawa ili wachaguliwe wanafanya siasa katika majimbo. Wanapoteza muda mwingi sana badala ya ku-*concentrate* kupanga mipango ya maendeleo wanafanya kazi ya kujihami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona ni muhimu nikapata mwongozo wako, kwa nini kama hawawezi kufanya uchaguzi kila baada ya miaka mitano, wafanye hata miaka minne na nusu, ili angalau huyu Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti ama Naibu Meya akishachaguliwa ajielekeze katika kumsaidia Mwenyekiti wake au Meya wake kupanga mipango ya halmashauri kuliko kila mwaka kuwa na habari ya uchaguzi? Uchaguzi ukienda kwenye vyama watu wanagawanyika kwenye halmashauri na *competence* inakosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba mwongozo wako katika jambo hili kwa sababu hatutakwenda kubadilisha sheria, ni Waziri tu wa TAMISEMI kutunga Kanuni ya Uchaguzi wa Halmashauri zetu halafu linaisha ili watu wafanye kazi ya kuwaletea wananchi wetu maendeleo badala ya kugombana na kutafuta vyeo kila mwaka, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba mwongozo wako kwa kupitia kanuni ya 53(1) kuhusu maswali kujibiwa kikamilifu na Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jibu langu la nyongeza kwa swali namba 460 sikuridhika na majibu ya Waziri ambaye katika swali la nyongeza nilitaka kujua kwamba ni viwanda gani ama viko wapi vinavyotengeneza makokoro ambapo hizi nyavu zimekuwa zikileta hasara kubwa sana kwa wavuvi kila wakati zinapokuwa zinaharibiwa? Nilitaka kujua ili nione Serikali inachukua hatua gani kuwasaidia wavuvi ili wasiingie hasara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Waziri katika majibu yake anataka mimi ndiyo nimsaidie kutafuta hivyo viwanda vipo wapi. Sasa naomba mwongozo wako, hivi Serikali na mimi ambaye sikujua na nilitaka nijue majibu na sikujibiwa. Serikali na mimi ni nani anatakiwa asaidie kupata majibu ya tatizo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako maana wao wanao watendaji, tuna vyombo vya usalama katika mikoa yetu na maafisa wa uvuvi katika mikoa yetu. Sasa wao kama hawajui na wala hawaoneshi kwamba anahatua mbalimbali anazochukua kutafuta haya makokoro yanatengenezwa wapi anategemea mimi nipate taarifa kutoka wapi? Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Waitara hapa kwa mujibu wa kanuni yetu ya 76 akitaka mwongozo kuhusu majibu yaliyotolewa kwenye swali namba 455 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Janejelly Ntate.

Waheshimiwa Wabunge, hoja yake ameieleza kwa kirefu, sina haja ya kuielezea, lakini Bunge hili limeshawahi kutoa mwongozo ambao unaongelea kuhusu majibu kutolewa kwa usahihi, lakini pia maswali kujibiwa kikamilifu. Ni kwamba mwuliza swali ndiye anayetakiwa kuomba mwongozo kuhusu swali fulani. *(Makofi)*

Hata hivyo mwongozo aliouomba Mheshimiwa Waitara ameuomba kwa sura ambayo haiashirii kwamba majibu yaliyotolewa hayaendani na swali, ameomba mwongozo kwa maana ya hilo jambo lenyewe.

Sasa kanuni zetu zinazungumzia kuhusu ukiomba mwongozo unataka kujua jambo hilo kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyoyatoa niliyoyasikia hapa na yale majibu ya msingi ukiyasoma anasema, watakapowasikia wadau wengi wanataka hivyo Serikali itafanya mabadiliko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani Waheshimiwa Wabunge na sisi hapa ni sehemu ya hao wadau, kama tunaona hiyo ndiyo njia bora

tuendelee kuishauri Serikali ili Serikali iweze kuchukua hatua. Kwa hiyo, kwa maana ya jambo hilo kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi, majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri inaruhusiwa kujibu kwa namna yeye alivyoona, lakini kwamba Bunge litatoa mwongozo gani ama Kiti kitatoa mwongozo gani kwenye jambo hili, kwa majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa majibu hayo yanaruhusiwa tuendelee kutoa ushauri kama tunaona jambo hili kwa utafiti tuliofanya tumejiridhisha kwamba wawe wanachaguliwa. Wakichaguliwa Meya na Naibu Meya waende kwa miaka mitano na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti waende kwa miaka mitano, tukijiridhisha hivyo basi tufanye kazi hiyo. Kwa sababu tunayo Kamati yetu hapa ambayo inasimamia TAMISEMI wao watalitazama hili jambo kwa mapana zaidi ili waone kama iko sababu ya kubadili.

Pia amesimama Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka kuhusu majibu yaliyotolewa kwenye swali lake la msingi na baadaye kwenye maswali yake mawili ya nyongeza aliyoyauliza. Swali mojawapo la nyongeza alilouliza lilikuwa linahusu viwanda viko wapi ili kuwaondolea adha wale wananchi ambao hawatengenezi wao nyavu na badala yake wananunua zile nyavu dukani ama popote wanaponunua halafu wanakwenda kuzitumia. Huko sasa ndiko wanakokamatwa na nyavu zile zinachomwa na kwa hivyo wanapata hasara.

Sasa ameomba mwongozo, ametupeleka kwenye Kanuni ya 53 inayohusu maswali kujibiwa kikamilifu kwa sababu anataka kujua, kwa kutumia kanuni ya 76 kama majibu aliyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri yanaruhusiwa au hapana, ya kumwambia yeye kwamba kama anayo hiyo taarifa aipeleke. Kwa sababu wakati akiendelea kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge ameeleza kwamba Serikali inayo mikakati na mikakati mingine haiwezi kusemwa hapa, japokuwa alikuwa hajibu swali lako. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa maana ya kujibu kwa sehemu ya kwanza, ni kweli anaweza kuuliza kama Mheshimiwa Mbunge anazo taarifa za ziada ili ampe na azifanyie kazi. Kwa sehemu ya pili, kwa sababu mimi ndiye niliyeombwa mwongozo, Mbunge alitaraji kwamba Serikali pengine inafuatilia hao watu, wale walionunua

zile nyavu kule walikonunua, kwa sababu kama amenunua dukani maana yake yule mwenye duka ndiye anayejua kiwanda kiko wapi. Kwa hiyo, Serikali inaweza kufanya utaratibu mzuri baada ya kumkamata huyu mwenye nyavu ambazo haziruhusiwi. Zinaitwa makokoro nadhani, nimeona hapa, ambazo haziruhusiwi basi aulizwe umenunua wapi hizi nyavu.

Sasa Serikali imsaidie kukamata kule alikonunua yule aliyenunua ili tujue kiwanda kiko wapi na kiwanda hicho kisifike mahali ambapo kinaendelea kutengeneza nyavu ambazo zinatuathiri pande zote. Wananchi wanapata hasara kwa sababu wamenunua hizo nyavu dukani na yeye hajui vile vipimo, wakati huo huo Serikali pia inatamani kulinda hivi vyanzo vyetu vya mapato na ili wale samaki waweze kukua kidogo na hivyo tuweze kufika kwenye ule uhifadhi ambao tunautaka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sehemu ya kwanza Mheshimiwa Waziri kile alichojibu alikuwa sahihi, anaweza akauliza kama kuna taarifa za ziada apelekewe, lakini wakati huo huo Serikali ilipaswa kumwambia Mbunge kwamba inachukua hatua kadhaa. Kwa sababu ikisema tu wanaingiza kwa njia za magendo kwa hivyo wananchi wataendelea kupata hasara, lazima Serikali ichukue hatua za ziada kwenye kuhakikisha kuwa wananchi hawa wanalindwa kama ambavyo Mbunge alivyokuwa amekusudia kuwawakilisha hao wananchi ambao ameuliza swali kwa niaba yao.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mwongozo wangu ni kwamba alichokijibu Mheshimiwa Naibu Waziri kinaruhusiwa, lakini alitakiwa kwenda mbali kwa sababu yeye anazungumza kwa niaba ya Serikali, kwamba Serikali inafanya nini kwenye jambo hilo.

Baada ya kutoa miongozo hiyo Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa January Yusuf Makamba, aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji na Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 na lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi mahiri na wa vitendo wenye mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali. Aidha, akiwa mwanadiplomasia namba moja nchini ameendelea kuimarisha uhusiano kati ya nchi yetu na mataifa mbalimbali pamoja na taasisi za kikanda na za kimataifa na kuiletea nchi yetu heshima kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha uongozi wake, Mheshimiwa Rais ametumia diplomasia kwa umahiri wa hali ya juu kulinda na kutimiza malengo ya kiuchumi ya Taifa letu kama inavyojidhihirisha katika maeneo mengi tutakayoyapitia kwenye hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango; Rais wa Zanzibar -

Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; Waziri Mkuu - Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa; na Naibu Waziri Mkuu - Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa utendaji wao mahiri ambapo ushauri wao umemwezesha Mheshimiwa Rais kutekeleza azma yake ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake iliyoeleza kwa ufasaha kuhusu mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka huu wa fedha na mwelekeo kwa mwaka ujao. Vilevile ninawapongeza Mawaziri wenzangu walionitangulia kwa kuwasilisha hotuba zao vizuri mbele ya Bunge lako Tukufu ambazo zimeainisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* ambacho ni chombo kikuu cha maamuzi kinachojumuisha Mabunge duniani kote. Umekuwa mwanamke wa kwanza shupavu katika Bara la Afrika kushika wadhifa huo tangu chombo hiki kianzishwe. Si tu umeipa heshima na sifa njema nchi yetu bali pia umeendelea kuwa kioo cha wanawake na vijana wa Tanzania hususani wa kike na kuwadhihirishia kuwa inawezekana kwao kushindana na kupigania nafasi za uongozi katika taasisi za kikanda na kimataifa. Pia mrejesho tunaoupata ni kwamba kazi hiyo unaifanya vizuri na jinsi unavyoifanya basi unaipa heshima na sifa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na Mwenyekiti wa Kamati yetu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote katika Kamati hiyo kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia na kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuishauri Wizara yetu na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba yetu hii ni kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba cha bajeti kilichowasilishwa kwako, nitatoa muhtasari tu na naomba hotuba kamili iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka huu wa fedha Serikali imesimamia masuala ya uhusiano wa kimataifa kwa kuzingatia misingi saba iliyowekwa katika Sera ya Mambo ya Nje na kwa kuzingatia urithi na maarifa ya waasisi wa Taifa letu na pia kwa kuzingatia miongozo ya mwanadiplomasia namba moja ambaye ni Rais wetu. Kutokana na usimamizi huu mzuri leo hii nchi yetu inasifika, inaheshimika, inaaminika na nchi yetu imejenga ushawishi katika masuala muhimu katika majukwa ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii nchi yetu ni rafiki wa karibu kila nchi duniani, hatuna uadui wala uhasama na Taifa lolote. Tunadumisha ujirani mwema na ni wanachama na washiriki waaminifu katika taasisi za kikanda na kimataifa. Vilevile kutokana na usimamizi mahiri wa Sera yetu ya Mambo ya Nje, nchi yetu imetumia fursa za mahusiano ya kimataifa kusukuma ajenda za maendeleo ya nchi yetu ikiwemo kuvutia uwekezaji na utalii, kupanua biashara na kupata rasilimali za utekelezaji wa miradi yetu ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya siasa, ulinzi na usalama duniani napenda kuripoti kuwa baadhi ya nchi Barani Afrika na ulimwenguni kote zimeendelea kukabiliwa na migogoro inayochagizwa na tofauti za kiitikadi, kudorora kwa uchumi, ugaidi na machafuko ya kisiasa. Hali ya ukosefu wa amani na usalama na umaskini vimeendelea kuwa chanzo cha maelfu ya watu kuyakimbia mataifa yao na hivyo kusababisha ongezeko la wakimbizi na wahamiaji na ongezeko la uhalifu unaovuka mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa upatikanaji wa amani ya kudumu duniani, nchi yetu ya Tanzania msimamo wake ni kuendelea kuunga mkono jitihada za Jumuiya ya Kimataifa za kutafuta amani ya kudumu Barani Afrika na duniani kwa ujumla. Aidha, nchi yetu haitatelekeza jukumu lake la kihistoria la

kuwezesha upatikanaji wa amani katika ukanda wetu na kuchangia ulinzi wa amani kote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina kuhusu hali ya siasa, ulinzi na usalama kimataifa ni kama inavyoonekana katika aya ya 26 hadi ya 43 ya hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa mapato na matumizi kwa mwaka huu wa fedha wa 2023/2024 nao unapatikana katika jedwali namba moja na jedwali namba mbili la hotuba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya msingi ya Wizara ni kusimamia utekelezaji wa sera na kwetu Sera ya Mambo ya Nje. Kutokana na mabadiliko makubwa ya mwenendo wa siasa na uchumi duniani iliamuriwa kwamba kufanyike marekebisho ya Sera ya Mambo ya Nje, hivyo mwezi Agosti mwaka uliopita Wizara ilikamilisha rasimu ya marekebisho ya Sera ya Mambo ya Nje na kuwasilisha rasimu hiyo kwenye Baraza la Mawaziri. Wizara ilielekezwa kukusanya maoni zaidi ya wadau. Kazi hiyo imefanyika na Sera Mpya ya Mambo ya Nje itatolewa katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msisitizo wa Sera yetu ya Mambo ya Nje ni diplomasia ya uchumi. Hata hivyo kwa muda mrefu kumekuwa hakuna mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Ninayofuraha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imekamilisha rasimu ya awali ya mkakati wa kitaifa wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Mkakati huu umeainisha maeneo saba ya kipaumbele ambayo Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine na taasisi za umma itatilia mkazo katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Maeneo hayo ni pamoja na: -

(a) Kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje;
(b) Kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania kutoka nje;
(c) Kuvutia watalii kuja Tanzania;
(d) Kutafuta misaada na mikopo ya masharti nafuu;
(e) Kutafuta fursa za ajira na masomo kwa Watanzania;
(f) Kujenga taswira nzuri ya nchi yetu; na
(g) Kujenga uwezo wa kitaasisi wa Wizara na Wizara na taasisi nyingine ili kusimamia vizuri utekelezaji wa Mkakati wa Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mkakati huu kutaiwezesha Serikali na wadau wote kutambua majukumu yao katika mnyororo wa hatua za kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara iliratibu shughuli mbalimbali zilizowezesha nchi yetu kuingia makubaliano mbalimbali yenye tija kwa Taifa letu. Makubaliano hayo yalikuwa na nia ya kuiwezesha nchi yetu kupata mikopo nafuu na misaada, kuvutia watalii, kupata masoko ya bidhaa zetu, kuvutia uwekezaji na wabia wa aina mbalimbali kwa ajili ya nchi yetu. Maelezo ya kina kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi yanapatikana katika aya ya 54 hadi aya ya 94 ya hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie uhusiano kati ya nchi yetu na mataifa mengine. Kama nilivyoeleza hapo awali uhusiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine duniani umeimarika. Nchi yetu imejiongezea marafiki na imeimarisha urafiki uliokuwepo na nchi mbalimbali. Mafanikio haya yamewezeshwa kwa sehemu moja na ziara zilizofanywa na viongozi wetu wa kitaifa kwenye nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai mwaka jana na Aprili mwaka huu Wizara iliratibu ziara 31 za viongozi wakuu wa kitaifa nje ya nchi. Ziara za viongozi wetu zimeliletea Taifa letu mafanikio makubwa ya kiuchumi. Ninaomba kwa ridhaa yako niyataje machache kama ifuatavyo: -

(a) Ziara hizo zimeimarisha uhusiano kati ya nchi yetu na nchi rafiki zetu na taasisi za kimataifa jambo ambalo linafungua milango ya kuongezeka kwa manufaa ya kiuchumi ambayo nchi yetu inayapata;

(b) Kupitia ziara hizo tumesaini mikataba na makubaliano 78 katika sekta mbalimbali;

(c) Tumefanikiwa upatikanaji wa nafasi za masomo kwa Watanzania;

(d) Upatikanaji wa fursa za ajira kwa Watanzania;

(e) Upatikanaji wa masoko ya mazao ya wakulima wetu;

(f) Upatikanaji wa fedha za miradi ya kimkakati, kwa mfano reli ya *SGR* na Bandari ya Mangapwani, Zanzibar;

(g) Ziara hizo zimewezesha kuvutia uwekezaji katika nchi yetu kiasi cha kufikia dola bilioni 5.7 kwa mwaka uliopita, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa katika historia ya nchi hii;

(h) Pia ziara hizo zimewezesha kuipa Tanzania fursa za kuongoza katika mijadala muhimu ya masuala ya kimataifa yenye maslahi kwa nchi yetu;

(i) Ziara hizo zimewezesha kuvutia utalii kuja kutembelea Tanzania baada ya kupata taswira nzuri ya nchi yetu kutokana na maelezo ya viongozi wetu; na

(j) Wataalamu wa Tanzania kutoka vyuo vikuu na taasisi nyingine kupata fursa ya kubadilishana ujuzi na uzoefu na wenzao katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya ziara hizi ni mengi na nimeeleza kwa kifupi. Mafanikio haya yameelezwa kwa kina katika hotuba za bajeti za kisekta kwa kutambua kwamba utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, vilevile nchi yetu ilipata heshima ya kutembelewa na viongozi wengi kutoka mataifa mbalimbali. Wizara yetu iliratibu na kufanikisha ziara za kikazi na kitaifa za viongozi hao wakuu katika mwaka huu wa fedha unaokwisha na jumla ya ziara hizo ni viongozi 33 wakuu wametembelea nchi yetu. Maelezo zaidi ya nchi na viongozi hao yanapatikana katika aya ya 99 hadi 101 ya hotuba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kusimamia na kuongoza kwa

ufanisi ushiriki wa Tanzania katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuimarika kwa ufanisi katika kusimamia masuala haya na kutokana na hatua ya Mheshimiwa Rais kuiongezea nguvu Wizara kwa kuipatia Naibu Waziri na Katibu Mkuu wanaosimamia masuala ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kufuatia jitihada za kurahisisha biashara ndani ya jumuiya, vikwazo vya biashara visivyo vya kodi baina ya Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki vimeendelea kupungua.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021/2022 vikwazo vinavyoihusu Tanzania vilikuwa 14, lakini hadi Februari mwaka huu, vikwazo hivyo vimekuwa vinne. Kwa sasa tunayo furaha kusema kwamba nchi yetu imeendelea kuwa na urari chanya wa biashara baina yake na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uoga kwamba Tanzania itakuwa soko tu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini kwa miaka mitano mfululizo sisi tumeuza zaidi kwenye nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuliko wao walivyonunua kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, ushiriki wetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na ufanisi uliopatikana katika ushiriki huo umewezesha nchi yetu kunufaika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika Bunge la Afrika Mashariki lilipitisha maazimio matano pamoja na kupitisha Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza ya Fedha katika Jumuiya ambapo pamoja na mambo mengine itawezesha kuimarisha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za jumuiya, maelezo ya kina yapo katika aya ya 131 ya hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *SADC,* Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika mtangamano wa *SADC* kwa lengo la kusimamia maslahi ya Taifa na kuzitumia fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii katika Jumuiya hiyo adhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mnamo mwezi Agosti mwaka huu, miezi mitatu kuanzia sasa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atakuwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama wa *SADC*. Nafasi hii itaiwezesha nchi yetu kuratibu, kusimamia na kuongoza majadiliano na maamuzi yote yanayohusu masuala ya siasa, ulinzi na usalama katika jumuiya hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha nafasi hii itaiwezesha nchi yetu kuimarisha ushawishi wake katika ukanda huu katika masuala haya muhimu ukizingatia kwamba Tanzania ni mmoja wa waasisi wa *SADC* na pia ilishiriki kwa hali na mali katika harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa *SADC* nchi yetu imekuwa mstari wa mbele katika kujitolea na kuitikia wito wa kuchangia juhudi za kuimarisha amani na usalama katika ukanda. Hatua hiyo inaenda sambamba na utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo ya Nje ambayo inayapa kipaumbele masuala ya amani na usalama pamoja na ujirani mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi kwa kuzingatia mkataba wa pamoja wa ulinzi wa *SADC* na kufuatia maombi ya Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Tanzania iliungana na nchi nyingine wanachama wa *SADC* kupeleka misheni ya ulinzi wa amani *DRC* mwezi Disemba mwaka jana kwa lengo la kurejesha hali ya usalama mashariki mwa Congo. Pamoja na kuchangia katika misheni hii ya amani, Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za kidiplomasia za kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro wa Mashariki mwa Congo kupitia michakato ya Nairobi na Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Tanzania inashiriki kikamilifu katika harakati za kuimarisha hali ya usalama katika Jimbo la Cabo Delgado nchini Msumbiji kupitia misheni ya ulinzi na usalama ya Msumbiji *(SAMIM)*. Tangu kuanzishwa kwa misheni hiyo mwezi Julai, 2021 nchi husika zimefanikiwa kudhibiti kwa kiasi kikubwa matukio ya ugaidi. Misheni hii inaisha mwezi Julai mwaka huu baada ya kukamilika kwa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia aya ya 147 na 161 ya hotuba yetu, tumeripoti kazi zilizofanywa na Wizara za kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi, Umoja wa Afrika na Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika. Ushiriki wa Tanzania katika jumuiya hizo umekuwa na manufaa makubwa kwa nchi yetu na ningependa nitaje baadhi ya manufaa ambayo nchi yetu imeyapata kwa kushiriki kwenye Umoja wa Afrika na hizi jumuiya nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Tanzania imechaguliwa kuhudumu muhula wa pili wa ujumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha mwaka 2024 – 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa makofi hayo naomba ninywe maji. Waheshimiwa Wabunge, mnaruhusiwa kuendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Tanzania imepata heshima ya kuwa mwenyeji wa Maadhimisho ya Miaka 20 ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika ambayo yalifanyika juzi jijini Dar es Salaam. Pia Tanzania imeweza kuwa mwenyeji wa kongamano la pili la wanawake na vijana katika biashara katika Eneo Huru la Biashara la Umoja wa Afrika lililofanyika Disemba mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumeweza kupitisha Itifaki ya Wanawake na Vijana katika biashara katika eneo hili huru ambapo Rais wetu ni kinara wa uhamasishaji wa wanawake na vijana Barani Afrika ambalo lilifanyika mwezi Februari mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kampuni 11 za Tanzania zimeanza kufanya biashara chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika. Vilevile fursa za kutangaza na kuvutia uwekezaji katika uchumi wa bluu na kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Nchi Mwambao wa Bahari ya Hindi katika kuimarisha usalama na ulinzi wa rasilimali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikiano wa kimataifa; Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika mwezi Disemba mwaka jana katika Umoja wa Falme za Kiarabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pembezoni mwa mkutano huo Rais wetu alizindua programu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wanawake Barani Afrika. Programu hiyo inalenga kusaidia wanawake Barani Afrika hususani wanaoishi vijijini kupunguza matumizi ya nishati zinazozalisha hewa ukaa na yenye athari hasi kwa mazingira na afya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia uzinduzi wa programu hii, Rais wetu alipewa heshima ya kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano Kilele wa Kimataifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika uliofanyika mwezi Mei huko Paris, Ufaransa. Miongoni mwa matokeo ya mkutano huo ni pamoja na kutolewa ahadi za fedha kiasi cha dola bilioni 2.2 kwa ajili ya kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Paris ambao ulihudhuriwa na Marais mbalimbali na wakuu wa taasisi mbalimbali duniani ulipongeza na kutambua mchango mahiri wa Rais wetu ambaye sasa anatambuliwa kama kinara wa ajenda ya nishati safi ya kupikia kote duniani. Nachukua fursa hii kumpongeza Rais wetu kwa heshima kubwa aliyoiletea nchi yetu katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Disemba 2023 Wizara ilifanikisha Tanzania kusaini Mkataba wa Ubia baina ya Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific na Umoja wa Ulaya ambao utatumika kama nyenzo ya kisera na kisheria kuratibu uhusiano wa kiuchumi uliopo kati ya pande hizi mbili kwa kipindi cha miaka 20 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba nchi yetu imepata mafanikio makubwa sana kutokana na ushiriki wake wa mikataba ya aina hii ambapo miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni ongezeko la mauzo ya biashara katika soko la Umoja wa Ulaya

ambapo yalifikia dola za Kimarekani milioni 910 kwa mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Tanzania ilipokea uwekezaji wa moja kwa moja wa zaidi ya dola bilioni 3.4 kutoka Umoja wa Ulaya na zaidi ya *Euro* bilioni 2.3 za msaada kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini kwetu na kusogeza huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *diaspora*; Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa *diaspora* katika mchango wa maendeleo ya Taifa letu. Mathalani, mwaka jana peke yake *diaspora* wa Tanzania walituma fedha nyumbani za kiasi cha dola za Kimarekani milioni 751.6. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeamua kujumuisha masuala ya *diaspora* katika Sera ya Mambo ya Nje na Sera mpya ya Ardhi na hivyo kutoa hadhi maalumu *(special status)* kwa raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania ili kuwapa haki na upendeleo mahsusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itakamilisha mchakato huu wa hadhi maalumu katika mwaka ujao wa fedha. Katika kutekeleza hili, Serikali itawasilisha katika Bunge hili linaloendelea muswada wa mabadiliko ya sheria utakaokuwa na marekebisho madogo ya Sheria za Uhamiaji na Sheria za Ardhi ili hatimaye kuwezesha sasa Serikali kutoa hadhi maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kwamba Serikali itakamilisha mchakato wa kutoa hadhi maalumu katika mwaka ujao wa fedha, lakini mwaka huu wa kalenda pale ambapo Bunge hili litapitisha mabadiliko madogo ya Sheria za Ardhi na Sheria za Uhamiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara pia inasimamia uendelezaji wa miradi mbalimbali ya majengo ya Wizara kule Mtumba, Dodoma; Mahakama ya Afrika, Arusha na Kituo cha Uhusiano cha Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim kule Dar es Salaam. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Wizara inaishukuru Kamati yetu ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa msukumo na

ushauri katika utekelezaji wa miradi hii kwa haraka na ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara imeendelea kuratibu masuala ya haki na kinga kwa jumuiya ya wanadiplomasia hapa nchini kama ilivyoainishwa katika sheria za kimataifa. Katika kuimarisha uhusiano na jumuiya ya wanadiplomasia hapa nchini, Wizara imeendelea kuimarisha utaratibu wa mashauriano katika utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ya maendeleo. Katika kipindi hiki, Wizara kupitia idara yake ya itifaki iliratibu uwasilishaji wa Hati za Utambulisho kwa mabalozi wa nchi mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha tunakwenda sambamba na maono na matarajio ya Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, mnamo mwezi Aprili mwaka huu tulifanya kikao na Mabalozi wote wa Tanzania wanaoiwakilisha nchi yetu nje ya nchi, ma-*counsellor* wakuu, wakuu wa utawala na fedha katika balozi zetu pamoja na menejimenti nzima ya Wizara, tulifanya mkutano wa faragha huko Kibaha, Mkoani Pwani uliokuwa na azma kuu ya kujitathmini na kuweka mikakati ya pamoja ya kuboresha utendaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkutano huo ulipata heshima ya kumsikiliza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alituhutubia na kutoa maelekezo mahsusi kuhusu utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kufuatia kikao hicho, Wizara imeanzisha utaratibu mpya wa kupima utendaji kazi wa mabalozi wetu nje ya nchi ili kuhakikisha kwamba uwakilishi wa nchi yetu kupitia balozi zetu unaleta mchango unaopimika kwa malengo ya nchi yetu. Mfumo huo ambao watu wengine wanauita *KPI (Key Performance Indicators)* utaanza kutumika katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa balozi za hapa nchini kuhamia hapa Dodoma. Wizara imeendelea kuhamasisha balozi za mataifa mbalimbali zilizopo nchini na mashirika ya kimataifa kuhamia Makao Makuu ya Serikali Dodoma. Napenda kulitaarifu

Bunge lako Tukufu kwamba mpaka sasa jumla ya balozi na mashirika mbalimbali zimefungua ofisi zake hapa Dodoma na tunaendelea kuzihamasisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu na upekee wa Wizara yetu hii katika mchango wa maendeleo ya nchi yetu, Mheshimiwa Rais aliamua kuunda kamati maalum iliyokuwa na jukumu mahsusi ya kufanya tathmini ya ufanisi na utendaji kazi wa Wizara yetu hii. Lengo lake ilikuwa ni kubaini mapungufu yanayokwamisha au kupunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo iliyoundwa na wajumbe waliobobea katika tasnia ya diplomasia ilitoa mapendekezo katika maeneo matatu ambayo ni kujenga uwezo wa Wizara katika rasilimali watu; kufanya maboresho ya muundo wa Wizara na kuimarisha uwakilishi na kuboresha mazingira ya kazi hususani ukarabati wa majengo na uendelezaji wa viwanja vya Serikali nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia mapendekezo ya kamati hiyo Wizara iliunda kamati ya ndani ya kujitathmini ambayo ripoti yake iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na baadaye kwenye Baraza la Mawaziri. Aidha, katika hatua ya kuboresha muundo wa Wizara na kuongeza ufanisi, kama nilivyoeleza awali, Mheshimiwa Rais aliteua Naibu Waziri na Katibu Mkuu wanaoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki mahsusi. Vilevile Wizara yetu imehuisha muundo wake ili kukidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya utekelezaji wa mapendekezo ya kamati hii hususani uendelezaji wa milki za Serikali nje ya nchi, Serikali imetoa kibali kwa Wizara kuendeleza viwanja na majengo yaliyopo nje ya nchi kwa kutumia njia mbadala ikiwemo ubia kati ya Serikali na sekta binafsi, hati fungani na karadha. Lengo la utaratibu huu ni kupunguza utegemezi wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali katika ujenzi wa ofisi na makazi ya mabalozi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yetu, inamiliki majengo na viwanja 111 nje ya Tanzania. Katika baadhi ya

maeneo, viwanja hivi vipo katika maeneo mazuri katika majiji mikubwa. Huko nyuma tulikuwa tunategemea fedha za Serikali kujenga vitega uchumi katika majiji ya Nairobi, Abuja, Kampala, Kinshasa lakini Serikali sasa imetoa kibali kwamba tutafute njia mbadala ili Tanzania na yenyewe iwe na majengo makubwa katika majiji mbalimbali duniani ambayo yanaingizia nchi yetu fedha za kigeni. Kwa hiyo, tuna furaha kwamba kazi hiyo tumeianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba; katika kuboresha utendaji wa chuo chetu cha Diplomasia ili kiweze kutoa mchango unaohitajika, Mheshimiwa Rais amekubali jina la chuo hicho sasa kiitwe Dr. Salim Ahmed Salim.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inaenda sambamba na kumuenzi huyu mwanadiplomasia nguli Nchini Tanzania na kote duniani. Kufuatia hatua hiyo, niliunda kamati ya wanadiplomasia nguli na wabobezi wakiongozwa na Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki na Balozi Dau kufanya mapitio na tathmini ya kina ya chuo hiki ili kubaini maeneo yanayohitaji magezuzi na maboresho ili kufikia azma ya nchi na Rais wetu kukifanya chuo hiki kiwe bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeanza mazungumzo ya kimkakati na marafiki zetu kuhusu uwezeshaji wa chuo hiki. Moja ya marafiki ambao tumeanza nao mazungumzo kuhusu chuo hiki ni Serikali ya China ambapo juzi nilikuwa huko na bahati nzuri balozi Chen Mingjian yuko hapa na yeye anasikia kwa hiyo, ni jambo ambalo tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha unaokwisha, Wizara yetu iliidhinishiwa shilingi 17,887,608,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kayi ya fedha hizo shilingi 8,400,000,000 ilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo kwenye balozi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba; hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu Wizara imepokea na kutumia fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali kiasi

cha shilingi 16,762,726,958.61 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,780,120,117 zimeelekezwa katika ukarabati wa majengo na ununuzi wa samani katika balozi sita za nje ya nchi. Vilevile, Wizara imeendelea na ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi wetu kule Washington DC ambapo mkandarasi tayari amelipwa anaendelea na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inaendelea na miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo manne katika ubalozi wetu kule Pretoria Afrika ya Kusini na kuanza mchakato wa ujenzi katika eneo letu la ubalozi wa Adiss Ababa kule Ethiopia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Wizara yetu imeingia Makubaliano ya Ubia na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kitega uchumi la Ubalozi wa Tanzania jijini Nairobi. Jengo hilo litakuwa jengo pacha lenye ghorofa 22 katikati ya jiji la Nairobi. Vilevile, tunajenga jengo la ghorofa 25 katikati ya jiji la Kinshasa kwa ushirikiano na NSSF. Kadhalika, Serikali kupitia Wizara inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya majengo ya Wizara pamoja na vitega uchumi katika viwanja vya Serikali vilivyopo Kampala, Uganda; Abuja, Nigeria na Lusaka, Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Lusaka peke yake, tuna viwanja 11 ambavyo viko katikati ya jiji la Lusaka na tunaanza ujenzi wa majengo ya vitega uchumi katika jiji hilo la Lusaka katika mwaka huu wa fedha unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mpango madhubuti wa kuendeleza viwanja na milki zake zilizopo nje, Serikali imeunda timu maalum ya wataalam, iliundwa na Katibu Mkuu Kiongozi, ikiwa na jukumu la kuishauri Serikali kuhusu namna bora ya kuendeleza na kusimamia milki hizo nje ya nchi, kazi hiyo inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia taasisi zilizoko chini yake kwa lengo la kuhakikisha zinafikia malengo ya

kuanzishwa kwake. Katika kipindi hiki, taasisi hizo zimetekeleza majukumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha *(AICC)*. Kituo hiki ni taasisi inayojiendesha kwa faida pasipo kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Majukumu ya Kituo hiki ni kuendesha biashara ya mikutano na upangishaji wa nyumba na ofisi kwa taasisi na watu binafsi. Vilevile, Kituo hiki kinatoa huduma ya afya kupitia hospitali zake.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kukujulisha kwamba kituo hiki katika mwaka wa fedha unaokwisha, kimehudumia mikutano 320 ya kitaifa, mikutano 23 ya kimataifa ambapo ilileta washiriki 82,436 Kitaifa na washiriki 22,104 wa kimataifa. Vilevile, Bodi iliomba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kufanya ukaguzi maalum wa hesabu za kituo hiki ambapo masuala mbalimbali yalibainika na yaliyopelekea kusimamishwa kazi kwa watumishi sita ikiwemo Wakurugenzi watatu na Wakuu wa Vitengo vitatu na kazi ya kurekebisha uendeshaji wa taasisi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inasimamia, kama nilivyoeleza awali, Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim na kazi zake zinazofanyika nimezieleza.

Mheshimiwa Spika, tulikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa bajeti hii inayokwisha, changamoto na hatua zilizochukuliwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana, zimeelezwa kwa kirefu kuanzia aya ya 254 na 255 ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu vipaumbele, malengo na majukumu ya kuzingatiwa katika mwaka wa fedha unaokuja. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yetu imejipanga kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji ili kuhakikisha kwamba tunatoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya Taifa letu na kutimiza azma ya Mwanadiplomasia namba moja katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa tija, ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imeandaa mpango

mahususi wa utendaji kazi kwa kutumia viashiria vya matokeo, kama nilivyowaeleza au *KPI* ambao utaanza kutumika katika mwaka ujao wa fedha. Mpango huu utaainisha vipaumbele vya Serikali, Mpango Mkakati wa Wizara na uhalisia wa eneo la uwakilishi. Aidha, mpango huu utawezesha Mabalozi wetu na Wakuu wa Idara na Vitengo, kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia shabaha zilizoainishwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imejipanga kuimarisha sauti ya Tanzania katika Jumuiya ya Kimataifa ili kuimarisha zaidi hadhi na heshima ya nchi yetu katika anga za Kimataifa. Tutahakikisha kwamba katika majadiliano, mikutano ya kimataifa tunazungumza, tunapiga kura au kuamua kwa kuongozwa na maslahi ya nchi yetu. Vilevile kwa kuzingatia sera ya mambo ya nchi yetu, lakini vilevile sera yetu ya kutofungamana na upande wowote. Aidha, nchi yetu itaongeza ushiriki katika majukwaa yanayojadili masuala ya kidunia ikiwemo masuala ya kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha unaokuja, Wizara itaweka msisitizo mkubwa zaidi katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi na kuhakikisha kwamba ushirikiano wetu na nchi nyingine na taasisi za kimataifa, unaleta tija na manufaa thabiti katika uchumi wa nchi yetu. Hivyo basi, Wizara yetu itashirikiana na Wizara za kisekta na wadau wengine kuhakikisha kwamba tunatoa mchango kwenye kukuza uwekezaji, kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, kuvutia watalii, kuongeza ajira na fursa za masomo ya Watanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuongeza viwango vya misaada na mikopo ya masharti nafuu na kuimarisha taswira ya nchi yetu kwa ujumla. Sambamba na hayo, Tanzania ni mwanachama wa taasisi, mashirika na jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa. Uanachama huo una faida mbalimbali kwa nchi yetu ikiwemo faida za kiuchumi, faida za kiufundi na ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia uanachama huo Watanzania wanapata nafasi za ajira katika ngazi za wataalamu na uongozi. Vilevile, nchi yetu inapata kushiriki katika Bodi za Uongozi za taasisi na mashirika hayo hivyo kuwa na ushawishi

katika maamuzi ya kisera yanayopitishwa. Ninaomba kutoa rai kwa Watanzania wote wenye sifa ikiwemo Waheshimiwa wa Bunge letu Tukufu, kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika taasisi za kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hapa, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, kwa kujitokeza kuwania nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani kwa Kanda ya Afrika. Ninapenda kulitaarifa Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeridhia ugombea huo wa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, na hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Dkt. Ndugulile yuko Geneva na Mheshimiwa Waziri wa Afya. Sisi Wizara tumeunda timu ya kampeni pale inazunguka naye Bara zima la Afrika kuhakikisha ushindi unapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru, tayari tumeungwa mkono na *SADC* nchi 16 na tunaamini Jumuiya ya Afrika Mashariki itatuunga mkono nchi saba ukiondoa sisi. Kura ziko 47, kwa hiyo tayari tuna mtaji wa karibia nusu ya kura zote, naamini tutashinda. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia ugombea huo na kutoa maelekezo thabiti ya kuhakikisha kwamba ushindi unapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ni mwanzo tu, Serikali kupitia Wizara yetu itaendelea kuhamashisha Watanzania wengi wagombee nafasi katika taasisi kubwa za kimataifa na tutawapigania kuhakikisha kwamba wanashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa *agenda* ya Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni kinara wa uhamasishaji wa *Agenda* hii ya Nishati Safi ya Kupikia kwa akina mama kama nilivyoeleza hapo awali. Kwa kuzingatia hatua hizo, katika mwaka wa fedha ujao, Wizara imejiwekea vipaumbele, malengo na majukumu yafuatayo, na ningependa kuyasoma:-

(i) Tumepanga kushamirisha kuliko ilivyowahi kutokea huko nyuma, Diplomasia ya Uchumi ili kuchochea uwekezaji, kukuza utalii, kuongeza biashara pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia

maendeleo ya nchi yetu. Hicho ni kipaumbele na malengo ya kwanza ya Wizara yetu;

(ii) Tutakuza ushirikiano wa uwili wa kimkakati *(Strategic Bilateral Relations)* pamoja na kuhakikisha kwamba ushiriki wa tija wa Watanzania katika jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa ili kulinda maslahi mapana ya Taifa pamoja na kustawisha diplomasia ya kisasa na kujenga uhusiano wa karibu zaidi na nchi washirika;

(iii) Kuifanya Tanzania kuwa na ushawishi na kuwa kinara kwa nchi nyingine katika masuala mtambuka kwenye jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa ili Tanzania ikisema isikilizwe, Tanzania ikisema iheshimike;

(iv) Tutaongoza na kushiriki katika jitihada za kikanda na za kimataifa za kudumisha amani, ulinzi na usalama ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inabaki kuwa kioo cha amani na usalama kote duniani; na

(v) Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi, kuimarisha utawala bora na rasilimali watu ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi ya ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi, makazi ya watumishi na vitega uchumi katika Balozi za Tanzania pamoja na Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, shukurani, ninapenda kwa heshima kubwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Uongozi wake umeifanya nchi yetu iendelee kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa na diplomasia ya nchi yetu kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau na washirika wa maendeleo, jumuiya za kikanda na kimataifa na kuhakikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, napenda kuzishukuru sana nchi zote rafiki, mashirika yote ya kikanda na kimataifa ambayo tumefanya nayo kazi vizuri. Tumeendelea kushirikiana vizuri kama ambavyo inaonekana katika Aya ya 256 hadi 260 ya hotuba yetu na kama ambavyo mmeona baadhi

yao wamekuja kutuunga mkono kwa uwakilishi hapa siku ya leo kama walivyotajwa na Mheshimiwa Spika. Ni dhahiri kwamba, ushirikiano wao kwa Serikali yetu umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara yetu na taasisi zilizopo chini ya Wizara yetu. Kwa kipekee, nawashukuru sana Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Naibu Waziri; Mheshimiwa Wakili Msomi Stephen Byabato, Naibu Waziri; Mheshimiwa Dkt. Samwel Shelukindo, Balozi na Katibu Mkuu; Mheshimiwa Balozi Stephen Mbundi, Katibu Mkuu vilevile; Mheshimiwa Balozi Said Shaib Mussa, Naibu Katibu Mkuu; na Wakuu wa Taasisi zote. Bibi Christine Mwakatobe kutoka *AICC*; Ndugu Lamau Mpolo kutoka *APRM*; na Ndugu Felix Wangwe kutoka *CFR* kwa kazi nzuri sana na menejimenti, Wakuu wa Vitengo wote kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kuhakikisha kwamba Wizara yetu inatimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Mabalozi wa nchi yetu wanaoiwakilisha Tanzania, wanafanya kazi nzuri na wengi mnawaona na wakati mwingine katika mazingira magumu. Tunawashukuru sana kwa weledi, ufanisi na umahiri na moyo wa uzalendo na kujitoa, kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu huko waliko.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuhitimisha kwa kusema kwamba, dunia ya sasa ni dunia ya ushindani na wote tunafahamu. Nchi hushindania watalii, biashara, uwekezaji, rasilimali za maendeleo, teknolojia na maarifa tupo katika ushindani. Kushindana na kushinda katika zama hizi za ushindani, kunahitaji mambo kadhaa. Kunahitaji maarifa ya wanadiplomasia, rasilimali za kuwezesha kutekeleza majukumu yao, lakini kunahitaji pia ushawishi wa nchi kwa ujumla ili tuweze kushinda.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Tanzania, tumejipanga kushindana na kushinda katika dunia hii ya ushindani, uwezo na maarifa tunayo. Nchi yetu ni kubwa na ina historia adhimu. Saa nyingine tunajichukulia kinyonge lakini Tanzania ni nchi kubwa, ina

historia adhimu, inaheshimika. Katika dunia hii ya ushindani, lazima tushindane na kushinda katika masoko, katika watalii, katika mitaji, katika teknolojia na katika maarifa, lazima tushindane na kushinda. Bahati nzuri tunazo silaha mbalimbali lakini moja ya silaha yetu kubwa ni Jemedari wetu na Mwanadiplomasia namba moja, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia hii siyo ya ushindani tu, lakini pia ni dunia ya ushirikiano vilevile. Lazima mataifa yaje pamoja na kutatua changamoto za pamoja za kidunia, iwe ni mabadiliko ya tabianchi, iwe ni umaskini, iwe ni nishati ya kupikia na mambo mbalimbali; iwe ni kupambana na magonjwa, kupambana na ugaidi, ulinzi na usalama. Pia ni dunia ya ushirikiano na ni dunia ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tumejipanga kushindana na kushinda, lakini pia tumejipanga kushirikiana na wenzetu kwa ukamilifu na kutoa mchango wetu kama sehemu ya familia ya mataifa. Wajibu huo tutautimiza na tutailinda hadhi na heshima ya Tanzania kwa wivu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamaliza kwa kusema kwamba, ili kuwezesha sasa kutekeleza kwa kikamilifu majukumu ya Wizara kama nilivyoyaeleza katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 241,099,232,000. Kati ya fedha hizo shilingi 229,435,856,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 11,633,376,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninamaliza tena kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu, nasimama hapa kwa mara ya kwanza katika nafasi hii ya Waziri wa Mambo ya Nje, kwa kuniamini niweze kumsaidia kama Mwanadiplomasia namba mbili. Ni heshima kubwa sana kuweza kuifanya kazi hii, tunashukuru sana. Mimi na wenzangu vilevile Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Byabato, Dkt. Shelukindo, Mheshimiwa Balozi Mbundi na Mheshimiwa Balozi Shaib Mussa, tunapata bahati kubwa sana ya kupata miongozo ya mara kwa mara, maelekezo ya mara kwa mara ili kutimiza malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo bahati kwamba, katika kipindi hiki ambapo Tanzania imefunguka sisi ndiyo tumepewa heshima ya kufanya kazi hii. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kwa ushirikiano wako na Bunge lako, na kwa ushirikiano wa wenzetu Serikalini na Watanzania wote kwa ujumla, kazi hii tutaifanya kwa weledi na uadilifu mkubwa. Hadhi, sifa na heshima ya Tanzania itaendelea kupanda mbele na mbele na mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge kuja kuwasilisha maoni ya Kamati, wako wageni ambao tuliwatangaza lakini kulikuwa na makosa kidogo kwenye uchapaji. Tunaye Balozi Stephen Mbundi ambaye ni… aah! mbona mmemwita tena, haya. Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia Afrika Mashariki, karibu sana. *(Makofi)*

Alitambulishwa kama Katibu Mkuu wa Bunge la Afrika Mashariki lakini yeye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia mambo ya Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, ninamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake anakuja kusoma Mheshimiwa Joseph Tadayo. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH A. TADAYO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama,

ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha hali ya mahusiano ya kimataifa kwa kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu sita, sehemu ya kwanza ikiwa ni sehemu ya utangulizi, sehemu hii inatoa maelezo ya jumla kuhusu msingi wa muundo wa taarifa. Sehemu ya pili inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge; sehemu ya tatu hadi ya nne zinafanya uchambuzi wa utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na kuchanganua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano inaonesha maoni na ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi. Aidha, sehemu ya sita na ya mwisho inakamilisha taarifa kwa kutoa shukurani na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, msingi wa uchambuzi wa Kamati; Msingi wa Kamati kuchambua makadirio ya Wizara ya Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni masharti ya kifungu cha 6(3) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Bunge. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za

Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba naliomba Bunge hili lijadili hoja ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya taarifa; taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi iliyochambuliwa inagusa Fungu moja la kibajeti ambalo ni Fungu 34. Baada ya kutambulisha mawanda ya taarifa, naomba kuisoma taarifa hii kwa muhtasari ili kuendana na muda pasipo kuathiri mtiririko wa maudhui. Hata hivyo, kwa umuhimu wa kumbukumbu kamili naomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa mezani mapema leo hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara wa Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, Jijini Dar es Salaam. Mradi huu ni moja ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi; wakati Kamati inatembelea mradi tajwa ilielezwa kuwa mradi unatekelezwa na Mkandarasi *Corporation Sole Works Superintendent* ambayo ni Kampuni ya Serikali chini ya Wizara ya Ujenzi. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa mwezi Machi, 2023 na kwa mujibu wa ujenzi ni miezi 12 kwa gharama ya shilingi 4,450,359,568.80. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi, ujenzi ulikuwa umefikia 18% na muda wa ujenzi wa miezi 12 ulikuwa umekwisha. Kamati haikuridhishwa na namna mradi huu unavyotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024; kutokana

na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kasi ya mkandarasi wa mradi ni ndogo sana ambapo kwa miezi 12 amejenga 18%. Ikiwa hali hii itaendelea kama ilivyo mradi utachukua miezi 66 kukamilika suala ambalo litaongeza gharama za mradi. Hivyo ipo haja ya kuchukua hatua za haraka ili mradi uendelee.

(ii) Mkandarasi *Corporation Sole Works Superintendent* ni Kampuni ya Serikali chini ya Wizara ya Ujenzi, mradi unaotekelezwa ni wa Serikali. Mkandarasi hakuwa na maelezo ya kuridhisha kuhusu kasi ndogo ya ujenzi wa mradi, ni maoni ya Kamati kuwa huenda mkandarasi anatoa kipaumbele kwa miradi mingine pasipo kuzingatia mkataba jambo ambalo akiendelea nalo litaathiri kampuni hiyo hata katika kupata miradi mingine hapo baadaye.

(iii) Mradi huu umetengewa shilingi bilioni 3.7 hadi sasa umepokea shilingi milioni 800 kutokana na kasi ndogo ya mkandarasi. Ikiwa imebakia miezi mitatu mwaka wa fedha kuisha ni wazi fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi haziwezi kutumika katika mwaka huu wa fedha, hali hiyo ni wazi itahathiri utekelezaji wa mradi na mpango wa Wizara.

(iv) Kutokana na mkandarasi na mshitiri kuwa taasisi za umma, Kamati ina maoni kuwa pande zote mbili ziweke mpango kazi unaotekelezeka ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024; uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 1 cha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti uliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024; ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi bilioni 1.55 kati ya fedha hizo shilingi 150,000,000 ni makusanyo ya makao makuu ya Wizara na shilingi bilioni 1.4 ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi milioni 781.55 sawa na 60.12% ya lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo ya Wizara kwa kipindi cha kufikia Februari, 2023 ambapo Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi milioni 528.57 na kubaini kuwa makusanyo ya kipindi hiki yameongezeka kwa shilingi milioni 252.98 sawa na 47% kulingana na uchambuzi. Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kamati ilipochambua taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilibaini kuwa hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 184.13 sawa na 74.3% ya shilingi bilioni 247.97 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha fedha kilichopokelewa ni ongezeko la shilingi bilioni 10.45 sawa na 7% ikilinganishwa na shilingi bilioni 178.68 zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2023. Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo limechangiwa na fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa 97.7% ya kiasi kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia kati ya fedha zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2023/2024 shilingi bilioni 155.17 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha hizo ni sawa na 73% ya shilingi bilioni 213.30 zilizotolewa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 12.20 zilipokelewa kwa ajili ya

mishahara ikiwa ni sawa na 73% ya shilingi bilioni 16.77 zilizotengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kati ya shilingi bilioni 184.13 zilizopokelewa shilingi bilioni 16.76 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na 94% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa fedha hizo zitumike kama ilivyokusudiwa kwa miradi kutekelezwa kwa kuzingatia thamani ya fedha za wananchi ili miradi hiyo iwe na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sura ya uwiano wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na ulinganisho wa fedha iliyopokelewa kufikia Februari, 2024 ni kama inavyoonekana katika katika Jedwali Na. 1 na Chati ya 1.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara; taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba katika kutekeleza majukumu yake Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo.

(i) Uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta binafsi kuhusu diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano na mahusiano ya kimataifa.

(ii) Upungufu wa watumishi katika idara na vitengo ikilinganishwa na mahitaji na majukumu ya Wizara, kwa sasa Wizara ina watumishi 554 wakati mahitaji ni watumishi 779.

(iii) Kutojenga na kuendeleza majengo ya Balozi na vitega uchumi katika Balozi zetu nje ya Tanzania kutokana na ufinyu wa bajeti na sheria kutowezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa changamoto zote zilizotolewa taarifa kuwa ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara wa mwaka 2023/2024 ni zile ambazo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; uchambuzi wa malengo ya bajeti; kabla ya kueleza uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara hii, napenda kutoa taarifa kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vitano tofauti na ilivyokuwa mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo Wizara iliweka vipaumbele 14.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kupunguza vipaumbele na kujikita kwenye vipaumbele vichache na vya muhimu kama Wizara inayohusika na masuala ya Kimataifa. Ni imani ya Kamati kwamba Wizara imejipanga ipasavyo kutekeleza vipaumbele hivyo kwa ufanisi ili kufikia malengo na tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato; Kamati ilipitia makadirio ya ukusanyaji wa mapato yanayopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mapitio hayo yalibaini kuwa Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 1.55. Maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa shilingi milioni 150 sawa na 9.6% ni fedha zinazotarajiwa kukusanywa na makao makuu ya Wizara. Aidha, kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 1.4 sawa na 90% kinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Balozi za Tanzania nje ya nchi. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024 ni sawa na malengo ya makusanyo yaliyowekwa katika mwaka wa fedha unaoishia 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa ni Balozi tano tu za Tanzania nje ya nchi katika Majiji ya Lusaka, Maputo, New York, Paris na Harare ndizo zinatarajiwa kukusanya mapato ya Serikali kupitia pango la nyumba za Serikali.

Balozi hizo pia zilitegemewa kukusanya mapato katika mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa kiasi cha fedha kinachotozwa katika kodi ya pango kwenye baadhi ya nyumba za Serikali zilizo nje ya nchi ni kidogo ukilinganisha na maeneo ambayo majengo hayo yapo katika nchi husika. Hii inatokana na majengo hayo kuchakaa kwani ni ya zamani na pia hayajafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa kina ni matarajio ya Kamati kuwa lengo la makusanyo limezingatia uhalisia pamoja na changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake pamoja na ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 241.09, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 210.92 sawa na 87.5% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; shilingi bilioni 18.50 sawa na 7.5% ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 11.66 sawa na 5% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa bajeti inayoombwa kwa ajili ya mwaka 2024/2025 imepungua kwa 3% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024. Upungufu huo umechangiwa na kupungua kwa bajeti ya maendeleo kwa 34% ukilinganisha na bajeti ya maendeleo iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, sura ya uwiano wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na ulinganisho wake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 inaonekana katika Jedwali Na. 2 na Grafu ya 1.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo imepungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 6.25 sawa na 34%

ikilinganishwa na shilingi bilioni 17.88 iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilikuwa imepokea na kutumia 92% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, tathmini inaonesha kuwa Wizara hii bado inahitaji kufanya ukarabati wa majengo na nyumba za ubalozi ambazo zimechakaa na hivyo kuathiri taswira ya nchi yetu katika medani za kidiplomasia. Hivyo matarajio ya Kamati ilikuwa ni kuona bajeti ya maendeleo ikiongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa Wizara inapotengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo huwa haijumuishi gharama za kubadilisha fedha katika nchi ambayo mradi unatekelezwa. Hali hiyo huathiri malengo ya utekelezaji wa mradi. Mathalani, unapotengewa shilingi bilioni mbili kutekeleza mradi Washington DC, kiasi hicho kinapobadilishwa kuwa dola haiwezi kubakia na thamani ya shilingi bilioni mbili. Hivyo, kuna umuhimu wa kujumuisha gharama za kubadilisha fedha kulingana na nchi mradi unapotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile taarifa iliyowasilishwa na Wizara pia ilionesha kuwa Wizara imepanga kutekeleza miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 343.10 kutoka vyanzo mbadala ikiwemo ubia na taasisi za umma na binafsi za hapa nchini. Miradi hiyo inakusudiwa kutekelezwa katika Balozi za Nairobi - Kenya, Kinshasa - DRC na Lusaka - Zambia. Ni matarajio ya Kamati kuwa miradi ya ubia itazingatia maslahi, faida na manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee maelezo haya yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; maoni ya Kamati; kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo

maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

(i) Kasi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Chuo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim siyo ya kuridhisha, huku mkandarasi akiwa hana maelezo kuhusu kusuasua kwa mradi huo. Kwa kuwa mshitiri na mkandarasi ni taasisi za umma kuna umuhimu wa watendaji wa taasisi hizo kuweka mpango kazi utakaonesha namna bora ya kukamilisha mradi na mkandarasi atoe kipaumbele kukamilisha mradi huo.

(ii) Zaidi ya 70% ya bajeti ya Wizara hii inakwenda kwenye Balozi. Hivyo, kuna umuhimu mabalozi na watumishi kufanya kazi kwa ufanisi ili kufikia tija iliyokusudiwa. Kwa muktadha huo umefika sasa wakati Mabalozi wawekewe vigezo vya utendaji *(Performance Indicators)* za utekelezaji wa majukumu yao.

(iii) Tanzania itakuwa mwenyeji wa michuano ya soka mataifa ya Afrika kwa mwaka 2027. Kwa ukubwa wa mashindano haya kuna umuhimu wa kutumia michuano hiyo kama sehemu ya diplomasia ya umma *(Public Diplomacy)* kwa nchi yetu. *(Makofi)*

(iv) Kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kupeleka watumishi Balozini kwa kutoa kipaumbele kwa Balozi za kimkakati ambazo nchi itanufaika zaidi katika diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

(v) Uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta ya umma na binafsi kuhusu diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano na mahusiano ya kimataifa bado imeendelea kuwa changamoto katika kunufaika na diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

(vi) Mpango wa ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi unakabiliwa na changamoto mbalimbali

ikiwemo ufinyu wa bajeti na sheria kutowezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu, changamoto hizi zinahitaji kufanyiwa kazi ili mpango huo utekelezwe.

(vii) Katika kutekeleza mpango wa ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi Wizara iongeze mawanda na kushirikisha kampuni binafsi na za umma katika nchi ambazo miradi hiyo inatekelezwa. *(Makofi)*

(viii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kiungo baina ya taasisi za umma na binafsi nchini pamoja na taasisi za kimataifa katika masuala yote ya uhusiano wa kimataifa. Mfumo wa mawasiliano uliopo sasa Wizarani hauleti tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hivyo, ipo haja ya kufanya tathmini ya mfumo wa mawasiliano uliopo na kuona namna ya kuuboresha zaidi. *(Makofi)*

(ix) Ziara za viongozi wa juu wa nchi katika nchi nyingine duniani, pamoja na za viongozi wa juu wa nchi nyingine wanaotembelea Tanzania zimekuwa na mafanikio makubwa kiuchumi, kidiplomasia na kijamii. Hivyo, ipo haja ya kuweka mikakati kuhakikisha wananchi wanaelezwa kwa kina faida zitokanazo na ziara hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wa Kamati; Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuutangaza mpango wa ujenzi wa majengo ya kitega uchumi na Ofisi za Ubalozi katika nchi ambazo miradi hiyo inatekelezwa. Kufanya hivyo kutavutia wabia kutoka sekta binafsi na umma katika nchi hizo hivyo kurahisisha utekelezaji wa mpango huo na kupata wawekezaji wenye uwezo na sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, mikataba ya ujenzi wa miradi ya kitega uchumi na Ofisi za Ubalozi katika nchi mbalimbali baina ya sekta binafsi na umma pamoja na mikataba ya uendeshaji wa miradi hiyo iandaliwe kwa umahiri na kuzingatia maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iandae mpango wa kuweka vigezo vya utendaji *(performance indicators)* kwa kila balozi kwa kuzingatia nchi ambayo ubalozi upo. Vigezo hivyo *(performance indicators)* vitumike katika kupima kazi ya balozi. Kufanya hivyo kutasaidia mabalozi kufanya kazi kwa malengo na kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa na hivyo nchi yetu kunufaika zaidi hasa katika eneo la diplomasia ya uchumi na sekta nyingine kwa ujumla. Hili liende sambamba na kuboresha mazingira ya kazi katika balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali iandae mpango mkakati unaotekelezeka ili kumaliza changamoto ya uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta ya umma na binafsi kuhusu diplomasia ya uchumi na fursa zinazotokana na mtangamano na mahusiano ya kimataifa. Kufanya hivyo kutasaidia nchi yetu kunufaika zaidi na fursa zitokanazo na mtangamano na uhusiano wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tano, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara ziandae mkakati wa kupeleka watumishi kwenye Balozi za kimkakati ambazo nchi inanufaika zaidi katika Diplomasia ya Uchumi na nyanja nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sita, Wizara ifanye tathmini mfumo wa mawasiliano uliopo sasa baina ya Wizara, taasisi za umma na binafsi pamoja na taasisi za kimataifa ili kuona namna bora ya kuboresha mfumo wa mawasiliano. Kufanya hivyo kutasaidia kuimarisha mawasiliano na wadau na hivyo kuboresha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali ifanye maboresho ya Sheria za Ununuzi wa Umma; *The Public Procurement Act, The Public Private Partnership Act, The Banking and Financial Institutions Act* pamoja na kanuni zake ili kuwezesha sekta binafsi na ya umma kushiriki kikamilifu katika mpango wa ujenzi wa Ofisi za Ubalozi na majengo ya kitega uchumi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nane, Serikali iandae mkakati maalumu ikiwemo ya kibajeti ambao utatumika kufanya *public diplomacy* (diplomasia kwa umma) kwa nchi yetu kabla na wakati wa

Michuano ya Soka ya Mataifa ya Afrika ya mwaka 2027 *(AFCON 2027)* ambayo yatafanyika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi, Wizara iandae mpango mahsusi wa kueleza mafanikio ya ziara za viongozi wa juu wanazofanya katika nchi mbalimbali duniani, pamoja na za viongozi wengine wanaotembelea nchini. Kufanya hivyo kutasaidia wananchi kufuatilia na kufahamu faida na fursa zitokanazo na ziara za viongozi kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususani katika bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa January Yusuf Makamba (Mbunge), Naibu Mawaziri Mheshimiwa Balozi Nassor Mbarouk (Mbunge) na Mheshimiwa Stephen Byabato (Mbunge) pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi zake kwa wakati. Vilevile naishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (FUNGU 34) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023]***

**SURA YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha hali ya mahusiano ya Kimataifa kwa kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na Diplomasia ya Uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa

hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) (c) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 26 Machi, 2024; kwa ajili ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama inavyoelekeza Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge; kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu: -

- i) Utangulizi;
- ii) Matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- iii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; iv) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na
- v) Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la maelezo hayo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili Bunge liweze kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

## SURA YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja wa Ujenzi wa Vyumba vya Mihadhara Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim Jijini Dar es Salaam. Mradi huu ni moja ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili: -

a) Muhtasari wa maelezo ya mradi uliotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizoziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 2.1 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa;

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ina miradi nane ya maendeleo ambayo ni Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na ukarabati wa Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Pretoria, Afrika ya Kusini, ukarabati wa Jengo la zamani la ubalozi Washington DC, ujenzi wa makazi ya Balozi na jengo la kitega uchumi Adis Ababa, Ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ubalozi na Majengo ya Vitega Uchumi Balozini na ujenzi wa vyumba vya Mihadhara

katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim - CFR. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi Kamati ilifanikiwa kukagua mradi mmoja wa Ujenzi wa Vyumba vya Mihadhara wa CFR. Maelezo kuhusu mradi uliokaguliwa ni kama ifuatavyo;

**2.1.1 Mradi wa Ujenzi Vyumba vya Mihadhara Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim-CFR**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kituo cha Dkt. Salim Ahmed Salim kimetengewa kiasi cha **Shilingi 3,700,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa Vyumba 9 vya Mihadhara.

**2.2 Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa mradi wa maendeleo uliokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa mradi huo, hadi Mwezi Machi, 2024. Wakati Kamati inatembelea Mradi tajwa, ilielezwa kuwa mradi unatekelezwa na Mkandarasi **Corporation Sole Works Superintendent** ambayo ni Kampuni ya Serikali chini ya Wizara ya Ujenzi. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa Mwezi Machi, 2023 na muda wa ujenzi ni miezi 12 kwa gharama ya **Shilingi 4,450,359,568.80/=**. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi, ujenzi ulikuwa umefikia **asilimia 18** na muda wa ujenzi wa miezi 12 ukiwa umekwisha. Kamati haikuridhishwa na namna mradi huu unavyotekelezwa.

**2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

i) Kasi ya Mkandarasi wa mradi ni ndogo sana ambapo kwa miezi 12 amejenga asilimia 18 tu. Ikiwa hali itaendelea kama ilivyo mradi utachukua miezi 66 kukamilika. Suala ambalo litaongeza gharama za mradi. Hivyo ipo haja ya kuchukua hatua za haraka ili mradi uendelee;

ii) Mkandarasi **Corporation Sole Works Superintendent** ni Kampuni ya Serikali chini ya Wizara ya Ujenzi. Mradi

unaotekelezwa ni wa Serikali. Mkandarasi hakuwa na maelezo yakuridhisha kuhusu kasi ndogo ya ujenzi wa mradi. Ni maoni ya Kamati kuwa huenda Mkandarasi anatoa kipaumbele kwa miradi mingine pasipo kuzingatia Mkataba. Jambo ambalo akiendelea nalo litaathiri Kampuni hiyo katika kupata miradi mingine hapo baadae;

iii) Mradi huu umetengewa **Shilingi Bilioni 3.7**, Hadi sasa Mradi umepokea **Shilingi Milioni 800** tu kutokana na kasi ndogo ya Mkandarasi. Ikiwa imebakia miezi mitatu mwaka wa fedha kuisha ni wazi fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi haziwezi kutumika katika mwaka huu wa fedha. Hali hiyo ni wazi inaathiri utekelezaji wa mradi na mipango ya Wizara; na

iv) Kutokana na Mkandarasi na Mshitiri kuwa Taasisi za umma Kamati ina maoni kuwa pande zote mbili ziweke mpango kazi unaotekelezeka ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa kasi.

## SURA YA TATU

## 3.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ilihusu maeneo Makuu matatu.

Maeneo hayo ni: -

i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati; ii) Mapitio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu kama ifuatavyo: -

**3.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa, taarifa ya Mtoa Hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu ya ushauri kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 1*** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu; -

i) Serikali kutoa Fedha za Miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kuzingatia mpango wa Miradi husika. Hadi kufikia Machi, 2024; Wizara ilipokea **Shilingi Bilioni 16.7** sawa na**asilimia 94** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

ii) Kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi; ambapo Kamati ilitaarifiwa kwamba Mkakati huo sasa umekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uzingatiaji wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kuhamasisha kimkakati Sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya nyingine za Kikanda.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla ushauri wa Kamati unaendelea kufanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 3.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

#### 3.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya Maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 1,559,879,000.00/=** Kati ya fedha hizo **Shilingi 150,000,000.00/=** ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na **Shilingi 1,409,879,000.00/=** ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 781,553,856.18/=** sawa na **asilimia 60.12** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo ya Wizara kwa kipindi cha kufikia Februari, 2023 ambapo Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 528,570,756.95/=** na kubaini kuwa makusanyo ya kipindi hiki yameongezeka kwa **Shilingi 252,983,699.23/=** sawa na **asilimia 47.**

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya kamati inaonesha kuwa katika kipindi cha miaka 4 ya fedha Wizara hii haikuweza kufikia lengo la makusanyo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za UVIKO 19. Kulingana na uchambuzi, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni wa kuridhisha.

#### 3.2.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ilibaini kuwa hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi**

**184,136,534,059.29/=** sawa na **asilimia 74.3** ya **Shilingi 247,971,524,000/=** zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kiwango cha fedha kilichopokelewa ni ongezeko la **Shilingi 10,455,741,691.7/=** sawa na asilimia **7** ikilinganishwa na **Shilingi 173,680,792,367.59/=** zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo limechangiwa na fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa kwa **asilimia 93.7** ya kiasi kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini pia, kati ya Fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 **Shilingi 155,172,918,905.68/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha hizo ni sawa na **asimilia 73** ya **Shilingi 213,304,516,000/=** zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha, **Shilingi 12,200,888,195.00/=** zilipokelewa kwa ajili ya mishahara ikiwa ni sawa na **asilimia 73** ya **Shilingi 16,779,400,000/=** zilizotengwa kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kati ya **Shilingi 184,136,534,059.29/= z**ilizopokelewa **Shilingi 16,762,726,958.61/=** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 94** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa fedha hizo zitumike kama ilivyokusudiwa kwa miradi kutekelezwa kwa kuzingatia thamani ya fedha za wananchi ili miradi hiyo iwe na tija kwa Taifa.


**Mheshimiwa Spika,** Sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Mishahara na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na ulinganisho wa fedha iliyopokelewa kufikia Mwezi Februari, 2024 ni kama inavyoonekana katika katika **Jedwali Na. 1** na **Chati Na. 1.**

**JEDWALI NA 1: Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na zilizopokelewa kwa Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| MWAKA | 2023/2024 | | | | % +/- |
|---|---|---|---|---|---|
| AINA YA MATUMIZI | KIASI KILICHOTENGWA | ASILIMIA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA | |
| MISHAHARA (PE) | 16,779,400,000 | 7 | 12,200,888,195.00 | 73 | 7 |
| MENGINEYO (OC) | 213,304,516,000 | 86 | 155,172,918,905.68 | 73 | 84 |
| MAENDELEO | 17,887,608,000 | 7 | 16,762,726,958.61 | 93 | 9 |
| **JUMLA** | **247,971,524,000** | **100** | **184,136,534,059.29** | **100** | **100** |

***Chanzo: randama ya Wizara 2024/2025***

**CHATI NA 1: Uwiano wa Fedha zilizopokelewa kwa Matumizi ya Wizara**




***Chanzo: randama ya Wizara 2024/2025***

### 3.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli, Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Itifaki, kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje, Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Watanzania waishio

ughaibuni, Kuratibu na Kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara, Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa; na kuratibu, kusimamia, kukuza biashara za kimataifa na kusimamia utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilichambua Taarifa za Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) na Kituo cha Mahusiano ya Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini (APRM). Kamati iliridhika na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni;-

i) Uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta binafsi kuhusu Diplomasia ya Uchumi na fursa zitokanazo na Mtangamano na Mahusiano ya Kimataifa;

ii) Upungufu wa Watumishi katika Idara na Vitengo ikilinganishwa na mahitaji na majukumu ya Wizara; kwa sasa Wizara ina Watumishi 554 wakati mahitaji ni Watumishi 779; na

iii) Kujenga na kuendeleza majengo ya Balozi na Vitega uchumi katika Balozi zetu nje ya Tanzania kutokana na ufinyu wa bajeti na Sheria kutowezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa changamoto zote zilizotolewa taarifa kuwa ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara wa Mwaka 2023/2024, ni zile ambazo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuzitatua.

## SURA YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 4.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, napenda kutoa Taarifa kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele Vitano tofauti na ilivyokuwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambapo Wizara ilijiwekea vipaumbele Kumi na Nne (14).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kupunguza Vipaumbele na kujikita kwenye vipaumbele vichache na vya muhimu na kama Wizara hii inayohusika na masuala ya Kimataifa; ni imani ya Kamati kwamba imejipanga ipasavyo kutekeleza vipaumbele hivyo kwa ufanisi ili kufikia malengo na tija iliyokusudiwa.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Mapitio hayo yalibaini kuwa Wizara imeweka lengo la kukusanya Shilingi 1,559,879,000.00/=

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, **Shilingi 150,000,000/=** sawa na **asilimia 9.6** ni fedha zinazotarajiwa kukusanywa na Makao Makuu ya Wizara.

Aidha kiasi kinachobaki cha Jumla ya **Shilingi 1,409,879,000/=** sawa na **asilimia 90** kinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Balozi za Tanzania Nje ya nchi. Uchambuzi wa Kamati ulibaini makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 ni sawa na malengo ya makusanyo ya mwaka wa fedha huu unaoishia yaani 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika Uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa ni Balozi tano (5) tu za Tanzania nje ya Nchi katika Majiji ya Lusaka, Maputo, New York, Paris, na Harare ndizo zinatarajiwa kukusanya mapato ya Serikali kupitia pango la Nyumba za Serikali. Balozi hizo ndizo pia zilitegemewa kukusanya mapato katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 hivyo hakuna Balozi mpya ambazo zinazotarajiwa kuiingizia Serikali mapato kutokana na kodi ya pango.


**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kamati pia ulibaini kuwa kiasi cha fedha kinachotozwa kama kodi ya pango kutokana na upangishaji wa nyumba za Serikali zilizo nje ya nchi ni kidogo sana ukilinganisha na maeneo ambayo majengo hayo yapo katika nchi husika. Hii inatokana na majengo mengi kuchakaa kwani ni ya zamani na pia hayaja karabatiwa kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya uchambuzi wa kina ni matarajio ya Kamati kuwa lengo la makusanyo limezingatia uhalisia pamoja na changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake pamoja na ukusanyaji wa maduhuli.

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 241,099,232,000/=** kati ya fedha hizo **Shilingi 210,926,213,000/=** sawa na **asilimia 87.5** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Shilingi 18,509,643,000/=** sawa na **asilimia 7.5** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 11,663,376,000/=** sawa na **asilimia 5** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika **Chart Na. 2**

**CHATI NA 2: Uwiano wa Fedha zinazoombwa kwa Matumizi ya Wizara**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa, Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Mwaka 2024/2025 imepungua kwa **asilimia 3** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Upungufu huo umechangiwa na kupungua kwa bajeti ya Maendeleo kwa **asilimia 34** ukilinganisha na Bajeti ya maendeleo iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024.


**Mheshimiwa Spika,** Sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Mishahara na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na ulinganisho wake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 inaonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Grafu Na. 1.**

**JEDWALI NA 2: Uwiano wa Aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa Mwaka 2023/2024 na 2024/2025**

| MWAKA | 2023/2024 | | 2024/2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| AINA YA MATUMIZI | KIASI | ASILIMIA | KIASI | ASILIMIA | |
| **MISHAHARA (PE)** | 16,779,400,000 | 7 | 18,509,643,000 | 7.5 | 10 |
| **MENGINEYO (OC)** | 213,304,516,000 | 86 | 210,926,213,000 | 87.5 | -1.1 |
| **MAENDELEO** | 17,887,608,000 | 7 | 11,663,376,000 | 5 | -34 |
| **JUMLA** | **247,971,524,000** | **100** | **241,099,232,000** | **100** | |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024 na 2024/2025***

**GRAFU NA 1: Ulinganisho wa Uwiano wa Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2023/2024 na 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa fedha iliyotengwa kwa ajili ya Maendeleo imepungua kwa kiasi cha **Shilingi 6,254,232,000/=** sawa na **asilimia 34** ikilinganishwa na **Shilingi 17,887,608,000/=** iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa katika mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ilikuwa imepokea na

kutumia **asilimia 92** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, tathmini inaonesha kuwa Wizara hii bado inahitaji kufanya ukarabati wa majengo na nyumba za ubalozi ambazo zimechakaa na hivyo, kuathiri taswira ya nchi yetu katika medani za kidiplomasia. Hivyo matarajio ya kamati ilikuwa nikuona Bajeti ya Maendeleo ikiongezeka.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa Wizara inapotengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo huwa haijumuishi gharama za kubadilisha fedha katika nchi ambayo mradi unatekelezwa. Hali hiyo huathiri malengo ya utekelezaji wa mradi. Mathalani, inapotengwa **Shilingi Bilioni 2** kutekeleza mradi Washington DC, kiasi hicho kinapobadilishwa kuwa Dola haiwezi kubakia na thamani ya **Shilingi Bilioni 2.** Hivyo, kuna umuhimu wa kujumuisha gharama za kubadilisha fedha kulingana na nchi mradi unapotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya miradi minne (4) iliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, miradi miwili ipo katika utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Miradi hiyo inayojumuisha Ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Arusha) na ujenzi wa Vyumba vya mihadhara katika Kituo cha uhusiano wa kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim. Miradi mingine ni pamoja na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi katika balozi za Tanzania na ujenzi wa majengo ya Ofisi na makazi ya watumishi balozi za Tanzania. Ni rai ya Kamati kuwa Wizara itakamilisha taratibu za awali mapema na kuomba fedha Hazina kwa wakati ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa iliyowasilishwa na Wizara pia ilionesha kuwa Wizara hii imepanga kutekeleza miradi ya maendeleo yenye thamani ya **Shilingi 343,100,000,000/=** kutoka vyanzo mbadala ikiwemo ubia na Taasisi za Umma na Binafsi za hapa nchini. Miradi hiyo inakusudiwa kutekelezwa katika balozi za Nairobi-Kenya, Kinshasa-DRC na Lusaka Zambia. Ni matarajio ya kamati kuwa Miradi ya ubia itazingatia maslahi, faida na manufaa kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

## SURA YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

i) Kasi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim sio ya kuridhisha huku Mkandarasi akiwa hana maelezo kuhusu kusuasua kwa mradi huo. Kwa kuwa Mshitiri na Mkandarasi ni Taasisi za Umma kuna umuhimu wa watendaji wa taasisi hizo kuweka mpango kazi utakaonesha namna bora ya kukamilisha mradi huo na mkandarasi atoe kipaumbele kukamilisha mradi;

ii) Zaidi ya asilimia 70 ya Bajeti ya Wizara hii inakwenda kwenye Balozi. Hivyo, kuna umuhimu mabalozi na watumishi kUfanya kazi kwa ufanisi ili kufikia tija iliyokusudiwa. Kwa muktadha huo umefika wakati sasa Mabalozi wawekewe Vigezo vya utendaji (*Perfomance Indicator)* za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi za Ubalozi.

iii) Tanzania itakuwa Mwenyeji wa Michuano ya Soka Mataifa ya Afrika kwa Mwaka 2027. Kwa ukubwa wa mashindano hayo kuna umuhimu wa kutumia michuano hiyo kama sehemu ya *Public Diplomacy* kwa nchi yetu;

iv) Kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kupeleka watumishi balozini kwa kutoa kipaumbele kwa balozi za kimkakati ambazo nchi itanufaika zaidi katika Diplomasia ya Uchumi;

v) Uelewa mdogo kwa wadau ikiwemo sekta ya Umma na Binafsi kuhusu diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na Mtangamano na Mahusiano ya Kimataifa bado imeendelea kuwa changamoto katika kunufaika na Diplomasia ya Uchumi;

vi) Mpango wa ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti na Sheria kutowezesha Sekta binafsi kushiriki kikamlifu. Changamoto hizi zinahitaji kufanyiwa kazi ili mpango huo utekelezwe;

vii) Katika kutekeleza Mpango wa ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi Wizara iongeze mawanda na kushirikisha Kampuni Binafsi na za Umma katika nchi ambazo miradi hiyo inatekelezwa;

viii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kiungo baina ya Taasisi za Umma na Binafsi nchini pamoja na Taasisi za kimataifa katika masuala yote ya Uhusiano wa Kimataifa. Mfumo wa mawasiliano ulipo sasa Wizarani hauleti tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. hivyo ipo haja ya kufanya tathmini ya mfumo wa mawasiliano uliopo na kuona namna ya kuuboresha zaidi;

ix) Ziara za viongozi wa juu wa Nchi katika nchi nyingine duniani pamoja na za viongozi wa juu wa Nchi nyingine wanaotembelea Tanzania zimekuwa na mafanikio makubwa kiuchumi, kidiplomasia na kijamii. Hivyo, ipo haja ya kuweka mikakati kuhakikisha wananchi wanaelezwa kwa kina faida na fursa zitokanazo na ziara hizo.

### 5.2 Ushauri wa Kamati

i) Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuutangaza mpango wa ujenzi wa majengo ya kitega uchumi na ofisi za ubalozi katika nchi ambazo miradi hiyo inatekelezwa. Kufanya hivyo kutasaidia kuvutia wabia kutoka sekta binafsi na umma katika nchi hizo na hivyo kurahisisha utekelezaji wa mpango huo na kupata wawekezaji wenye uwezo na sifa.

ii) Mikataba ya ujenzi wa miradi ya kitega uchumi na ofisi za ubalozi katika nchi mbalimbali baina ya Sekta Binafsi na Umma pamoja na mikataba ya uendeshaji wa miradi hiyo iandaliwe kwa umahiri na kuzingatia maslahi mapana ya nchi.

iii) Serikali iandae mpango wa kuweka vigezo vya utendaji (*Perfomace Indicator)* kwa kila balozi kwa kuzingatia nchi ambayo ubalozi upo. *Performance indicator* hizo zitumike katika kupima utendaji kazi wa Balozi. Kufanya hivyo kutasaidia Mabalozi kufanya kazi kwa malengo na kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa na hivyo nchi yetu kunafaika zaidi katika eneo la diplomasia ya uchumi na sekta nyingine kwa ujumla. Hili liende sambamba na kuboresha mazingira ya kazi katika Balozi zetu.

iv) Serikali iandae mpango mkakati unaotekelezeka ili kumaliza changamoto ya uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta ya umma na binafsi kuhusu Diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na Mtangamano na mahusiano ya kimataifa. Kufanya hivyo kutasaidia nchi yetu kunufaika zaidi na fursa zitokanazo na Mtangamano na uhusiano wa Kimataifa.

v) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara ziandae mkakati wa kupeleka watumishi kwenye Balozi za kimkakati ambazo nchi inanufaika zaidi katika diplomasia ya uchumi na nyanja nyingine.

vi) Wizara ifanye tathmini mfumo wa mawasiliano uliopo sasa baina ya Wizara, Taaasisi za Umma na Binafsi pamoja na Taasisi za Kimataifa ili kuona namna bora ya kuboresha mfumo wa mawasiliano. Kufanya hivyo kutasaidia kuimarisha mawasiliano na wadau na hivyo kuboresha utendaji wa Wizara.

vii) Serikali ifanye Maboresho ya Sheria za Ununuzi wa Umma, *The Public Private Partnership* Act, The Banking *and Financial Institutions Act* pamoja na Kanuni zake ili kuwezesha Sekta binafsi na ya Umma kushiriki kikamilifu katika Mpango wa ujenzi wa Ofisi za Ubalozi na Majengo ya Kitega Uchumi nje ya nchi.

viii) Serikali iandae mkakati maalum ikiwemo wa kibajeti ambao utatumika kufanya *Public Diplomacy* kwa nchi yetu kabla na wakati wa michuano ya Soka ya Mataifa ya Afrika ya Mwaka 2027 (AFCON 2027) ambayo yatafanyika Tanzania.

ix) Wizara iandae mpango mahsusi wa kueleza mafanikio ya ziara za viongozi wa juu wanazofanya katika nchi mbalimbali duniani pamoja na za viongozi wengine wanaotembelea nchini. Kufanya hivyo kutasaidia wananchi kufuatilia na kufahamu faida na fursa zitokanazo na ziara za viongozi kwa nchi.

x) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024.

## SURA YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao Maoni, Ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*: -

1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dr. Alfred James Kimea, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - Mjumbe

14. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Minza Simon Mjika, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. January Yusufu Makamba (Mb), Manaibu Waziri Mhe. Balozi Mbarouk Mbarouk (Mb) na Mhe. Steven Byabato (Mb) pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi yake kwa wakati. Vilevile niishukuru Sekretariat ya Kamati kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, Naunga Mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Vita Rashid Kawawa, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

28 Mei, 2024

**Kiambatisho Na. 1**

**UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

**Maelezo ya Jumla**

Wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambapo maelezo ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri huo ni kama ifuatavyo: -

***(i) Kwa muda wa miaka mitatu mfululizo Wizara imeshindwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati kutokana na kutopokelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Hali hiyo imeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa na hivyo kutofikiwa kwa malengo na tija iliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.***

***1. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kutopokelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo miradi ya Wizara kutokidhi vigezo vya upokeaji fedha vilivyowekwa na Wizara ya Fedha pamoja na vigezo vya wabia ikiwemo sekta binafsi kwa miradi inayotekelezwa kwa kutumia vyanzo mbadala vya fedha. Vigezo hivyo ni pamoja na miradi kukosa nyaraka muhimu kama michoro, gharama halisi za utekelezaji pamoja na maandiko ya miradi hiyo. Katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara imeandaa mkakati wa ujenzi, ukarabati na ununuzi wa majengo ya ubalozini kuanzia mwaka 2023 hadi 2033, ambapo pamoja na mambo mengine mkakati huo umeweka kipaumbele katika kuandaa nyaraka na mahitaji mengine ya miradi ili kuwezesha utekelezaji wake kwa mapema.

***2. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** baadhi ya miradi ambayo Wizara imehakikisha imekidhi vigezo vya kupokea fedha kutoka Wizara ya Fedha ni pamoja na mradi wa ujenzi wa majengo ya makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu - Lakilaki Arusha; mradi wa ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim

Ahmed Salim – Kurasini; mradi wa ukarabati wa nyumba nne (4) za ubalozi wa Tanzania Pretoria; mradi wa ujenzi wa uzio katika viwanja vya ubalozi wa Tanzania Addis Ababa.

***3. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara pia imekamilisha nyaraka muhimu za utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa majengo katika balozi za Nairobi na Kinshasa kwa kutumia vyanzo mbadala vya fedha. Kukamilika kwa hatua hii, kumewezesha Wizara kuingia makubaliano ya kujenga Jengo la Kitega Uchumi katika ubalozi wa Tanzania uliopo Nairobi kwa ubia na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

***4. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara itaendelea kuhakikisha miradi yake inakidhi vigezo vyote vya upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

***(ii) Kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo kutakuwa na tija ikiwa Wizara itakamilisha taratibu za awali kwa wakati ili kuweza kuomba fedha Hazina na Serikali kutoa fedha kwa wakati kuzingatia mipango ya utekelezaji wa miradi.***

***5. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** ushauri huu umepokelewa na Wizara imeanza kuufanyia kazi kwa kuhakikisha taratibu za awali zinakamilishwa kwa wakati ili kuweza kuomba fedha kutoka Wizara ya Fedha. Katika kutekeleza ushauri huo, Wizara imefanikisha uombaji wa fedha za maendeleo kwa wakati kwa mradi wa ujenzi wa majengo ya makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu - Lakilaki Arusha; mradi wa ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim; mradi wa ukarabati wa nyumba nne (4) za ubalozi wa Tanzania Pretoria; mradi wa ujenzi wa uzio katika viwanja vya ubalozi wa Tanzania Addis Ababa na miradi ya ukarabati katika balozi za London, Geneva, Beijing, Ottawa, Brussels, na Stockholm.

***(iii) Kitendo cha kushindwa kuanza ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa miaka 16 tangu kuingia makubaliano husika na Umoja wa Afrika ni hali ambayo ikiendelea, huenda ikatia doa taswira ya nchi yetu kidiplomasia hasa katika Umoja wa Afrika na dunia kwa ujumla.***

***6. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu umeendelea kuwa kipaumbele cha Serikali ikiwa ni utekelezaji wa makubaliano kati yake na Umoja wa Afrika. Ninayo heshima kutoa taarifa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeanza utekelezaji wa mradi huo na tayari mkandarasi kampuni ya *CRJE (East Africa)* Limited kutoka nchini China anaendelea na kazi za ujenzi ambapo anatekeleza mradi huo kwa gharama ya shilingi 62,968,086,187.78 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Aidha, usimamizi wa mradi unafanywa na mshauri elekezi kampuni ya *Aru Built Environment Consulting Company (ABECC)* ya Chuo Kikuu Ardhi kwa gharama za shilingi 2,956,000,000 pamoja na VAT.

***7. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** ujenzi wa mradi ulianza tarehe 28 Agosti, 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 27 Februari, 2025. Hadi kufikia mwezi Machi 2024 kiasi cha shilingi 11,777,968,375.04 kilitolewa na kulipwa mkandarasi kampuni ya *CRJE (East Africa) Limited* ikiwa ni malipo ya kazi za ujenzi wa mradi huo ambao umefikia asilimia 12.2 ya kazi zote za mkataba.

***(iv) Baadhi ya nyumba za makazi ya watumishi katika Balozi mbalimbali zimechakaa na hivyo kuathiri hadhi ya Nchi, Balozi na watumishi wetu katika nchi walizopo.***

***8. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa ukarabati na ujenzi wa majengo balozini ambao umeainisha miradi 15 ya kipaumbele itakayotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi 2026/2027). Mkakati huo umepanga kutumia vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwemo bajeti ya Serikali, mikopo ya masharti nafuu kutoka taasisi za fedha na kwa kuingia ubia na mifuko ya taifa ya hifadhi ya jamii, mashirika ya umma na sekta

binafsi. Baadhi ya miradi hiyo 15 ya kipaumbele ni pamoja na ujenzi wa majengo katika ubalozi wa Nairobi – Kenya (NSSF) na Ujenzi wa majengo katika ubalozi wa Kinshasa – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (NSSF).

***9. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** katika utekelezaji wa mpango huo, Serikali imetenga fedha kutoka mfuko mkuu na kuzielekeza katika ukarabati wa nyumba nne (4) za Ubalozi wa Tanzania Pretoria, mradi wa ujenzi wa uzio katika viwanja vya ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, ukarabati wa Makazi ya Balozi London, ukarabati wa Makazi ya Balozi Geneva, ukarabati wa majengo katika Balozi za Beijing, Ottawa, Brussels, na Stockholm. Kufikia mwezi Februari 2024, jumla ya Shilingi 4,780,120,117 zimekwishatolewa na Serikali na zimetumwa kwenye vituo hivyo kwa kazi za ukarabati.

***10. Mheshimiwa Mwenyekiti***, Aidha, mnamo mwezi Januari 2024 Wizara ilifanya wasilisho katika Baraza la Mawaziri kuhusu uhitaji wa kufanya ukarabati katika Balozi zetu nje ya nchi na Baraza liliridhia hoja hiyo na kuagiza kuanza utekelezaji wake.

***(v) Balozi zetu ni moja ya Ofisi muhimu katika kuutangaza utalii wa nchi yetu. Hivyo ni muhimu ofisi hizo kuwa na mkakati wa kutangaza utalii wa nchi yetu ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais katika kutangaza utalii nakuongeza mapato ya nchi. Ni muhimu sana balozi zetu zikawekewa malengo katika kuutangaza utalii.***

***11. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara kupitia balozi za Tanzania nje ya nchi na kwa kushirikiana na wadau wengine zikiwemo wizara za kisekta hususan Wizara ya Maliasili na Utalii, taasisi za umma na sekta binafsi zimeendelea kutangaza fursa za utalii zilizopo nchini kupitia Mpango Mkakati wa Wizara kama hatua muhimu ya kutekeleza Mpango wa Serikali katika kutangaza utalii na kutekeleza Diplomasia ya Uchumi. Aidha, Balozi zetu zinatekeleza mipango kazi yao ya kila mwaka ambapo jukumu moja wajawapo ni kutangaza na kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini. Pamoja na hatua hizo, Wizara imeandaa Mfumo wa kuwawekea malengo balozi zetu nje ya nchi ambapo suala la

kutangaza utalii litauwa mojawapo wa vigezo vya kupimwa katika utendaji kazi (*Key Perfomance Indicators – KPI)*.

***12. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara kwa kushirikiana ***na*** Wizara ya Maliasili na Utalii, itaanzisha utaratibu wa kuwa na waambata wa Utalii katika Balozi ambazo zina mchango mkubwa katika kuleta watalii nchini. Vilevile katika jitihada za kuongeza watalii wanaokuja nchini, Wizara imeongoza na kuratibu vikao kazi vya wataalamu vya kuandaa mkakati wa utekelezaji wa zao la kitalii la Utalii wa Halal (*Halal Tourism*). Inategemewa kuwa utekelezaji wa mkakati huo utaongeza watalii kwa asilimia 20. Majukumu hayo yanatekelezwa sambamba na majukumu mengine ya ubalozi kama vile kuvutia wawekezaji, kubidhaisha Kiswahili, kutafuta masoko ya bidhaa na huduma na fursa za masomo na ajira. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia maonesho ya biashara, makongamano ya biashara, machapisho, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

***(vi) Miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ni kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi. Diplomasia ya uchumi bado haijaeleweka kwa ufasaha kwa wananchi na hata viongozi ambao wanasimamia sekta mtambuka ambazo zinahusika na uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa. Hili linasababisha nchi kutonufaika ipasavyo na diplomasia ya uchumi.***

***13. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** diplomasia ya uchumi ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ambayo inajumuisha jitihada zinazolenga kulinufaisha Taifa kiuchumi na kijamii kupitia uhusiano na ushirikiano na mataifa mengine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Jitihada hizo zinajumuisha utafutaji wa masoko ya bidhaa na huduma nje ya nchi; kuwezesha uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji muhimu ya ndani; kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje; na kuhamasisha uwekezaji wa moja kwa moja kwenda nje ya nchi. Hatua muhimu iliyofikiwa na Wizara katika kipindi hiki ni kukamilika kwa utayarishaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ambao utaratibu utekelezaji na utoaji wa elimu ya umma kuhusu diplomasia ya uchumi nchini.

***14. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuelimisha umma kuhusiana na diplomasia ya uchumi na ushirikiano wa kikanda. Hatua hizo ni pamoja na kuandaa vipindi vya redio na runinga. Aidha, Wizara inatumia warsha na makongamano kuwasilisha mada zinazohusiana na dhana ya diplomasia ya Uchumi, kwa mfano:

a) Wizara iliwasilisha mada katika mkutano wa ngazi ya juu ya majadiliano baina ya serikali, sekta binafsi na washirika wa maendeleo uliofanyika mwezi Februari 2024 jijini Dar es Salaam; na

b) Wizara iliwasilisha mada ya jukumu la diplomasia ya uchumi katika kuwawezesha wajasiriamali na wanawake katika kuchangamkia fursa zilizopo kwenye soko Huru la Bara la Afrika (AfCFTA).

c) Wizara imekuwa ikishiriki kwenye vipindi mbalimbali vya radio na televisheni kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma juu ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi

d) Wizara imekuwa na vikao mbalimbali na wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi kuhusu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

***15. Mheshimiwa Mwenyekiti*** Wizara pia kwa kushirikiana na wadau imetoa elimu mahususi kwa wazalishaji na wafanyabiashara kuhusu fursa za soko la Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA). Miongoni mwa wanufaika wa elimu hiyo ni pamoja na wazalishaji na wafanyabiashara wa tumbaku na bidhaa za tumbaku; kahawa; viungo na katani. Kutokana na kupata elimu hiyo, Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika biashara ndani ya AfCFTA kupitia mpango wa majaribio unaojulikana kama *Guided Trade Initiative* kwa kuuza zaidi Kahawa, Katani, viungo na tumbaku katika kipindi cha mwaka 2023.

***16. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara itaendelea kuelimisha umma ikiwa ni pamoja na kutoa semina elekezi kuhusu dhana ya diplomasia ya uchumi katika ngazi ya wilaya na mikoa na kwa wafanyabishara ili watanzania kwa ujumla waweze kutumia

ipasavyo fursa zinazopatikana kutokana na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

***(vii) Kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kupeleka watumishi balozini kulingana na fani maalum zinazohusika na masuala ya uchumi, uwekezaji na utalii. kufanya hivyo itakuwa ni sehemu ya nchi yetu kunufaika na diplomasia ya uchumi.***

***17. Mheshimiwa Mwenyekiti***, Wizara inaendelea kupeleka watumishi balozini kwa kuzingatia mahitaji ya Ikama katika Kituo husika ikiwemo wataalam katika sekta za uchumi, biashara, uwekezaji, kilimo, mazingira na utalii kama hatua muhimu ya kuwezesha Taifa kunufaika na Diplomasia ya Uchumi. Aidha, Wizara imeendelea na juhudi za kuwapatia watumishi mafunzo mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu zaidi ya moja vituoni (*multitasking)* kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama. Hali kadhalika, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais - Utumishi ili kupata vibali vya ajira mpya na vibali vya kuhamishia watumishi wengine ili kuongeza nguvukazi Makao Makuu na Balozini. Vilevile, kupitia kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Zanzibar mwezi Januari, 2024 baraza liliridhia Wizara kushirikiana na Sekta ili kupata wataalamu hao.

***(viii) Wananchi wana haki ya kunufaika na fursa za kiuchumi na masoko zinazopatikana katika jumuiya za kikanda. Tathmini na ufuatiliaji unaonesha kuwa watanzania hawajanufaika ipasavyo na fursa za kiuchumi na masoko katika jumuiya za kikanda.***

***18. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** moja ya lengo la nchi kujiunga na jumuiya za kikanda ni kufungua fursa za kiuchumi na kibiashara kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan fursa za soko la bidhaa na huduma. Katika kufikia lengo hilo Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Wizara nyingine za kisekta zikiwemo Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Wizara ya Uchukuzi zimeendelea kuwahamasisha wananchi kuchangamkia fursa zilizopo katika jumuiya za kikanda. Vilevile, Serikali imeendelea kuchukua hatua zenye lengo la

kuwezesha watanzania pamoja na kuwajengea uwezo ili kunufaika na fursa zitokanazo na jumuiya za kikanda.

***19. Mheshimiwa Mwenyekiti***, kutokana na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali kuwahamisha wananchi, hasa wafanyabiashara kunufaika na masoko ya kikanda ya Afrika Mashariki (EAC) na kusini mwa Afrika (SADC), wananchi wengi wameendelea kunufaika na fursa zilizopo katika masoko hayo ya kikanda. Kwa sasa Tanzania ni muuzaji mkubwa wa bidhaa za kilimo kama vile nafaka na mboga mboga kwenye soko la Afrika Mashariki na pia bidhaa za viwandani. Kwa sababu hiyo, urari wa biashara baina ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki umekuwa mzuri kwa upande wa Tanzania.

Takwimu zinaonyesha urari wa biashara baina ya Tanzania na nchi za Africa Mashariki ni mzuri kwa zaidi ya dola za Marekani milioni 500.

***20. Mheshimiwa Mwenyekiti***, vilevile, katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Tanzania imekuwa ikinufaika na soko hilo hasa katika sekta ya bidhaa za viwandani, sekta ya madini na sekta ya usafirishaji ambapo wafanyabiashara wengi wa Tanzania ndio wenye kumiliki malori yanayosafirisha bidhaa baina ya Tanzania na Zambia, Malawi na nchi nyingine za SADC. Takwimu zinaonyesha urari wa kibiashara baina ya Tanzania na nchi za SADC ni mzuri kwa zaidi ya dola za Marekani bilioni moja.

***21. Mheshimiwa Mwenyekiti***, pamoja na mafanikio hayo, Wizara imeendelea ***kuchukua*** hatua ili kuongeza manufaa zaidi kwa wananchi katika Jumuiya hizo za kikanda. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu mahususi kwa wazalishaji na wafanyabiashara kuhusu fursa za soko la Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Aidha, Nchi yetu imekuwa miongoni mwa nchi ambazo zimefanya vizuri katika kutumia soko la AfCFTA kupitia mpango wa majaribio unaoitwa *Guided Trade initiative* ambapo mwaka 2023 kampuni 11 zimeuza katika soko la AfCFTA.

***(ix) Mpango wa ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsi katika ujenzi wa majengo ya ubalozi na vitega uchumi unakabiliwa na changamoto mbalimbali; zikiwemo za kisheria. Hivyo, ili mpango huo uweze kutekelezeka kuna umuhimu wa kuchukua hatua kumaliza changamoto hizo***

***22. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara ipo kwenye utekelezaji wa mkakati wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Balozini ambapo mkakati huu umelenga kutumia vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwemo ubia na sekta binafsi. Mkakati huo umeainisha maeneo saba (7) ya sheria, kanuni na taratibu za ndani zinazopunguza ufanisi katika utekelezaji na ugharamiaji wa miradi ya uendelezaji wa viwanja na ukarabati wa majengo ya serikali nje ya nchi, pamoja na vyanzo vingine ikiwemo ushirikiano na sekta binafsi. Wizara imewasilisha maeneo saba (7) ya kisheria yenye changamoto katika Mamlaka husika ikiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Wizara ya Fedha ili yaweze kufanyiwa kazi. Maeneo hayo ni pamoja na a) Sheria ya Ununuzi wa Umma; b) Sheria ya Fedha za Umma (Kifungu 6(a)(1), CAP 348); c) Sheria ya Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP); d) Muongozo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (aya ya 8, mwaka 2021); e) Kanuni za Kifedha za Kigeni (Kanuni ya 37, GN 294 ya mwaka 2022); f) Kanuni za Taasisi za Fedha na Benki (Kanuni ya 10, GN 290 ya mwaka 2014); na g) Kanuni ya Ukomo wa mikopo na Hasara nyingine tarajiwa (Kanuni ya 6, 18 GN 288 ya mwaka 2014).

***(x) Ili kuhakikisha kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 miradi yote ya maendeleo inatekelezwa kwa wakati; Wizara iweke mkakati maalum wa kuanza maandalizi mapema ya kukamilisha taratibu zote muhimu za awali zinazohitajika ili kuanza utekelezaji wa miradi na kuomba fedha Hazina kwa wakati.***

***23. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara imejipanga kuwezesha miradi kupata fedha kwa wakati kwa kuhakikisha inazingatia na kukamilisha vigezo vinavyohitajika ikiwa ni pamoja na kuandaa nyaraka muhimu kama vile michoro, makadirio halisi ya gharama, maandiko ya miradi husika pamoja na kukamilisha taratibu za zabuni.

***24. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** baadhi ya miradi ambayo Wizara imeandaa na imekidhi vigezo vya kupokea fedha kutoka Wizara ya Fedha ni pamoja na mradi wa ujenzi wa majengo ya makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu - Lakilaki Arusha; mradi wa ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim – Kurasini; mradi wa ukarabati wa nyumba nne (4) za ubalozi wa Tanzania Pretoria; mradi wa ujenzi wa uzio katika viwanja vya ubalozi wa Tanzania Addis Ababa.

***25. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara imekamilisha nyaraka muhimu za utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa majengo katika balozi za Nairobi na Kinshasa kwa kutumia vyanzo mbadala vya fedha. Kufanikisha hatua hii, kumeiwezesha Wizara kuingia makubaliano ya kujenga Jengo la Kitega Uchumi katika ubalozi wa Tanzania uliopo Nairobi kwa ubia na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

***(xi) Ili kupata tija iliyokusudiwa katika miradi ya maendeleo Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kuzingatia mpango wa Wizara wa utekelezaji wa miradi husika.***

***26. Mheshimiwa Mwenyekiti***, Serikali imeendelea kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mahitaji. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Wizara imepokea kiasi cha shilingi 16,762,726,958.61 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 93.7% ya shilingi 17,887,608,000 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi 11,777,968,375.04 ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; shilingi 204,638,466.57 ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim (CFR) na shilingi 4,780,120,117 ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo na ununuzi wa samani katika balozi za Tanzania nje ya nchi.

***27. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kwa kuzingatia umuhimu wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo, Wizara ya Fedha imeongeza wigo wa bajeti kwa kiasi cha shilingi 8,776,519,684.56 na hivyo

kuifanya kuwa na wigo wa shilingi 26,664,127,684.56. Naomba nitumie fursa hii kukushukuru wewe na Kamati yako kwa juhudi zenu za kutuwezesha kupata fedha hizi.

***(xii) Kutokana na umuhimu wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hiyo. Kufanya hivyo kutawezesha kuanza kutekelezwa kwa mradi huo na kuendelea kujenga taswira nzuri ya kidiplomasia iliyonayo nchi yetu katika Umoja wa Afrika na duniani kwa ujumla.***

***28. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu umeendelea kuwa kipaumbele cha Serikali ikiwa ni utekelezaji wa makubaliano kati Tanzania na Umoja wa Afrika. Ninayo heshima kuitaarifu Kamati yako kuwa Serikali kupitia Wizara ilishampata mkandarasi kampuni ya *CRJE (East Africa)* Limited kutoka nchini China ambaye anatekeleza mradi huu kwa gharama ya shilingi 62,968,086,187.78 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Aidha, usimamizi wa mradi unafanywa na mshauri elekezi kampuni ya *Aru Built Environment Consulting Company (ABECC)* ya Chuo Kikuu Ardhi kwa gharama za shilingi 2,956,000,000 pamoja na VAT.

***29. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** ujenzi ulianza rasmi tarehe 28 Agosti, 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 27 Februari, 2025. Hadi kufikia mwezi Machi 2024 kiasi cha shilingi 11,777,968,375.04 kilitolewa na kulipwa mkandarasi kampuni ya *CRJE (East Africa) Limited* ikiwa ni malipo kazi za ujenzi wa mradi huo ambao umefikia asilimia 12.2 ya kazi zote za mkataba.

***(xiii) Serikali iendelee kutekeleza mkakati maalum wa kukarabati nyumba za watumishi katika balozi zetu kwa awamu ili nyumba hizo ziendane na hadhi ya Tanzania iliyonayo nje ya nchi.***

***30. Mheshimiwa Mwenyekiti***, Ushauri huu umezingatiwa pia katika hoja namba iv ambapo Wizara inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa ukarabati na ujenzi wa majengo balozini ambao

umeainisha miradi 15 ya kipaumbele itakayotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi 2026/2027). Mkakati huo umepanga kutumia vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwemo bajeti ya Serikali, mikopo ya masharti nafuu kutoka taasisi za fedha na kwa kuingia ubia na mifuko ya taifa ya hifadhi ya jamii, mashirika ya umma na sekta binafsi. Baadhi ya miradi hiyo 15 ya kipaumbele ni pamoja na ujenzi wa majengo katika ubalozi wa Nairobi – Kenya (NSSF) na Ujenzi wa majengo katika ubalozi wa Kinshasa – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (NSSF).

***31. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** katika utekelezaji wa mpango huo, Serikali imetenga fedha kutoka mfuko mkuu na kuzielekeza katika ukarabati wa nyumba nne (4) za Ubalozi wa Tanzania Pretoria, mradi wa ujenzi wa uzio katika viwanja vya ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, ukarabati wa Makazi ya Balozi London, ukarabati wa Makazi ya Balozi Geneva, ukarabati wa majengo katika Balozi za Beijing, Ottawa, Brussels, na Stockholm. Kufikia mwezi Februari 2024, jumla ya Shilingi 4,780,120,117 zimekwishatolewa na Serikali na zimetumwa kwenye vituo hivyo kwa kazi za ukarabati.

***32. Mheshimiwa Mwenyekiti***, Aidha, mnamo mwezi Januari 2024 Wizara ilifanya wasilisho katika Baraza la Mawaziri kuhusu uhitaji wa kufanya ukarabati katika Balozi zetu nje ya nchi na Baraza liliridhia hoja hiyo na kuagiza kuanza utekelezaji wake.

***(xiv) Kamati inapongeza Serikali kwa utekelezaji wa maombi ya watanzania (diaspora) ambao wamekuwa wakiomba kutambuliwa na Serikali; mchakato huu unaendelea vizuri ikiwa ni pamoja na kuzinduliwa rasmi kwa mfumo wa kukusanya na kutunza taarifa za diaspora kidigitali (diaspora digital hub) uliozinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Stergomena L. Tax (Mb), aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mwezi Mei, 2023. Kamati inashauri mchakato huu ukamilishwe mapema iwezekanavyo ili kuleta tija inayokusudiwa.***

***33. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Serikali imeendelea na juhudi za kuwatambua na kuwashirikisha Diaspora katika maendeleo ya Taifa ambapo kwa sasa iko katika hatua za kukamilisha taratibu za kutoa hadhi maalumu (*special status*) kwa raia wa nchi

nyingine wenye asili ya Tanzania (*Tanzania non-citizen diaspora*) kwa kuzingatia maombi yaliyowasilishwa. Serikali tayari imeridhia utoaji huo wa hadhi maalumu kwa diaspora. Aidha, katika kutekeleza azma hii, Serikali inaendelea na taratibu husika za kisheria ili kuwasilisha katika Bunge la 12, Mkutano wa 15 mabadiliko madogo *(miscellaneous amendments)* ya Sheria mbili ambazo ni Sheria ya Uhamiaji, Sura 54 na Sheria ya Ardhi, Sura 113 ili kuwezesha utekelezaji wa hadhi maalumu.

***34. Mheshimiwa Mwenyekiti***, vilevile, tangu kuzinduliwa kwa mfumo wa kukusanya na kutunza taarifa za diaspora kidigitali (*Diaspora Digital Hub - DDH*) hadi kufikia mwezi Machi, 2024 diaspora zaidi ya 1,400 wamejisajili. Idadi hii haijumuishi takwimu za waliojisajili nje ya mfumo huo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea na maboresho ya mfumo huo kwa lengo la kutatua changamoto zilizobainika na kuufanya kuvutia diaspora kujisajili kwa wingi zaidi. Hatua nyingine ni kuufanya mfumo usomane na mifumo mingine ya watoa huduma za diaspora kwa lengo la kuongeza ufanisi.

***(xv) Serikali izidishe juhudi katika kuzisimamia balozi zetu nje ya nchi kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali vilivyopo nchini. Hii iende sambamba na kuhakikisha kunakuwa na mkakati unaotekelezeka utakaoainisha malengo na namna ya kutekeleza malengo hayo katika sekta ya utalii kwenye balozi zetu.***

***35. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara kupitia balozi za Tanzania kwa kushirikiana na wadau wengine zikiwemo wizara za kisekta hususan Wizara ya Maliasili na Utalii, taasisi za umma na sekta binafsi zimeendelea kutangaza fursa za utalii kupitia sera ya mambo ya nje na mpango mkakati wa Wizara. Aidha, balozi zetu zinatekeleza mipango kazi yao ya kila mwaka ambapo jukumu mojawapo ni kutangaza na kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini.

***36. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** pia, Wizara inaendelea kupeleka watumishi balozini kwa kuzingatia mahitaji ya ikama katika kituo husika ili kutekeleza diplomasia ya uchumi ikiwemo kutangaza fursa za utalii. Aidha, Wizara imeendelea na juhudi za kuwapatia watumishi mafunzo mbalimbali ili waweze kutekeleza

majukumu zaidi ya moja vituoni (*multitasking)* kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama.

***37. Mheshimiwa Mwenyekiti***, vilevile, Wizara imekamilisha uandaaji wa rasimu ya mkakati mahususi wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi (*National Economic Diplomacy Implementation Strategy - NEDIS*) kwa mwaka 2024 – 2027. Kukamilika kwa mkakati huo kutaiwezesha Wizara na wadau wote kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuzingatia vipaumbele ili kukuza maslahi ya nchi kiuchumi kwa kiwango cha kimataifa. Hatua hii itahusisha kuweka malengo na juhudi za kukuza utalii nchini kupitia balozi zetu. Pamoja na hatua hizo, Wizara imeandaa Mfumo wa kuwawekea malengo balozi zetu nje ya nchi ambapo suala la kutangaza utalii litauwa mojawapo wa vigezo vya kupimwa katika utendaji kazi (*Key Perfomance Indicators – KPI)*.

***(xvi) Katika kuhakikisha kuwa nchi inanufaika ipasavyo na diplomasia ya uchumi Wizara ikamilishe mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kukamilisha mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi pamoja na faida nyingine pia utasaidia diplomasia ya uchumi kutekelezwa katika ngazi ya mkoa na wilaya.***

***38. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara imekamilisha uandaaji wa rasimu ya mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi (*National Economic Diplomacy Implementation Strategy - NEDIS*) kwa mwaka 2024 – 2027. Mkakati huo umeianisha maeneo ya kipaumbele kwenye eneo la diplomasia ya uchumi na pia kuainisha mfumo wa uratibu baina ya Wizara na wadau wengine katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ni pamoja na kuvutima wawekezaji, kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi, kukuza utalii, kukuza mauzo ya huduma mbalimbali nje ya nchi, kukuza ushirikiano wa maendeleo ili kuongeza misaada na mikopo kwa nchi yetu, kubaini na kuongeza fursa na masomo na ajira kwa watanzania nje ya nchi, na pia kuimarisha uratibu na uwezo wa kitaasisi katika kutekeleza diplomasia ya uchumi. Kukamilika kwa mkakati huo kutaiwezesha serikali na wadau wote nchini na nje ya nchi kutekeleza diplomasia ya uchumi ya

Tanzania kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa ili kukuza maslahi ya nchi kiuchumi na kibiashara kwa viwango vya kimataifa.

***39. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** hatua hii itahusisha juhudi mbalimbali zikiwemo za kuongeza mauzo ya nje ya Tanzania, kuvutia viwango vya juu vya uwekezaji wa moja kwa moja wa nje, kukuza utalii, kubidhaisha lugha ya Kiswahili, kukuza ushirikiano wa kiuchumi hasa katika sayansi na teknolojia, na kuwezesha fursa za ajira na elimu kimataifa kwa watanzania.

***(xvii) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara ziandae mkakati wa kupeleka watumishi wenye fani maalum kwa kuzingatia mahitaji; ikiwemo fani za uchumi, uwekezaji, utalii na biashara. Kufanya hivyo kutachochea kasi ya kutafuta wawekezaji na watalii katika balozi zetu.***

***40. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** ushauri wa Kamati umepokelewa na tayari Wizara imeendelea kuufanyia kazi kwa kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara za Kisekta. Katika kipindi hiki, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepokea watumishi wabobezi 32 kutoka wizara na taasisi mbalimbali, pamoja na kuajiri watumishi wapya 12. Hatua hizi zote zinalenga kuhakikisha kuwa Wizara inaongeza watumishi wenye ujuzi katika fani mbalimbali, wanaoweza kutekeleza diplomasia ya uchumi kikamilifu wakiwa wizarani na katika balozi zetu.

***(xviii)Ikiwa ni sehemu ya kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Serikali iongeze kasi katika kukamilisha sera ya mambo ya nje ambayo imekuwa ikishauriwa na wabunge katika vipindi tofauti.***

***41. Mheshimniwa Mwenyekiti***, Wizara ilikamilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 ambayo yalijadiliwa na Baraza la Mawaziri mwezi Agosti, 2023. Baraza la Mawaziri lilielekeza Wizara kukusanya maoni zaidi kutoka kwa wadau mahsusi kupitia makongamano.

***42. Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara imefanya makongamano ya kukusanya maoni ya ziada kutoka kwa wadau mahsusi katika miji ya Arusha mwezi Novemba, 2023; Dar es Salaam mwezi Januari, 2024; Unguja na Pemba mwezi Februari, 2024. Makongamano mengine yamepangwa kufanyika katika miji ya Mwanza, Mbeya, Mtwara na Dodoma mwezi Machi na Aprili 2024. Wadau wa makongamano hayo wanajumuisha viongozi na wawakilishi wa vyama vya siasa; viongozi wa dini; asasi za kiraia; wanataaluma, watafiti na sekta binafsi. Wizara imepanga kukamilisha ukusanyaji wa maoni na kuwasilisha maboresho ya Sera kwa ajili ya maamuzi ndani ya Serikali mwisho wa mwezi Aprili, 2024.

***(xix) Serikali iendelee kuhamasisha kimkakati sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki pamoja na jumuiya nyingine za kikanda.***

***43. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** ili kuhakikisha sekta binafsi ya Tanzania inanufaika kiuchumi kutokana na mtangamano wa Afrika Mashariki, Wizara kwa kushirikiana na wizara na taasisi nyingine za Serikali imeendelea na jitihada zifuatazo:

i) Kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za mtangamano wa jumuiya za kikanda na taratibu za kufikia masoko ya kikanda kupitia majukwaa mbalimbali ya kitaifa na kikanda;

ii) Kushirikisha sekta binafsi katika mikutano ya ndani ya maandalizi na mikutano, semina na warsha za kikanda kupitia mashirika miamvuli, katika maandalizi ya programu za kikanda ili kujenga uelewa wa fursa zitokanazo na programu hizo za kikanda;

iii) Kufanya ziara katika mipaka ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kubaini changamoto na kuwaelimisha watumishi wa umma na wadau wa sekta binafsi kuhusu makubaliano ya kurahisisha biashara miongoni mwa nchi wanachama; na

iv) Kufanya makogamano ya kibiashara kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na nchi jirani zilizopo katika jumuiya za kikanda ili kuimarisha ushirikiano wa kibiashara kati ya sekta binafsi ya Tanzania na nchi jirani.

***(xx) Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023.***

***44. Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepokea ushauri uliotolewa na Kamati na imeendelea kuufanyia kazi.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya mchango huo ambao umetolewa hapa na Mheshimiwa Tadayo kwa niaba ya Kamati, sasa ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii.

Yupo Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwanzo kwenye hotuba hii ya Wizara, lakini naomba nianze kwa mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake kubwa katika kuhakikisha kwamba anaifungua nchi yetu ili iweze kurudi katika hadhi yake kubwa na mahusiano mazuri. Vilevile kufungua nafasi ya uchumi kwenye nyanja za utalii, uwekezaji na mambo mbalimbali. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niishukuru Wizara nikianza na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ambaye kwa kweli

anajitahidi kufanya kazi zake kwa kuimarisha mahusiano kwa sababu mahusiano kila siku nasema ni jambo la gharama, lakini wanaendelea kuifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba tunarudi na tunairudisha nchi yetu kwenye nafasi yake halisi kama kiungo na kuleta chachu kwenye maendeleo ya uchumi wetu. Naomba niwapongeze, waendelee na kazi hiyo kwa sababu suala la kutunza marafiki ni suala gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo naomba nichangie mambo mawili au matatu; jambo la kwanza; pamoja na kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Wizara yetu hii bado sisi kama Bunge naomba tuisaidie Wizara hii ili iweze kufikia malengo hasa kwenye miradi yake ya maendeleo kwa sababu kwa kweli fedha wanazoomba hazifikii kiwango ambacho kingeweza kusaidia kuleta maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tuliwahi kusema miaka miwili au mitatu huko nyuma kwamba yapo maeneo yetu muhimu ambayo kwa kweli yangeweza kuisaidia Serikali kuweza kupata kipato, lakini bahati mbaya sana maeneo haya bado hayajapelekewa fedha na kwa kweli kama Taifa tunashindwa kupata fedha na badala yake tunapeleka fedha nje, ili ziweze kufanya mambo mengine badala ya fedha hizi kupatikana kutoka kwenye vyanzo vyetu vya mapato vilivyopo nje. Kwa mfano, tunayo maeneo mawili mazuri sana huko Addis, lakini tumeshindwa kuyafanyia kazi ili yaweze kuongeza kipato kwenye Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunalo tatizo Marekani kule tumekwenda kuona bado maeneo yetu hayajafanyiwa maboresho ili yaweze kulisaidia Taifa kupata kipato. Tunayo maeneo DRC, Mheshimiwa Waziri amesema hapa mipango ya kujenga, lakini mipango siyo matumizi. Ningeomba sana Serikali hasa Wizara ya Fedha ione umuhimu wa kujipunguzia mzigo huu wa kuendelea kubeba taasisi zetu hizi hasa za mabalozi wakati tungeweza kuwapa fedha, tukajenga maeneo yale, tukaisaidia Serikali kuipunguzia mzigo wa kepeleka fedha kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa maana hiyo hiyo tulizungumza pale nyuma juu ya uwezo wa kuwawezesha Wizara kuwa na

wataalamu wazuri kwenye maeneo mbalimbali. Bado Wizara yetu haijapatiwa watendaji wa kutosha ili kuweza kutekeleza mipango yao ya maendeleo na kidiplomasia. Naomba sana, tumezungumza kwenye taarifa yetu huku kwamba wenzetu wa utumishi wafanye kazi ya makusudi ili kuweza kuirudisha Wizara na Taifa hili kwenye nafasi yake ya kuwawekea wataalamu wanaoweza kufanya kazi kwenye mataifa mbalimbali. Itasaidia sana ili kuhakikisha kwamba lile ambalo wanalipanga ndilo ambalo linatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa maana hiyo hiyo kwenye suala la mahusiano naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwani alitushirikisha kama Kamati jinsi ya kuona namna gani tunarudisha mahusiano yetu na mataifa mbalimbali kwa sababu yaliyumba kidogo. Sasa ningemuomba Mheshimiwa Waziri aendelee na kazi hii ni ngumu, inakufanya usikae nyumbani na sisi wenzako tukuone kama vile Bungeni unatoroka kumbe ndiyo kazi zako. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba kazi zako ni za nje, lakini Bunge ni *part and parcel* ya kwako, jitahidi basi angalau tuwe tunakuona hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa maana hiyo nimwombe Waziri na Wizara kwa ujumla kwamba tunayo au tunazo balozi ambazo zinahudumia mataifa mengine. Kwa mfano, Brazil inahudumia mataifa mengi sana na India inahudumia mataifa mengi sana. Kwa hiyo, tuwawezeshe kuwapa *instruments* ambazo wataweza kusimamia yale mataifa. Kwa mfano, India inaongoza nadhani nchi tano za ziada, lakini bahati mbaya sana wanashindwa kwenda kufanya kazi zao kama balozi kwa sababu hatuwapatii *instruments* ili waweze kutambulika kwenye mataifa yale. Huu ni wajibu wetu, kama umempa mtu nafasi afanye kazi mahali, lazima aweze kutambulika na Taifa husika kwamba na yeye ni balozi kwenye eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na yote hayo ningeomba sana Wizara hii ina umuhimu mkubwa sana. Nyuma tuliwahi kusema kwamba Wizara hii ndiyo kioo chetu, tunapimwa kwa mazuri na mabaya na wenzetu kutokana na Wizara hii. Ningeomba sana pamoja na uchache wa fedha tulionao, tumeona hapa kwenye maendeleo, fedha iliyopatikana bado ya

mwaka huu ni pungufu ukilinganisha na mwaka uliopita. Ningeomba sana tuone namna gani tunaweza tukajibana, lakini Wizara hii tuiwezeshe ili iweze kufanya kazi zake na kuirudisha Wizara na Taifa hili kwenye vigezo vyake vya kuwa Taifa unganishi, ili iweze kufikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Valentine Magige atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mheshimiwa Ali Juma Mohamed ajiandae.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Mambo ya Nje. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kwa kweli matunda ya kazi yao tunayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi pia ziende sambamba na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya. Tumekuwa tukishuhudia mama hapumziki, amekuwa akisafiri mataifa mbalimbali kuhakikisha anaenda kutatua kero za Watanzania. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kumshukuru, kuendelea kumuombea na kumtia moyo azidi kusafiri kutafutia Watanzania fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa baadhi ya mafanikio ya ziara ya Rais wetu nikuongezeka kwa *FDI (Foreign Direct Investment)* kutoka dola bilioni mbili mwaka 2020 hadi dola bilioni tano Juni, 2023. Lengo ni kufikia dola bilioni 15 ifikapo mwaka 2025 na kwa jitihada hizi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunajua malengo haya yatatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais amepelekea nchi kuingia hati za makubaliano na nchi nyingi ikiwemo nchi kubwa kiuchumi kama Marekani na India. Safari ya India tu wamesaini hati 14 za makubaliano katika sekta ya afya, maji na teknolojia ya habari. Pia nchi ilipata fursa ya kuuza mbaazi zake katika soko la India.

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kufanya vizuri kimataifa na kutuheshimisha nchi yetu katika mataifa mbalimbali na mwezi wa nne atachukua Uenyekiti wa *SADC Organ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimataifa amekuwa sauti ya wanawake wa Afrika katika ajenda ya kuwawezesha wanawake wa Kiafrika kupata nishati salama ya kupikia. Amefanikisha nchi kupata mikopo kwa riba nafuu na imepelekea kwenda kumalizia reli ya *SGR*, ujenzi wa miundombinu ya madarasa na vituo vya afya. Amepata fursa ya kushiriki majukwaa mapya kama *BRICS*. Hapa tunaona ni jinsi gani Rais wetu anavyotambulika na anavyoiheshimisha nchi yetu ya Tanzania kwenye mataifa mbalimbali. Ametusaidia tumepata masoko ya biashara zetu kwenye masoko mapya kama vile kuuza mabondo ya samaki na maparachichi kwenye soko la India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nitaomba tuendelee kuangalia ziara hii…

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ningependa kumwongezea pia aendelee kumpongeza na sisi tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanya umataifashaji katika utamaduni wa Tanzania na jana ameahidi kwamba ataanza kwenda na wasanii wetu nje ya nchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, naipokea Taarifa hii na tuna imani na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na tunaona matokeo makubwa ya ziara zake anazofanya. Kwa hiyo, kwa wale wanaopinga ziara za Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan na hapa nikiendelea kutaja mafanikio yake sitamaliza na muda wangu ni mchache wa dakika 10 tu. Tumpongeze Mama Samia, *big up* Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze mchango wangu katika Kituo chetu cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha *(AICC)*. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa *AICC* ambaye ameteuliwa siku za karibuni Ndugu Christine Mwakatobe kwa uteuzi huu. Nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwaona wanawake. Kwa kipindi kifupi tu tunamuona mama huyu ameshaanza kufanya vizuri katika kazi yake, lakini kitakachomwangusha ni madeni. *AICC* inazidai taasisi mbalimbali *more than five billion*. Inadai taasisi kubwa hata kuzisoma hapa mtashangaa na ninazo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba muwalipe *AICC* fedha zao ili waendelee kujiendesha na kufanya kazi vizuri na Mkurugenzi huyu mpya mumtie moyo aendelee kujiamini afanye *wonders*. Tunaomba taasisi za Serikali ikiwemo na Wizara ya Mambo ya Nje muwalipe *AICC* fedha zao. Wizara mbalimbali mnadaiwa huku, mlipe *AICC* fedha zao na sisi tutaendelea kufuatilia kwa ukaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile niipongeze Serikali kwa mradi mkubwa wa ukumbi mpya wa *AICC* ambao utahudumia watu zaidi ya 6,000 kwa wakati mmoja. Mradi huu mkubwa wa mkutano utachochea ukuaji wa uchumi, kutuingizia fedha za kigeni, ukuaji wa huduma za malazi na kuitangaza Tanzania. Pia utakapokamilika utaongeza ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa hivi nijielekeze katika suala zima la *diaspora*. Ninaipongeza Wizara kwa hatua nzuri iliyofikia ya kutoa hadhi maalumu kwa raia wa nchi za nje wenye asili ya Kitanzania *(Tanzania Noncitizen Diaspora)*. Suala hili limekuwa la muda mrefu sana, lakini sasa hivi naona linaenda kufikia tamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba iongezwe kasi zaidi kwa kuwasilisha muswada wa mabadiliko ya sheria mbili za

Uhamiaji Sura Na. 54 ili kuwawezesha kuingia na kukaa nchini bila ukomo na Sheria ya Ardhi Sura Na. 113 ili kuwawezesha kumiliki ardhi kwa utaratibu utakaotolewa, ili *diaspora* hawa wapate haki na upendeleo waliopoteza kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya kuhamasisha *diaspora* kuchangia maendeleo ya Taifa lao la Tanzania. Tumesikia baadhi ya maeneo yamenufaika kwa kutuma pesa kwa ajili ya kununua nyumba, uwekezaji katika Mfuko wa *UTT*, kuchangia visima vya maji kama huko Pemba, kulima zao la *cacao* ambapo wanatengeneza *chocolate* kule Kyela, Mbeya.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaomba Balozi za Tanzania zishirikiane na wadau wengine ili kuongeza kasi katika kutoa huduma hasa za *passport* na Vitambulisho vya Taifa. Pia ninashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii. *TTB* iwatumie *diaspora* hawa kutangaza utalii katika nchi mbalimbali. Nina imani kabisa kwamba *diaspora* wana wivu na nchi yao na wanapenda maendeleo ya nchi yao. Ninaomba kero zao ziangaliwe na zitatuliwe. Mimi nina imani kubwa na uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hata *diaspora* watafaidika kwa kuwa kero zao zote zitatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kama walivyosema wenzangu ninapenda kuanza kwa kupongeza na kumpongeza Mheshimiwa Rais kama mwanadiplomasia namba moja na pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri January Makamba na wasaidizi wake wote, kwa maana ya Mheshimiwa Balozi Mbarouk na wakili msomi Mheshimiwa Byabato pamoja na Katibu Mkuu Balozi Samwel Shelukindo, wasaidizi wake wote, watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na mabalozi wanaotuwakilisha katika nchi zetu maeneo

mbalimbali, yakiwepo maeneo ambayo ni Ofisi za Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi chache, ninapenda pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maamuzi yake ya kuamua kukiita Chuo cha Diplomasia au Kituo cha Diplomasia cha Kurasini *CFR* ambacho mimi ni sehemu ya zao lake, kwa jina la Dkt. Salim Ahmed Salim katika kumuenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dkt. Salim Ahmed Salim amewahi kuwa Katibu Mkuu wa *OAU* kabla haijawa *AU*. Kwa hiyo, kwa kweli ni maamuzi sahihi ya kuwaenzi viongozi ambao wametumika ndani ya nchi, lakini pia wametumika Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake ametueleza jinsi ambavyo Wizara inafanya kazi na jinsi ambavyo imefanya kazi mojawapo ya kuratibu ziara za viongozi wakuu wa nchi kwenda nje kama ziara 31 na viongozi wa nje kuja nchini kama ziara 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, Tanzania ni mwanachama mwaminifu na wa kuaminika kikanda na kimataifa. Pengine hapa niseme kidogo, wakati mwingine pengine kutokana na mapokeo au pengine kukosa uelewa, wakati mwingine baadhi ya watu hudhani kwamba ziara hizi ni ziara za kwenda tu kutembea, hapana. Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake ametueleza manufaa yanayotokana na ziara za viongozi, ametueleza kuongezeka kwa uwekezaji, fursa za masoko, fursa za masomo na fursa za ajira. Tunafahamu nchi yetu takribani 10% inategemea mikopo ya riba nafuu na misaada katika kuendesha bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yote haya hayaji tu, ni matunda yatokanayo na ziara za viongozi wetu na hasa ikiongozwa na mwanadiplomasia namba moja Mama Samia Suluhu Hassan katika kufanya ziara na kushiriki mikutano na makongamano mbalimbali. Hata hivyo, ninatoa ushauri kwa Wizara. Viongozi wanapofanya ziara kuna matunda mengi, Mheshimiwa Waziri ametoa takwimu hapa, hasa katika uwekezaji

na mabilioni ambayo tumepata kama mitaji ya moja kwa moja kuja kuwekeza hapa nchini. Tupanue wigo kwa kuijulisha jamii yale yatokanayo na ziara za viongozi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ninakumbuka Mheshimiwa Rais na viongozi kadhaa walikwenda kwenye *Expo Dubai.* Je, baada ya ziara ile mpaka sasa ni mambo gani ambayo yanatokana na ziara ile? Hii itasaidia kuwafanya wananchi kwa ujumla kuelewa matunda yatokanayo na ziara hizi na pia kung'amua na wao kushiriki katika fursa ambazo zinatokana na ziara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulisema pia ni huu ushiriki wa Mheshimiwa Rais. Pamoja na faida nyingi ambazo anazileta hapa nchini, pamoja na hii diplomasia ya uchumi, pia tunaweza tukafanya diplomasia nyingine ndani ya wigo huu wa diplomasia ya uchumi. Nilisema siku ya michezo kuwa kuna kitu kinaitwa *sports diplomacy*, ndiyo maana Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba sisi kama Taifa tutakuwa wenyeji wa *AFCON 2027*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usione mataifa yanang'ang'ana kutafuta kuwa wenyeji wa mashindano wa michezo mbalimbali, ni sehemu pia ya kukuza diplomasia, lakini pia ni sehemu ya kukuza fursa mbalimbali za kiuchumi. Kwa mfano, kwa kuandaa *AFCON* maana yake ni kwamba tutapata fursa mbalimbali, viwanda vya malighafi mbalimbali vitauza malighafi kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya michezo, hoteli na fursa nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi ninatoka Mafinga, sisi ni mahiri sana katika mazao ya misitu. Tutauza, tutauza mirunda, tutauza *linea boards* katika ku-*facilitate* mafanikio ya kuelekea maandalizi ya *AFCON 2027*. Haya yote hayatokei tu, kama tunavyosema kwamba *foreign policy* ni *extension* ya *domestic policy,* kwamba ni mwendelezo wa yale mambo yanayotokezea ndani. Maana yake ni kwamba jinsi ambavyo tuko vizuri ndani ndiyo maana hata inakubalika kwamba tuweze ku-*host* hiyo *AFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, utakumbuka wakati ilipoanzishwa ile *African League* ambayo walishiriki timu kubwa nane katika Afrika, uzinduzi wake ulifanyika hapa Dar es Salaam ambapo viongozi wakubwa wa mpira duniani walikuja, akiwemo Rais wa *FIFA*, aliyekuwa kocha maarufu wa Arsenal Arsene Wenger na viongozi kadha wa kadha. Maana yake ile ndiyo *sports diplomacy*. Unalitangaza Taifa letu, unaliweka kwenye ramani na pia unaleta uchumi katika Taifa lako. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kama nilivyosema, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri alivyosema kwenye hotuba yake kwamba amekuwa mshiriki wa makongamano mbalimbali ya Kimataifa. Hapa pengine nijielekeze, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alikuwa Paris kwenye kongamano muhimu kuhusu nishati safi ya kupikia. Ni jambo muhimu ambalo linaenda kukabiliana na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kwenye hotuba yake kwamba wataendelea kushirikiana na Wizara za kisekta katika kuhakikisha kwamba hizi fursa zinazotokana na ziara za viongozi na ushiriki wa Taifa letu katika makongamano mbalimbali zinakuwa na tija katika Taifa letu. Kwa hiyo, natoa ushauri katika suala la madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele, ameshiriki mikutano yote ya mazingira kuanzia kule Scotland, Dubai, Egypt na huu wa juzi aliokwenda pale Paris. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwa dhati ya moyo na kwa hali kubwa ya *confidence* ameyaambia mataifa makubwa ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo yanayochangia madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwamba yaweze kuheshimu ahadi zao na kutoa fedha ambazo zitasaidia mataifa madogo kukabiliana na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *Loss and Damage Fund* kwamba mataifa makubwa yachangie katika mfuko huu ili kuyapa mataifa madogo. Kwa mfano mwaka huu tumepata madhara makubwa

yanayotokana na mafuriko. Niombe Mheshimiwa Waziri a-*take lead* kwa kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ili kuwezesha pia kupata hizo fedha kutoka mifuko kama *Adaptation Fund* na *Global Climate Fund,* kwa sababu fedha zile nyingi ni *grants* wala si mikopo. Kwa hiyo, tutafute namna ya kushirikiana Wizara za kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake kwamba watataka sasa mabalozi wawe na mchango unaopimika, kwa maana ya kuwa na *KPI*. Ninakubaliana naye, lakini lazima pia iendane na vitendea kazi na kuwepo majengo. Ni kweli amesema ni muhimu sana kujenga taswira nzuri ya nchi yetu, lakini taswira nzuri ya nchi yetu inakuwa nzuri kama tunakuwa na majengo mazuri ya makazi na ofisi.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusiana na mpango wa majengo wa Mheshimiwa Waziri, hapa nina takwimu chache tu. Katika miaka kama miwili tumetumia karibu shilingi bilioni 50 kwa ajili ya makazi na ofisi. Kwa hiyo, ninawaomba pia Wizara ya Fedha, kwa sababu wao ni waratibu, fedha zipatikane ili tujenge majengo ya ofisi, majengo ya makazi na majengo ya vitega uchumi. Kwanza tutapunguza gharama zile ambazo tunalipa sasa, lakini pia tutapata fedha za kigeni kutokana na majengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumzie namna fursa za kikanda zilivyo wazi. Kwa mfano, hivi karibuni kuna majirani zetu waligombana na majirani wengine, shirika lao la ndege likaacha kwenda kule, ile ni fursa kwetu sisi kwa *ATCL*. Ninafahamu tumeshapata kibali kwenda kutua Goma na Kinshasa, basi tutumie fursa hizo kwa *ATCL* kuhudumia eneo letu la *SADC* kama sehemu pia ya kuleta dola hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na Mungu atubariki wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kupata nafasi hii ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni mwanadiplomasia namba moja nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Naibu Mawaziri wake wawili, Mheshimiwa Balozi Mbarouk na Mheshimiwa Byabato. Pia ninapenda nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii, niwapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Katibu wa Kamati Kuu ambaye ni Katibu wa Siasa na Mahusiano ya Kimataifa wa Chama Cha Mapinduzi, Dada yangu Rabia. Amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha chama chetu, Chama Cha Mapinduzi kinakuwa na ushirikiano mzuri na vyama mbalimbali duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niende kwenye takwimu kidogo. Katika nchi yetu ya Tanzania tumebahatika kuwa na akinamama wengi ambao wameipaisha nchi yetu katika diplomasia ya uchumi ya Tanzania na mataifa mbalimbali duniani. Akinamama hawa wameweza kuongoza taasisi mbalimbali za kimataifa pamoja na za kikanda katika kuiwakilisha Tanzania. Ninaomba niweze kuwataja kina mama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wa kwanza ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wa pili ni Balozi Gertrude Mongella, wa tatu Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, wa nne Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, wa tano ni Balozi Amina Salum Ali, wa sita ni Jaji Imani Aboud na huyu ni Jaji wa Mahakama Kuu ya Afrika. Saba ni Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, wa nane ni Maimuna Tarishi, wa tisa ni Mheshimiwa Stergomena Lawrence Tax na wa kumi Mheshimiwa Prosefa Anna Tibaijuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika chama chetu Chama Cha Mapinduzi tuna utamaduni wa kusema kuwa wanawake ni jeshi kubwa, lakini si jeshi kubwa katika nchi yetu tu, ni jeshi kubwa mpaka nje ya mipaka ya nchi yetu. Wanawake hawa wametuheshimisha sana katika anga ya kimataifa. Hii iwe shime na hawa niliowataja ni wachache, lakini iwe shime kwa akinamama, waweze kufanya kazi vizuri ili nchi yetu iendelee kuwa kinara katika diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali yetu kupitia Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iendeleze jitihada zake za kuweza kukuza lugha yetu ya Kiswahili Kimataifa. Hivi sasa lugha yetu ya Kiswahili imekuwa ni lugha ya tatu katika Bara la Afrika na hivi karibuni *UNESCO* wametangaza rasmi kuwa kila tarehe 7 Julai ya kila mwaka itakuwa ni Siku ya Kiswahili Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Serikali kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iongeze kasi ya kuharakisha Sera mpya ya Mambo ya Nje ili nchi yetu iweze kukaa vizuri katika safu hii ya kimataifa. Hii sera iko njiani katika kuelekeza mambo mbalimbali, lakini imechukua muda mrefu, takribani ni mwaka wa tatu sasa, lakini bado utaratibu wa kukamilika kwake haujamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania imekuwa ni kinara mkubwa wa amani na utulivu katika Bara la Afrika, lakini kupitia hiyohiyo nchi yetu imekuwa ikishiriki katika *mission* mbalimbali za kimataifa na *mission* hizo zimeiweka nchi yetu kuwa ni nchi ya 13 duniani kati ya nchi 122. Tanzania imo kati ya nchi ambazo zinapeleka askari wengi katika *mission* za kimataifa. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iendelee kuweka mkazo katika jambo hili ili idadi ya askari wetu wanaoshiriki katika *mission* za kimataifa iweze kuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia inatuonesha vilevile kwamba nchi yetu imekuwa na ukarimu wa kupokea wakimbizi mbalimbali kutoka nchi mbalimbali za jirani ambazo zimetuzunguka. Hii imetuweka katika taswira nzuri ya kuhakikisha kuwa Tanzania

inakuwa juu siku zote katika mapambano ya kuifanya dunia pamoja na Afrika kwa ujumla kuwa na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru na mimi kwa kunipatia fursa hii kuchangia chochote kuhusiana na bajeti ambayo iko mbele yetu. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai ambaye ameniwezesha kusimama leo mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwanadiplomasia namba moja katika nchi yetu kwa namna ambavyo amekuwa akiitambulisha nchi hii kimataifa. Kwa kweli amefanya kazi kubwa, kazi ambayo tunaiona na matokeo tunayaona. Kuanzia kwenye *Royal Tour,* Mheshimiwa Rais alianzia huko na leo watalii wengi wanakuja kwenye nchi yetu, tunampongeza sana. Si hayo tu, amekuwa akifanya mambo mengi na kufungua milango ya fursa ili nchi yetu iendelee kuneemeka kutokana na mataifa ambayo tunashirikiana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara, nikianzia na Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote. Tunawapongeza sana Wizara ya Mambo ya Nje kwa namna ambavyo wamekuwa wakitekeleza majukumu yao. Pia ninakupongeza Mheshimiwa Spika wetu, Dkt. Tulia Ackson, nawe ni miongoni mwa wanadiplomasia ambao wameitangaza Tanzania Kimataifa. Tunakupongeza sana. Vilevile ninapongeza uwasilishaji wa bajeti ambao Wizara umeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache, miongoni mwa mambo hayo ni kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nje kwa kuanza kubuni utaratibu mpya wa namna ya kuwapima wawakilishi ambao ni mabalozi wetu walioko katika nchi

mbalimbali. Wamesema kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2024/2025 mabalozi katika nchi zetu watapimwa, watapewa *key performance indicators* ili kuweza kusimamia utendaji kazi katika nchi ambazo wanazisimamia. Ninashukuru katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika upimaji wa namna mabalozi wetu wanavyofanya kazi nina maoni machache. Wapo mabalozi ambao wanahudumia nchi zaidi ya tatu, nne, tano na kuendelea, tunao, lakini kwa bahati mbaya sana ili kutambulishwa katika nchi nyingine wanapata wakati mgumu wa kuzifikia, kwa sababu hizo *credentials* hazifikii nchi nyingi kati ya zile ambazo wanazisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunakwenda kuwapima, huyu mtu amekaa sehemu moja, namna ya kumpima kama hatujamtambulisha kwenye yale mataifa mengine ambayo anasimamia itakuwa ni mtihani. Ile *key performance indicator* yetu ambayo tumepanga tukawape hawa watu inaweza isifikiwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukienda kwa Balozi wa India, ana nchi karibu tano, lakini ameenda kutambulishwa au amepeleka hiyo *credentials* katika nchi moja. Kwa hiyo, inakuwa ni changamoto sasa namna yeye atakavyoenda kujitambulisha yeye mwenyewe. Niombe Wizara ipange ratiba kwa mabalozi wake wakatambulishwe katika zile nchi ambazo wamepewa kuzisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hiyo tu, Kenya, Balozi wa Kenya ana nchi karibu tano, Balozi wa Brazil ana nchi karibu tisa, Balozi wa Cuba ana nchi karibu tano, lakini unakuta amekaa sehemu moja ndiyo anayoifanyia kazi, ndiyo ambayo tumemtambulisha. Sasa tutampimaje kule kwingine ambapo tunatakiwa aende, afike huko ili tuweze kumpima sawasawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo *gap* naomba Wizara basi ikafanye *coverage* ili tupate matokeo ambayo sisi kama Taifa tunakusudia kuyapata kutokana na mabalozi wetu ambao ndiyo daraja la kutuvusha kati ya nchi yetu na hizo nchi zingine

kidiplomasia ya uchumi. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara ilifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, upimaji huo wa pamoja na kwamba *credential* tutapeleka basi bajeti, iende sambamba na bajeti ambazo tutawapatia. Wasipokuwa na bajeti za kutosha pamoja na vitendea kazi, ufanisi wa kazi zao tunaweza tusiuone, basi tuwape bajeti ya kutosha ili wafanye kazi katika mazingira ambayo hata wao wenyewe watakuwa huru kufanya kazi na sisi kama nchi tupate matokeo ambayo tunataraji kuyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niombe mbali na bajeti, tuwapatie watumishi wa kutosha kulingana na mahali walipo. Kama watakuwa na watumishi wa kutosha, bajeti tumewapelekea nadhani watafanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Kwa hiyo, niombe Serikali na katika hili la kibajeti nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha, ajitahidi kupeleka fedha kadiri ya bajeti inavyopitishwa katika Bunge, kwa sababu wale wanategemea rasilimali fedha ili wakatekeleze majukumu yao, kama wasipopata hizo fedha itakuwa shida sana kwetu namna ambavyo tunaweza kuwapima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine linahusiana na ofisi zetu za kibalozi nchi za nje pamoja na vitega uchumi tulivyonavyo. Taarifa ambayo tumesomewa zipo balozi pamoja na ofisi ambazo hali yake siyo nzuri, zimechoka, zimechakaa. Niombe sana, utendaji kazi ni pamoja na uwepo wa mahali pazuri pa kufanyia kazi. Kama ofisi zimechoka, vitega uchumi havipo sawasawa, basi tutakosa rasilimali fedha ambayo ingekuja katika nchi na wao wakafanya kazi yao vizuri, lakini na huku Tanzania tukanufaika kwa uwepo wa vitega uchumi na ofisi zetu katika balozi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo hata ukiangalia kwenye Randama ya Wizara ambayo tumewasilishiwa kuna kipengele kinasema maduhuli kutoka makusanyo ambayo walitarajiwa kama Wizara hayakutimia, wamekusanya kwa uchache maduhuli ya mwaka 2023/2024 lakini inawezekana wameshindwa kukusanya kwa sababu ya hali ya majengo hata wale

wanaotakiwa kwenda kupanga wanaona hapa hapapangiki kwa sababu ya hali ilivyo.

Mheshimiwa Spika, basi niombe Serikali ikiwezekana itumie sekta binafsi, kwa sababu siyo rahisi sana Serikali kufanya kila jambo yenyewe. Basi tushirikishe na sekta binafsi, najua baadhi ya sekta binafsi tayari zimeshaanza kushirikiana na Wizara katika kuboresha miundombinu ya Wizara pamoja na vitega uchumi kule nje.

Mheshimiwa Spika, tusimamie basi vitega uchumi vikafanywe na sekta binafsi kwa kushirikiana na Serikali ili tupate tija ile ambayo sisi kama Taifa tulikuwa tunaitarajia kutoka katika hivyo vitega uchumi ambavyo vipo nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulisema linahusiana na uelewa mdogo, naomba ninukuu kutoka kwenye Taarifa ya Kamati, mimi ni-*declare interest* ni miongoni mwa Wanakamati, katika ushauri wa Kamati pamoja na maoni kipengele cha tano kinasema; "Uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta ya umma na sekta binafsi kuhusu diplomasia ya uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano na mahusiano ya kimataifa bado imeendelea kuwa changamoto katika kunufaika na diplomasia ya uchumi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wizara, sisi ndiyo wenye jukumu la kufikisha taarifa sahihi kwa wananchi kule chini, lazima tujipange kama nchi tuone wananchi wetu wanafikiwaje na fursa hizi za kiuchumi kwa sababu mataifa mbalimbali yanahitaji kupata bidhaa kutoka kwetu na ukiangalia Watanzania na nchi yetu Tanzania inayo mazao ya kilimo mengi, uvuvi kila kitu tunacho. Sasa namna ya kutoka kule chini kwa mkulima au mwananchi wa kawaida akaweza kunufaika na diplomasia ya kiuchumi iliyopo duniani ndipo mtihani ulipo. Kwa hiyo, niiombe Wizara hili jukumu ni letu, hatuna namna ya kulikwepa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, tuwafikie wananchi wa kawaida ili waweze kunufaika na fursa zilizopo nje kutokana na rasilimali ambazo tunazo kama nchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa nafasi, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Njau, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru tena kupata nafasi hii ya kuchangia katika bajeti ya Wizara hii.

Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwa bingwa wa diplomasia katika dunia na katika Afrika, hili ni jambo ambalo lipo wazi, Watanzania wanajua na dunia inalifahamu pia.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa ajili ya kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, katika sekta hii ya muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaje tu hapa kabisa ninapoanza kwamba nimeguswa sana na alilolisema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwamba Tanzania inataka kuendelea kuwa na sauti katika diplomasia ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuwekeza sana tukawa na majengo mazuri, tukawa na balozi nzuri na kadhalika, lakini kama hatuna sauti katika diplomasia ya Afrika, diplomasia ya dunia bado tutakuwa hatujafika mahali panapotakiwa. Tungetamani ifike wakati kwamba dunia ikiwa Afrika, ikiwa na migogoro watu wasikilize Tanzania inasema nini juu ya migogoro hiyo. Tungetamani mifumo ya uchumi ya dunia inapoyumba basi katika nchi za kusikilizwa na sisi Tanzania tuwe wamojawapo na biashara na kadhalika. Sauti katika diplomasia ni jambo la

muhimu sana katika kuifanya nchi yetu ifanikiwe hata katika mambo mengine. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwekea msisitizo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inatekeleza miradi mingi, lakini upo mradi mmoja ambao mimi ningependa niuzungumzie ni mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mradi huu ninaomba kusisitiza na kuiomba Serikali kwamba fedha ziendelee kupelekwa ili uweze kumalizika kwa wakati kwa sababu ni mradi wenye faida nyingi sana. Tukumbuke kwamba Tanzania ni moja kati ya waasisi wa *AU (African Union)* wa Umoja wa Afrika. Kwa hiyo, kituo hiki ambacho ni muhimu sana katika utekelezaji wa kazi za *African Union,* suala la haki za binadamu ambalo ndilo linalogusa na demokrasia na kila kitu, kuwepo kwa kituo hiki katika nchi yetu ni heshima kubwa na ni moja kati ya maeneo ambayo yanaongeza sauti yetu katika diplomasia ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili pia tukumbuke kwamba tumepewa heshima ya Rais wa Kwanza wa Mahakama hiyo kuwa Mtanzania, tena Mtanzania mwanamke Mheshimiwa Jaji Imani Aboud ambaye amefanya kazi nzuri sana toka mahakama ile ianze mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, Watanzania wanapata fursa ya kuitumia ile mahakama kwa sababu ipo karibu, ukifuatilia kesi zinazoamuliwa pale nyingi ni za kutoka hapa kwetu Tanzania na kwa bahati Mahakama ile ya Afrika imekuwa ikikubaliana na mahakama zetu jambo ambalo ni kipimo juu ya ufanisi wa mahakama zetu na suala zima la haki za binadamu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kufanikisha lile la Mheshimiwa Waziri analosema kwamba tuwe na sauti katika diplomasia ya Afrika na dunia, mradi huu ni moja kati ya maeneo ya muhimu ya kuongeza sauti yetu. Zipo faida nyingine nyingi tu ambazo kwa sisi Tanzania hatuhitaji kwenda mbali sana kuziona. Tulikuwa na Mahakama ile ya *ICTR* ile ya Rwanda wakati ule hata kodi za pango Arusha zilipanda, bei za usafiri kule magari mjini na kila kitu kwa sababu bajeti ile ilikuwa ikitumika pale na hata bajeti

hii ya Mahakama ya Afrika inapotumika pale ni faida kubwa kwa uchumi wetu na kuongeza hasa hadhi ya utalii wa jiji letu la Arusha na nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza miradi mingi nje kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza. Tuna majengo ya ubalozi mengi sasa kama Lusaka peke yake tuna viwanja kumi na kwenda juu. Ni rai yangu kwamba miradi hii hatutaweza kuitekeleza kwa bajeti ya Serikali peke yake au kwa kutegemea wabia. Miradi ya ujenzi sasa hivi duniani kote inaenda kwa utaratibu wa *mortgage finance*.

Mimi ningeshauri kwamba Serikali ibadilishe sheria za fedha ilete muswada hapa turekebishe sheria za fedha ili kuiruhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, itekeleze miradi kwa mfumo huo wa *mortgage finance* huko kokote ambapo tuna miradi inayotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatutaweza kutekeleza miradi hii kwa fedha zetu au kutegemea wabia. Mfumo wa kidunia sasa hivi kwenye *real estate* ni *mortgage finance* hasa nchi kama Marekani tungekuwa tumeshajenga ubalozi wetu pale kama sheria yetu ingeruhusu utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa nitilie tu msisitizo juu ya suala la kutangaza mafanikio ya ziara za viongozi wetu wanapokwenda nje au viongozi wa nje wanapokuja nchini, tunaona kweli linafanyika mawasiliano Ikulu na kadhalika na kadhalika, lakini mimi nadhani bado halijatosha kwa mfumo wa sasa hivi ulivyo na siasa zilivyo na kadhalika ni vizuri Wizara ikaratibu vyombo vya habari vikubwa na vidogo mpaka vile vya mitaani ambavyo vimeratibiwa, lakini siyo kuachia kila chombo, viwe vinatangaza ziara hizi na mafanikio yake ili taarifa zifike kuanzia juu kabisa mpaka kule chini vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiachia vyombo vikubwa peke yake au tukiachia Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu au Makao Makuu ya Wizara hatutaweza kuwafikia watu wote. Kwa hiyo, nadhani Wizara ingefanya uratibu zaidi ili wananchi waweze kusikia zaidi faida kubwa inayotokana na ziara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa machache hayo mimi naunga mkono hoja kwa 100%, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Njau, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwa uchache katika Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Wizara kwa namna ambavyo iliipambania bajeti ya maendeleo ya mwaka uliopita ambapo mwaka ule tulisimama hapa kwa ajili ya hilo, lakini wameweza kupata na kupelekewa 94%. Pamoja na hayo, 70% ya bajeti yote ya Wizara ya Mambo ya Nje inakwenda balozini. Inakwenda balozini kwa maana ya kulipa kodi za mapango na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye ripoti ya *CAG* ya hesabu za Serikali Kuu ya Machi, 2024 walitembelea katika balozi 43, balozi 39 walizozitembelea zilikuwa zinakodi nyumba ambayo ni ofisi pamoja na makazi ya watumishi ambapo wametumia zaidi ya shilingi bilioni 18. Fedha hizi ni nyingi na kuna balozi tatu ambazo ni kinara zilionekana kuongoza katika fedha nyingi za pango. Balozi hizi ni Balozi ya Tanzania nchini Moscow ambayo ni shilingi bilioni 1.5, Balozi wa Tanzania Abu Dhabi shilingi bilioni 1.4, Balozi wa Tanzania Vienna shilingi bilioni 1.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni nyingi kwa kulipa pango tu na pamoja na balozi hizi kuongoza, lakini Serikali haikuonesha mkakati *at least* wa kuwekeza kwenye ujenzi wa ofisi au makazi kwenye hizi balozi ambazo zinaonekana pia ni za kimkakati. Kwa hiyo, hakuna mawazo kabisa ambayo yalikuja kwa mapendekezo kwenye hizi balozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zingeweza kutumika kwenye miradi ya maendeleo, balozini kuna kero nyingi ambazo fedha hizi

zingeweza kupelekwa, lakini zinakwenda kwenye kulipa pango. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunavyoziangalia fedha hizi tunaangalia pia na matokeo, je, balozi hizi zina matokeo chanya kwa uchumi wa Taifa letu au tumepeleka tu? Kuwepo na utafiti wa kimkakati wa kuona balozi zinazoweza kulipa kwenye Taifa letu ndipo tuweze kuwekeza namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tunatangaza diplomasia ya uchumi na kimsingi tumeona ina matokeo chanya kwenye Taifa letu, hakuna ubishi kuna matokeo chanya kwenye mambo ya diplomasia ya uchumi lakini kuna balozi ambazo zilionekana ni za kimkakati ni chakavu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na balozi hizi ndiyo sebule, ndiyo *reception* ya wawekezaji, ndiyo *reception* ya watalii, ndiyo *reception* ya kukuza hii diplomasia ya uchumi. Niende moja kwa moja kwa ubalozi wa Tanzania Uingereza, jengo hili limechakaa tunalipa shilingi milioni 320 kwa mwaka, limechakaa kabisa tunalipa hiyo kodi. Ubalozi wa kudumu New York Marekani tunalipa shilingi milioni 24.8 ni hali ambayo haieleweki kwa sababu mwisho wa siku balozi hizi zinatakiwa ziwe taswira kwa Taifa letu, tunapoimba Tanzania ni pamoja tuna-*reflect* kwenye zile balozi kama zimechakaa, zipo hoi wanatuonaje sisi kwa upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hili jengo la balozi, Ubalozi wa Washington DC. Hili jengo limechakaa na kimsingi limepoteza hadhi ya kidiplomasia, hili jengo ni jengo ambalo lipo katikati linaonekana, hatuwezi kujificha, limechakaa kabisa mpaka limeondolewa hiyo hadhi.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaenda kuimba na wakati Mheshimiwa Rais anatembea nchini kwa ajili ya kuangalia fursa mbalimbali, wanaenda pia balozini ndiyo eneo ambalo wanapokelewa kwa ajili ya kuangalia fursa za nchini Tanzania. Tuliangalie kwa kina Serikali iweke mkakati madhubuti kwenye hizi balozi chakavu, lakini kwenye maeneo ambayo tunatakiwa tukajenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Balozi ya Harare, Zimbabwe, uchakavu mkubwa wa hili jengo umefanya nchi ile kutuongezea bima ya majengo kutoka shilingi bilioni 49 kwenda shilingi bilioni 58 maana wanaona hatari ipo pale. Kama tumeongezewa ni *indicator*, wakati tunapanga bajeti zetu kwenye kukarabati tuangalie sehemu kama hizi ili kuliokoa Taifa na mikono mibaya kwa sababu hii hii ndiyo itatumika kutuchafua. Kwa hiyo, sisi kama Taifa tulichukulie kwa u-*serious* wake ili tuweze kulisimamia ili balozi hizi basi ambazo zinatuchafua wakati tumeshaanza kung'aa ziweze kujengwa, ziweze kukarabatiwa, lakini ziteuliwe na balozi za kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la diplomasia ya uchumi nchini Tanzania, hili suala ni kama kitendawili kwa raia wa kawaida, hawaelewi kabisa, fursa za kiuchumi zinazotokana na diplomasia ya uchumi hawaelewi. Kwa hiyo, tulimpa ushauri Mheshimiwa Waziri kutafuta mbinu mbadala, majarida, makongamano, vyombo vya habari tuna redio, tuna *TV*, siyo mipasho, twende tukaangalie na kutangaza fursa zetu za kiuchumi zilizopo huku chini, wakulima wadogo wadogo...

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Lugangira.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba ili Wizara hii iweze kutekeleza ipasavyo diplomasia ya uchumi nadhani wakati umefika ili Wizara hii iwe *Central Ministry* ili waweze kusimamia namna ambavyo sekta zingine zinatekeleza diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, naipokea.

Mheshimiwa Spika, tuna wakulima wakina mama wa mboga mboga huku chini, wafundishwe namna gani ya kulima maparachichi, tuna matunda mbalimbali, tunaweza kwenda kupeleka moja kwa moja kwenye sehemu zenye mahitaji. Tuliomba Wizara kwenda kuangalia ni nchi gani inataka nini ili twende kimkakati, ni lazima tuguse maeneo ya kimkakati, tuguse watu wa kimkakati, tuguse mataifa ya kimkakati ili tuweze kufikia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukimwita mkulima mdogo kule chini ukamwambia kuna masoko Ujerumani, kuna masoko Uingereza hujamjengea uwezo hajui kiwango kinatakiwaje. Tutakuwa tunaimba, lakini hii diplomasia ya uchumi haiwezi kuwagusa hawa ambao tunatarajia iwaguse.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nami niwe miongoni mwa wachangiaji katika hotuba ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya njema na kuweza kushiriki katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu ambaye ndiye mwanadiplomasia namba moja kwa kazi kubwa anayofanya katika kuendelea kulitangaza Taifa letu Kimataifa hali ambayo imesaidia kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja *(DFI)*, lakini kama hiyo haitoshi ongezeko la watalii hivi karibuni pamoja na mambo mengine ni pamoja na nchi yetu kuendelea kung'aa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ihakikishe majengo na Balozi tunazoendelea kupangisha yanapewa kipaumbele kwa kufanya ukarabati na kujenga kwa kuishirikisha sekta binafsi kwani siyo rahisi kwa kutegemea bajeti ya Serikali pekee yake kwa kuzingatia kwamba rasilimali fedha haiwezi kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa machache haya naomba kuunga mkono hoja na kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa January Makamba na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbaroruk na Mheshimiwa Stephen Byabato na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu suala la uraia pacha na hadhi maalumuu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kumekuwepo na mjadala mkali kutoka makundi mbalimbali kuhusiana na baadhi ya watu kudai uraia pacha. Katika mijadala hiyo, kuna baadhi ya raia wa Tanzania wameainisha kwamba kuna madhara makubwa ya kuwapa wageni uraia pacha wa Tanzania. Hawa wametoa sababu zenye mashiko.

Mheshimiwa Spika, uraia pacha kwa kiasi kikubwa utamnufaisha zaidi mtu anayeomba kuwa na uraia wa nchi mbili au tatu kuliko nchi husika. Kwenye kutoa uamuzi ni vyema kabisa suala la usalama wa Taifa likapewa kipaumbele. Kutokana na utofauti wa itikadi za mataifa mtu mwenye uraia pacha anaweza akatumika kuhujumu nchi mojawapo.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba baadhi ya hao hao wanaoomba uraia pacha walipokuwa wanauomba uraia huko ughaibuni ilibidi kwanza waukane uraia wa nchi yetu na kupewa hadhi ya uraia katika nchi nyingine. Vilevile suala la uraia pacha halijakubalika duniani kote na hata ikiruhusiwa Tanzania baadhi ya wana-*diaspora* ambao tayari ni raia wa nchi nyingine ambazo

hawajakubali uraia pacha watakuwa na wakati mgumu ikiwa ni pamoja na kupoteza haki zao katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwenye kutetea hoja ya uraia pacha, baadhi ya watu wanatoa mfano wa nchi jirani ya Kenya ambayo iliruhusu uraia pacha mwaka 2010. Kwa maoni yangu, hoja hii haina uzito kwani si vyema kuiga majirani, kwani hatuna uhakika kama wamefanya kitu sahihi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania ni nchi yenye rasilimali na maliasili nyingi. Uzoefu umeonesha kwamba baadhi ya nchi duniani zenye utajiri kama sisi na ambazo sio za kibepari, zinakataa uraia pacha. Kwa mfano, nchi za Urabuni, India, Singapore, Malaysia, Indonesia, China na nchi nyingi za mashariki ya mbali na baadhi ya nchi za Ulaya zimekataa uraia pacha. Kutokana na mifano hii, ninaishauri Serikali ifanye utafiti wa kina ili kubaini matatizo yanayoweza kuikumba nchi yetu kama itakubali kuruhusu uraia pacha.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali yetu kwa uamuzi wa kuja na mpango wa kuwapatia *diaspora* wenye asili ya Tanzania hadhi maalumuu itakayowawezesha kufanya shughuli za kiuchumi nchini Tanzania. Huenda hadhi hili itaanza kufanya kazi mwaka wa fedha wa 2024/2025, hii ni hatua muhimu. Hivyo basi, naishauri Serikali iliweke hiki suala la hadhi maalumuu kwenye sheria zetu ili lisije kubadilishwa kiholela na kusababisha usumbufu.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali, hiyo hadhi iwape uhuru wa kurudi nyumbani Tanzania bila kuomba viza, haki ya kuwekeza hapa nyumbani na hadhi hiyo kutambua warithi wa mali watakaoteuliwa na wahusika na pia waruhusiwe kuleta maarifa mapya kutoka huko nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa January Yusuph Makamba, Naibu

Mawaziri, Katibu Mkuu na watumishi wengine wa Wizara kwa hotuba nzuri yenye taarifa muhimu za kutuwezesha Waheshimiwa Wabunge kujadili na kufanya maamuzi sahihi juu ya maendeleo ya sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwapongeze Waheshimiwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika mataifa mbalimbali duniani kwa kazi nzuri mnayofanya ya kutekeleza kwa vitendo falsafa ya diplomasia ya uchumi. Pia niwapongeze Watanzania wanaoishi nje ya nchi *(diaspora)* kwa namna wanavyochangia maendeleo ya nchi yetu. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kiujumla; nianze na fedha za matumizi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2024/2025 fedha zinazoombwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni kiasi cha shilingi bilioni 11.6 sina tatizo na bajeti hiyo. Tatizo ni miradi ya kupitia ubia na sekta binafsi na utaratibu maalumuu wa Kiserikali miradi mitatu yenye thamani ya shilingi bilioni 343.1, je, ubia huu unatekelezwa kwa vigezo na masharti gani?

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mrejesho wa ajenda zinazosukumwa katika Mabunge ya Dunia na Kikanda, nchi yetu na nchi za Afrika zimekuwa na Mabunge ya Kikanda kama *EALA, SADC, PAP, CPA* na *IPU* lakini hakuna mrejesho wa ajenda zinazosukumwa kupitia mabunge hayo, hotuba ya Waziri na ya Kamati hazijasema chochote kuhusu jambo hili. Hivi sasa nchi yetu ina mpaka Rais wa Bunge la *IPU,* Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson.

Mheshimiwa Spika, pia nchi yetu iliwahi kuwa na Rais wa *PAP,* Mheshimiwa Dkt. Getrude Mongela na Makamu wa Rais wa *PAP,* Mheshimiwa Stephen Masele, *Chief Secretary* wa Mabunge ya *CPA,* Mheshimiwa Dkt. William Shija, Katibu Mtendaji wa *SADC,* Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama zinatumia gharama kubwa kugharamia vikao katika mabunge hayo na hivyo isingetarajiwa mijadala inayoendelea katika mabunge hayo kuwa ya siri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutokulipwa fidia kwa askari wanaoshiriki operesheni za kulinda amani nje ya nchi; askari wetu wanapochukuliwa katika misheni mbalimbali za operesheni za kulinda amani kama *SADC, EAC, MUNUSCO* na kadhalika, familia za walinda amani kutoka nchi wanachama waliopoteza maisha au kupata ulemavu katika operesheni za ulinzi wa amani na mazoezi ya kijeshi nje ya nchi wamekuwa hawalipwi fidia na kuziacha familia zao kwenye ufukara wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madereva wanaosafirisha mizigo nje ya nchi; madereva hawa husafiri masafa ya mbali huku wakiwa wameacha familia zao na kuwa kwenye hatari kubwa za kiusalama na pengine sheria hutofautiana nchi na nchi kama kuzuia baadhi ya bidhaa kuingia nchi nyingine, uzito wa mzigo na sheria zingine za barabarani, lakini pia kutekwa na ajali. Lakini pamoja na hayo yote madereva wetu na vijana wetu wanaendelea kulitetea Taifa lao kwa kuhakikisha kuwa mizigo yote inafika panapohusika sehemu mbalimbali duniani na kwenda kwa majirani zetu nchi za Rwanda, Burundi, DRC Congo, Zambia, Kenya, Malawi, Zimbabwe, Uganda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, madereva hawa kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamika kwa kutokuwa na mikataba ya ajira baina yao na matajiri, kutokuwa na bima, kulipwa masurufu kidogo yanayopelekea kushindwa kujikimu wawapo safarini na kuhudumia familia zao. Familia kuachwa kwenye dhiki kubwa inapotokea vifo na ulemavu unaosababishwa na ajali au kutekwa. Waziri wa Mambo ya Nje atueleze ni mkakati gani uliopo wa kuhakikisha madereva hawa wanapata maslahi mazuri na kuwakinga dhidi ya majanga ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Kuhusu kukosekana kwa mtandao mpana wa utoaji habari *(massive coverage)***;** nchi za Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla hazina mkakati wa pamoja wa kutangaza mambo ya ndani ya nchi husika na kubadilishana taarifa kama ilivyokuwa miaka ya mwanzoni mwa Uhuru ambapo kila nchi iliripoti mambo ya nchi zingine za Afrika. Licha ya mageuzi makubwa ya teknolojia ya habari kiwango cha kubadilishana habari ni kidogo sana na hivyo kila nchi imejifungia na mambo yake. Nakumbuka waasisi wetu

walitumia vyema redio na magazeti kudai Uhuru, pia Redio ya Taifa ya Kenya *(KBC Nairobi)* ilisikika maeneo mbalimbali ya Tanzania hadi vijijini, lakini leo maeneo mengi redio hiyo haipatikani. Nawakumbuka Kina Leonard Mambo Mbotela katika kipindi maarufu cha Je Huu ni Uungwana? Mambo yalikuwa mazuri sana. Leo mambo yamegeuka, mtandao wa mawasiliano Afrika Mashariki umekatika vimebaki vyombo vya habari vya kimataifa ambavyo navyo huripoti mambo mabaya tu kama mizozo na machafuko, vita, njaa, ukame katika nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, taasisi za umma zinavyodharauliwa kama TBC kuacha kurusha Bunge na kwenda kwenye matukio mengine na ziara za viongozi, Bunge lingepewa heshima inastahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Umoja wa Afrika; ushirikiano wa nchi za Afrika ulianza mapema katika kipindi cha mapambano ya ukombozi wa mataifa ya Afrika kutoka kwenye makucha ya wakoloni ambapo nchi za Afrika ziliungana kwa pamoja kudai Uhuru kutoka kwa Waingereza, Wajerumani, Wafaransa, Makaburu, Waarabu na kadhalika. Hatutasahau namna waasisi wetu walivyojitoa kwa hali na mali kupigania Uhuru wa Bara la Afrika hadi nchi zote za Afrika zikapata Uhuru. Viongozi wetu mashuhuri *(illustrious leader)* wakiongozwa na Kwame Nkrumah, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Jomo Kenyatta, Samora Machel, Nelson Mandela, Sam Nujoma, Kenneth Kaunda, Robert Mugabe, Thomas Sankara na wengine wengi. Viongozi hawa walifanya kazi kubwa ya kuzipatia Uhuru nchi zetu, kuweka mifumo ya utawala, kukuza uchumi ambapo njia kuu za uchumi zilirejeshwa na kumilikiwa na umma na vita dhidi ya maadui ujinga, umaskini na maradhi vikatangazwa. Tumekuwa tukiendelea kushuhudia ustawi wa nchi za Afrika tangu mapambano yalipoanza.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mapambano hayo nchi za Afrika zimeungana katika kanda mbalimbali ikiwemo *AU, EAC, COMESA, SADC* na kadhalika na ajenda mbalimbali zikiwemo zimekuwa zikiwekwa na kutekelezwa. Mfano Dira ya Maendeleo ya Afrika (Ajenda 2023 - *The Africa We Want), APRM* na Misheni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo bado kuna changamoto nyingi zinazokwamisha ustawi wa Bara ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matatizo sugu Barani Afrika; pamoja na mafanikio tuliyoyapata Afrika Mashariki na Afrika, lakini zipo baadhi ya changamoto ambazo binafsi naona bado hazijashughulikiwa kikamilifu na hivyo kuhitaji mikakati mipya, maarifa mapya na mbinu mpya katika kuyatafutia ufumbuzi matatizo hayo. Naomba kutoa mifano tisa kama ifuatavyo:-

(i) Mapigano na uvamizi wa magaidi baina ya nchi za Afrika Mashariki na Afrika; baadhi ya nchi zimekuwa zikikabiliwa na migogoro inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na tofauti za kiitikadi, kudorora kwa uchumi, ugaidi, mizozo na machafuko ya kisiasa hali ambayo imekuwa ikipelekea vifo, majeruhi, njaa, wakimbizi na wahamiaji haramu, ongezeko la uhalifu unaovuka mipaka, mateso ya kina mama na watoto na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishuhudia mapigano yasiyokwisha Mashariki mwa Congo baina ya majeshi ya Serikali ya Congo *(FARDC)* na vikundi vya waasi ikiwemo Vikosi vya M23 ambavyo vimedumu kwa zaidi ya miaka 30 sasa.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa, tumekuwa tukishuhudia tume za upatanishi na misheni za ulinzi wa amani za kijeshi zimekuwa zikiundwa kutoka *EAC, SADC, SAMIM, AU, FIB* na kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa *(MONUSCO)* ili kukomesha mapigano hayo na kurejesha amani Mashariki mwa Congo, lakini jambo la kusikitisha mapigano hayo yanazidi kupamba moto kila uchao.

Pia huko Kaskazini mwa Ethiopia mapigano yamekuwa yakiendelea baina ya majeshi ya Serikali na waasi *(Tigray rebels)* katika vita maarufu ya *Tigray War.* Huko Somalia chokochoko ya vita ya wenyewe kwa wenyewe *(Somalia Civil War)* na uvamizi wa magaidi hali inayoleta machafuko ya mara kwa mara katika nchi hizo na kuhatarisha usalama wa raia wake na nchi jirani. Tumeshudia pia kuwepo kwa machafuko huko Msumbiji, Libya, Mali, Morocco, Saharawi, Sudan na kadhalika. Ni ukweli usiopingika kuwa kukosekana kwa amani katika nchi hizo ni

kukosekana kwa amani kwa Afrika Mashariki, Afrika na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, maswali ya kujiuliza kwa nini mapigano hayakomi na kwa nini amani hairejei katika maeneo hayo licha ya hatua zinazochukuliwa na *UN, AU, SADC* na *EAC?* Binafsi naona nchi za Afrika Mashariki na mamlaka zingine hazijawekeza kikamilifu kushughulikia mizizi ya machafuko hayo ili kukomesha mapigano na kurejesha amani.

Mheshimiwa Spika, tulishuhudia kiongozi wa kundi la kigaidi la *Al Qaeda,* Osama Bin Laden alipofanya shambulio la kigaidi katika jengo refu la *World Trade Centre* Mjini New York nchini Marekani tarehe 11 Septemba, 2001 na kusababisha vifo vya watu 3,000. Nchi ya Marekani chini ya Rais George W. Bush na marafiki zake ikiwemo Uingereza chini ya Waziri Mkuu wa wakati huo Tony Blair walitangaza vita dhidi ya magaidi kote duniani na wakaapa kuwa hawatapumzika hadi ugaidi utokomezwe na kurejesha amani duniani kote.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo tukaanza kushuhudia mapigano makali ya vita dhidi ya ugaidi pamoja na mtandao wake wa *Al Qaeda,* mashambulio makali yalifanywa na majeshi ya Marekani, Uingereza na *NATO* katika nchi za Pakistan na Afghanistan ambako ndiko ilikuwa hifadhi ya magaidi. Hatimaye tulisikia kuwa Osama Bin Laden ameuawa na mtandao wake wa *Al Qaeda* wote kuteketezwa na amani duniani kurejea.

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa walijua athari za kuenea ugaidi duniani na ndiyo maana walitangaza na kupigana vita na walikataa suluhu ya aina yoyote. Leo kwa nini machafuko ya rejareja yaruhusiwe katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, mizozo, machafuko na mapigano yanayoendelea yanarudisha nyuma jitihada za nchi za Afrika kujiletea maendeleo. Wakuu wa nchi na Serikali za Umoja wa Afrika mko wapi haya yanaendelea? Dkt. Samia Suluhu Hassan mwanamke shupavu, Dkt. William Ruto msomi kiongozi Bara la

Afrika, Yoweri Kaguta Museveni, Rais mkongwe mko wapi haya yanaendelea.

(ii) Ufisadi, rushwa na matumizi mabaya ya raslimali; kutokana na kushamiri kwa rushwa, ufisadi na matumizi mabaya ya rasilimali za asili nchi nyingi za Afrika, umasikini unazidi kuongezeka licha ya utajiri mkubwa tulionao wa rasilimali kama bahari, maziwa, mito, madini, ardhi yenye rutuba, mifugo na wanyama, misitu, gesi asilia, mafuta na kadhalika. Nchi nyingi zinakosa mapato ya kutosha kwa ajili ya maendeleo na kuendesha nchi kwa sababu fedha na rasilimali za umma ziko mikononi mwa watu binafsi huku nchi kwa sehemu kubwa zinategemea misaada na mikopo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mifumo madhubuti ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na rasilimali za umma hali inayopelekea fedha za umma kuishia mikononi mwa watu wachache. Chanzo kikubwa ni uingiaji wa mikataba mibovu, utoroshaji wa rasilimali na fedha nje ya nchi *(illicit financial flows), transfer pricing, capital flight,* wizi, rushwa na ufisadi ni kidonda ndugu kilichokosa tiba Barani Afrika. Pamoja na kuwepo sheria, wakaguzi wa ndani na nje, Mamlaka za Kudhibiti na Kupambana na Rushwa, kuanzishwa kwa vitengo vya *FIU* na *EITI, APRM* na mamlaka zingine za usimamizi wa sheria, lakini hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya nchi za Afrika zinakusanya kodi kwa uwiano wa pato la Taifa chini ya kiwango kinachokubalika cha 15%, mfano Tanzania inakusanya 12.5% tu, Uganda 13.3%, Kenya 14.2% ya Pato la Taifa na hivyo kukosekana mapato ya kutosha kugharamia shughuli za maendeleo na uendeshaji wa Serikali. Mfano Tanzania inaripotiwa kutorosha nje ya nchi zaidi ya shilingi trilioni 3.5 kwa mwaka na Kenya inaripotiwa kutorosha zaidi ya shilingi ya Kenya bilioni 40 (sawa na shilingi bilioni 744) kwa mwaka. Pia nchi nyingi zipo kwenye viwango visivyokubalika vya riba za mikopo, mfumuko wa bei na viwango vya ubadilishaji fedha. Swali la kujiuliza ni kwa nini mwanya huu wa upotevu wa mapato na rasilimali za nchi umeshindwa kudhibitiwa Barani Afrika?

(iii) Mikopo na misaada; nchi nyingi za Afrika zimetumbukia kwenye mzigo mkubwa wa madeni *(Highly Indebted Poor Countries-HIPC)* na mikopo hiyo inatolewa kwa masharti magumu na ya kinyonyaji. Nchi nyingine kuchukua mikopo inayolindwa na dhamana ya maliasili za nchi kama madini, gesi, mafuta, bandari na kadhalika; kuingiliwa katika utungaji na usimamizi wa sera, sheria, kanuni, miongozo, programu na mikakati na hivyo kunyang'anywa uhuru wa kujiamulia mambo wakati mwingine kutekeleza miradi ambayo haipo kwenye vipaumbele vya nchi ili kukidhi matakwa ya wahisani, mikopo kukosa uwazi, ulinganifu na yenye riba kubwa na masharti mengi ya kinyonyaji na kusababisha mfumko mkubwa wa bei za bidhaa.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya aina hii imezifanya nchi nyingi za Afrika kufilisika na kurudi nyuma kiuchumi na kuendelea kuishi kwa kutegemea misaada na mikopo na kupelekea kuongezeka kwa migogoro ya kifedha hasa inapotokea ugumu wa kurejesha mikopo hiyo. Kwa nini nchi za Afrika zimeshindwa kujenga uchumi imara na kuendelea kutegemea misaada na mikopo. Bwana Donald Kaberuka, gwiji wa uchumi huko nchini Rwanda aliwahi kusema Waafrika tunatakiwa kugundua namna ya kutumia rasilimali zilizopo katika Bara la Afrika ili kuibadilisha Afrika. Nchi zingine kukusanya kodi chini ya 15% ya pato la Taifa na kuendelea kutegemea mikopo na misaada ambapo kumepelekea nchi nyingi za Bara la Afrika kuwa na madeni makubwa ya nje kiasi cha kushindwa kuendelea kukopesheka na kusababisha matatizo makubwa kwenye nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, wakuu wa nchi na Serikali na Umoja wa Afrika wana mipango gani ya kufanya mageuzi katika kuweka mikakati mipya ya kuondokana na mtego huu wa madeni katika nchi za Afrika?

(iv) Uwekezaji na biashara katika nchi za Afrika Mashariki; shughuli za uwekezaji na biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na mafanikio tuliyoyapata bado zinachangamoto nyingi licha ya uwepo wa Itifaki ya Umoja wa Forodha *(EAC- Common External Tariff),* Itifaki ya Soko la Pamoja na Itifaki ya Sekta za Uzalishaji na Miundombinu zilizowekwa kwa ajili ya kuongeza kasi ya kufufua uchumi na kuimarisha sekta za

uzalishaji katika jumuiya. Pia mikakati mingi imekuwa ikiwekwa kama kuanzishwa kwa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki *(EABC)* na Eneo Huru la Biashara Afrika *(AfCFTA)* kwa lengo la kuongeza kasi ya biashara na uwekezaji, kuongeza uzingatiaji wa viwango na ubora wa bidhaa, kuongeza thamani na kupanua soko la bidhaa, lakini bado nchi za Afrika zinaendelea kuwa soko la bidhaa kutoka nje na zenyewe kukazana kuuza malighafi badala ya bidhaa zilizoongezwa thamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashirikiano ya kibiashara baina ya nchi za Afrika Mashariki na Afrika; mashirikiano ya kibiashara baina ya nchi za Afrika Mashariki *(Intra -EAC Trade)* ni mazuri japo yana changamoto nyingi hususan biashara za Serikali na Serikali ambapo baadhi ya nchi zinaagiza bidhaa kutoka nje ya ukanda wa *EAC, SADC, COMESA, AU* na kadhalika hata kwa bidhaa ambazo zinapatikana ndani ya kanda husika. Mfano mchele, ngano, mahindi, samaki, nyama, maziwa, matunda na mbogamboga, mafuta ya kupikia, sukari, mashudu, wanyama hai na mazao ya misitu kama samani, karatasi, pia vifaa vya ujenzi kama saruji, mabati, vigae, chuma na plastiki, mifumo ya TEHAMA na kadhalika, kwa mfano Tanzania inauza nchini Kenya wastani wa 3.8% tu ya thamani ya mauzo kwa mwaka.

Kuhusu kuchelewa kwa matumizi ya sarafu moja katika nchi za Afrika Mashariki, vikwazo visivyo vya kikodi na ukosefu wa mitaji unachangia kwa kiwango kikubwa kuzorota kwa uwekezaji na biashara. Ubinafsi huu unazifanya nchi za Afrika Mashariki na Afrika kutokufanya vizuri zaidi katika biashara za kikanda. Mimi naamini kwamba kukosekana kwa mashirikiano thabiti ya kibiashara inatokana na kukosekana kwa utashi wa kisiasa. Tumekuwa tukifanya vibaya katika eneo hili licha ya kuwepo kwa Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayosisitiza kuongeza uzalishaji na kiwango cha matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, *CCECC* na makampuni mengine ya nje ya *Africa Tech Mahindra;* kuuza malighafi badala ya bidhaa zilizoongezwa thamani; nchi nyingi za Afrika Mashariki zinauza malighafi katika masoko ya Afrika Kusini, Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE),* India, China, Uswisi na Masoko ya *AGOA* na kuuza

kiasi kidogo sana katika masoko ya *EAC, SADC, COMESA, ECOWAS* na kadhalika. Hali hii inazifanya nchi za Afrika Mashariki kutonufaika kikamilifu na rasilimali zake. Ni kitu cha kusikitisha sana kwamba tunasafirisha nje ya nchi mbegu za mafuta halafu tunaagiza mafuta ya kupikia kwa gharama kubwa, tunasafirisha nje ya nchi pamba ghafi halafu tunaagiza nguo kwa gharama kubwa, tunasafirisha magogo halafu tunaagiza karatasi, samani, nguzo za umeme kwa gharama kubwa, tunaagiza mbolea tani kwa tani wakati tuna samadi na mboji zikioza ardhini na kadhalika, ipo mifano mingi inaumiza sana.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kwamba hakuna kizuizi kinachofanya nchi za Afrika zisijenge viwanda vya kuongeza thamani mazao, hivyo kitendo cha kuendelea kuuza malighafi katika masoko ya Ulaya, Asia, Marekani na Masoko mengine ni kukosekana kwa dhamira ya dhati. Pamoja na kuwepo kwa utekelezaji wa programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika sekta za uzalishaji, miundombinu ya Uchumi, lakini bado tunafanya vibaya katika eneo hilo.

(v)Kuchelewa na kusuasua kwa utekelezaji wa maazimio, itifaki na makubaliano; kumekuwepo na itifaki, maazimio na makubaliano mbalimbali ambayo yamekuwa yameridhiwa katika vikao halali vya *AU, SADC, EAC* na kadhalika, lakini uridhiwaji na utekelezaji umekuwa wa kusuasua na kurudisha nyuma kasi ya maendeleo katika nchi za Afrika. Pia zipo changamoto za kukosekana kwa mfumo wa kupata mrejesho wa mabunge ya kikanda kama EALA, SADC, PAP, CPA, IPU na kupelekea kusuasua kwa maamuzi na kutungwa sheria za ndani ya nchi husika.

Pamoja na tathmini ya utekelezaji wa mpango wa kwanza wa miaka kumi ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Afrika *(Agenda 2063, The Africa We Want)* lakini matokeo ya tathmini hiyo kuhusu mafanikio, fursa na changamoto hayawekwi wazi na wakuu wa nchi na Serikali na Umoja wa Afrika ili kutoa fursa ya kujipima hatua iliyofikiwa.

(vi) Tatizo la ajira; nchi za Afrika kupitia Umoja wa Afrika zimeweka mikakati, programu na kuchukua hatua mbalimbali ili kutatua tatizo la ajira katika Bara la Afrika *(Youth Employment*

*Intervention in Africa)* lakini badala yake tatizo la ajira linazidi kuongezeka kila siku. Nchi za Afrika zimeanzisha Umoja wa Vijana *(Pan African Youth Union-PYU)* na pia kuingia katika makubaliano ya kisheria *(The African Youth Charter)* ili kuweka mikakati itakayowezesha kusukuma ajenda ya upatikanaji wa ajira katika bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa ajira bado ni kubwa ambapo 5.1% ya wananchi wote duniani hawana ajira kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2023. Huku kwa upande wa Bara la Afrika ikiwa ni 7%. Serikali za nchi wanachama, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi nazo hazijarudi nyuma katika mapambano ya upatikanaji wa ajira kwa vijana.

Pia nchi wanachama zinapata msaada mkubwa kutoka *ILO* na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* katika kutengeza ajira za vijana. Hata hivyo nchi za Afrika bado hazijafanikiwa kutatua tatizo la ajira kwa vijana, ukipitia utekelezaji wa *MDGs* na *SDGs* unathibitisha wazi kuwa nchi za Afrika zinahitaji mikakati mipya kupambana na hali ya ukosefu wa ajira kwa vijana katika sekta za umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zinazosababisha hali kuendelea kuwa mbaya zaidi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana sera na sheria madhubuti za kulinda na kutengeneza ajira za wazawa katika Bara la Afrika, sheria na sera zilizopo zinakinzana na hazitoi ulinzi wa kutosha kulinda ajira. Mfano manunuzi, *local content* na mikataba inayoingiwa. Katika sekta ya ujenzi miradi mingi imechukuliwa na wageni mfano Kampuni ya *CCECC* imepewa miradi ya maji, barabara, ujenzi wa *SGR,* madaraja, bandari na kadhalika.

(ii) Kukoseka kwa mifumo ya udhibiti hali inayopelekea kushamiri kwa biashara za magendo, kugeuzwa kuwa dampo za bidhaa hafifu na zilizokwisha muda wa matumizi, kukwepa kodi na hivyo kupelekea kuua viwanda vya ndani na ajira.

(iii) Sekta kubwa zinazoajiri Waafrika wengi kutopewa kipaumbele katika mipango na bajeti za nchi wanachama kama

Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Madini, kukosekana kwa viwanda vya chakula, nguo, dawa, ngozi, viatu, nyama, maziwa, mbolea huku wanaochimba madini kwa sehemu kubwa sio Waafrika na hao wachache wachimbaji wadogo wanakutana na hujuma za kila aina. Hii inapelekea nchi nyingi za Afrika kuendelea kutegemea bidhaa kutoka nje huku ikiuza bidhaa zake kama malighafi kwa mataifa ya nje tena kwa bei ya kutupa na kuua ajira nchini.

(iv) Mifumo dhaifu ya elimu na ujuzi, mitaala na namna tunavyowandaa vijana wanashindwa kukidhi mahitaji ya soko la ajira, wanakosa ujuzi na maarifa ya kuajiriwa na kujiajiri. Hata mageuzi makubwa ya TEHAMA yameshindwa kuwa suluhisho la upatikanaji wa ajira nchini.

(vii) Umasikini na maradhi; licha ya mikakati inayowekwa kitaifa na kimataifa kama malengo ya *MDGs, SDGs* nchi nyingi za Afrika zilishindwa kufikia malengo hayo, nchi zingine umasikini umepungua kwa kiwango kidogo na zingine umasikini unazidi kuongeza kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo usimamizi hafifu wa sera za fedha na bajeti, mizozo na machafuko ya kisiasa, ukosefu wa ajira, wizi, rushwa, ufisadi na matumizi mabaya ya rasilimali za nchi, lakini pia kumekuwa na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza kama figo, moyo, kisukari, saratani, shinikizo la damu na kadhalika. Magonjwa haya yanaongezeka kwa kasi kila uchao, lakini hakuna tafiti za kitabibu *(medical research)* zilizofanywa ili kujua kiini cha tatizo na hatua za kudhibiti magonjwa hayo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; tunataka Afrika yenye amani na utulivu, tunataka Afrika yenye maendeleo na ustawi wa watu wake, hivyo ni lazima kufanyia kazi na kuyatafutia suluhisho la kudumu matatizo sugu yanayolikabili Bara la Afrika. Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika waandae mikakati mipya ya namna ya kukabiliana na matatizo hayo na tukaioneshe dunia uelekeo mpya.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kazi nzuri inayofanywa na nchi wanachama na Umoja wa Afrika *(AU)* katika kufikia maendeleo ya kweli ambapo pia tume na misheni mbalimbali zimekuwa zikiundwa. Hili la matatizo sugu nalo linahitaji kuundiwa

tume na nimuombe Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika *(AU)* na Rais wa Mauritania Mheshimiwa Mohamed Ould Cheikh Gazouani aunde tume kuandaa mikakati mipya ya namna ya kukabiliana na matatizo sugu Barani Afrika na ikimpendeza aniteue mimi Luhaga Joelson Mpina niwe miongoni mwa wajumbe wa tume hiyo ili nitoe mchango wangu kwa Bara langu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha uhusianao na ushirikiano wetu na mataifa mengine, pia nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje - Mheshimiwa January Makamba, ni Waziri mchapakazi na sio muongo, akisema ndiyo ni ndiyo na akisema hapana ni Hapana. Ni kiongozi wa mfano wa kuigwa. Mwenyezi Mungu aendelee kuwapigania siku zote viongozi wetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi naomba kuchangia kama ifuatavyo na kwanza niombe Wizara hii ishirikiane kwa karibu na sekta binafsi hasa wadau wanaojihusisha katika umataifashaji wa sekta mbalimbali nchini, ikiwemo kumataifisha elimu yetu ya juu, utamaduni wetu na biashara zetu ili kukuza utalii nchini, kuongeza fursa za ajira, kunufaika na uchumi wa kidunia pia. Wadau wakiwepo mawakala kama *overseas education agencies* mfano *Global link* na wengine, mawakala wa kupeleka wananchi na wafanyabiashara nje na ndani ya nchi kama *SiMAC*.

Mheshimiwa Spika, pili Wizara isaidie kuwaunganisha sekta binafsi na fursa zilizopo nje ya nchi kwa ku-*recruit* wananchi kuhudhuria maonesho mbalimbali huko nje, ikiwemo makongamano na matamasha mbalimbali na kadhalika kwa ajili ya *exposure* kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iharakishe mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Mambo ya Nje ili kuleta mabadiliko yatakayoihusisha sekta binafsi katika kushirikiana na Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante Sana. Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk na Mtoa hoja, ajiandae. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. STEPHEN L. BYABATO):** Mheshimiwa Spika, mimi kama walivyotangulia wenzangu nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia mimi afya lakini na wengine wote ambao tupo humu leo. Tunaweza kujadiliana na kupitisha bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ajili ya utekelezaji mkubwa wa mambo ambayo Mheshimiwa Waziri katika hoja aliyatoa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwa na imani na mimi na kuendelea kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na hasa ninayeshughulikia Mambo ya Afrika Mashariki, imani hii kwangu ni kubwa. Ninamwahidi yeye, ninakuahidi wewe pamoja na Bunge lako na Watanzania wote kwamba nitaendelea kutumikia Taifa hili kwa moyo mkunjufu na thabiti na kwa kujitoa kwa kiwango ambacho Mwenyezi Mungu atanijalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango; Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais, majukumu na sisi tukiwa chini yao tukiwa tunafanya kazi hiyo kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano ambao mimi binafsi mnanipatia lakini na Wizara kwa ujumla na tunaweza kutekeleza majukumu ambayo Watanzania wanayatarajia kutokea kwetu.

Mheshimiwa Spika, nisiache kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini, ambao ndio walionituma katika jengo hili tukufu na ninawaahidi kuendelea kuwatumikia. Ninawahakikishia kwamba kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaonekana siyo tu Bukoba peke yake na Kagera peke yake ila kwa Taifa zima na kazi yake nzuri ndio itakayotubeba sisi, wao na yeye kuendelee kusonga mbele. Ninaomba tuendelee kushikamana na waendelee kunipa ushirikiano ambao wananipatia. Wengine wachache umewaona hapa wamekuja kushuhudia kijana wao nikifanya kazi ambayo wamenituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kuishukuru sana familia yangu ambayo imeendelea kunivumilia na kunipa *support* katika utendaji wa kazi na leo tunaweza kufikia hatua hii tuliyofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nizungumze kidogo kwenye maeneo mawili; nitazungumzia kidogo umuhimu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia, nitasema kwa uchache ni mambo gani mawili ambayo tumejipanga nayo makubwa katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, Tanzania sisi ni wanachama wa Jumuiya za Kikanda na za Kimataifa nyingi Afrika Mashariki ni moja wapo, lakini tupo kwenye *SADC*, tupo kwenye Umoja wa Nchi ambazo zinazunguka Bahari ya Hindi, tupo kwenye Umoja wa Afrika, tupo kote huko. Mheshimiwa Rais, ikampendeza mwaka jana mwezi wa Agosti, mwishoni akaniteua mimi kuwa Naibu Waziri ninayesimamia mambo ya Afrika Mashariki katika Wizara inayoongozwa Mheshimiwa January Makamba, ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja. Pia, akamteua Mheshimiwa Balozi Stephen Mbundi, ambaye ni Katibu Mkuu, anayesimamia upande ambao ninasimamia mimi wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kusema tu kwa kifupi ni kwa nini tunaona Mheshimiwa Rais ameamua kuipa uzito Jumuiya ya Afrika Mashariki na kufanya hayo? Sababu ya kwanza, ni katika kutekeleza maelekezo ya mkataba wetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ibara ya 13 ya mkataba wetu

ambao tuliusaini mwaka 2000 unaeleza kwamba, kila nchi itakuwa ina Waziri anayesimamia mambo ya Afrika Mashariki au aliyekasimiwa au kuelekezwa kusimamia mambo au masuala hayo. Sasa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaongozwa na Mheshimiwa Waziri kaka yetu Mheshimiwa January Makamba, lakini Mheshimiwa Rais akaona haitoshi aongeze watu wengine ambao watakuwa ni *focal persons* kwa ajili ya kushirikiana na Mheshimiwa Waziri na kutimiza maelekezo yanayotolewa kwenye upande wa Afrika Mashariki ambayo ilitajwa kwenye mkataba wetu tuliousaini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ambalo pia ni la muhimu ujirani mwema uliopo katika hizi Nchi za Afrika Mashariki ukiendelea vyema sisi kama Tanzania tunaendelea vyema. Ukiharibika sisi kama Tanzania tunaharibikiwa. Sisi sote hapa ni mashahidi pale ambapo nchi za jirani zinapata matatizo kama magonjwa ya kuambukizwa, sisi huku tuna haha, kwa sababu tunajikinga na tunalazimika kuwasaidia wenzetu kwa kipato kidogo tulicho nacho na walichokuwa nacho wao.

Mheshimiwa Spika, wakiwa na mambo ambayo hayaleti amani katika usalama, sisi Tanzania tunahaha tunatakiwa tuhakikishe usalama katika nchi hizo upo na unaendelea kuwepo. Pia, wakipata mambo mema sisi tuna neemeka.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Uganda walipata sehemu ya kuchimba mafuta na wameanza kuchimba. Sisi Tanzania ni wanufaika kwa sababu Bomba la *EACOP* linapita hapa kwetu. Mahitaji ya kuzalisha umeme kwenye nchi yao yakiongezeka, sisi tunavyo vyanzo vya kuwauzia. Viwanda vikiongezeka sisi tunayo malighafi ya kuwapelekea. Kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha hizi Nchi za Afrika Mashariki, zinapewa kipaumbele na mtazamo ambao ni chanya kuhakikisha kwamba, tunaendelea kushirikiana kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni kubwa kabisa, taarifa zinaonesha katika *export* za vitu vinavyotoka viwandani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ndiyo inaongoza kwa *export* kutoka kwenye bidhaa za viwandani ukiachana na madini. Bidhaa nyingine zinazotoka viwandani karibia 99% ya *export* ni

katika Eneo la Afrika Mashariki. Ni kwa sababu hizo nchi nyingine za mbali zaidi tunapeleka *raw materials* na tukipeleka *raw materials* huko ajira zetu hapa nyumbani zinapotea.

Mheshimiwa Spika, katika hili soko kubwa la hapa Afrika Mashariki ambalo tunaweza kupeleka bidhaa zetu zilizochakatwa na tukaweza kupata pesa nyingi zaidi. Imeonekana ni vyema na ni bora ipewe kipaumbele mahususi cha kuhakikisha ina watu ambao wakilala wanawaza Afrika Mashariki, wakiamka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja. Malizia Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. STEPHEN L. BYABATO):** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Basi nimalizie la mwisho, kwamba, katika mwaka unaokuja tumejipanga kuhakikisha yale ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaelekeza ameyataja katika hotuba kwamba, tutakwenda hasa kwenye Eneo la *KPI* kuweka viwango vya kuweza kupima.

Mheshimiwa Spika, katika hilo itatusaidia kwenye kubidhaisha Kiswahili, kwa sababu tunataka tutoke kwenye kubidhaisha Kiswahili kwa kipindi cha ukombozi ambapo tulikuwa tunapelekea Kiswahili kwa gharama. Tunataka sasa kianze kununuliwa kwa sababu watu wengi watakuwa wanakuja kutafuta *material* Tanzania na hivyo lazima wajifunze Kiswahili kutoka kwetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa kunipa hii fursa ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Ninaomba kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu

Mtukufu mwingi wa rehema kwa kuturuzuku afya njema na kutuwezesha kujadili hotuba hii siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kipekee nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuhudumu katika nafasi ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko (Mbunge), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa miongozo yao na maelekezo yao katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nikushukuru wewe binafsi; Mheshimiwa Naibu Spika; na Wenyeviti wote wa Bunge hili kwa namna ambavyo mnaliongoza Bunge letu kwa hekima, busara na umahiri mkubwa. Aidha, ninaomba kuishukuru Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maoni na ushauri wao ambao siku zote wamekuwa wakitupatia.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ni Kamati makini sana na imekuwa msaada mkubwa sana kwa Wizara yetu. Kwa kweli na Wajumbe wake ni wabobezi katika masuala ya kidiplomasia na hivyo wamekuwa chachu katika kuboresha utendaji wa Wizara na diplomasia ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia, ninaomba kumshukuru sana Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa uongozi wake mahiri na ushirikiano mkubwa ambao ananipatia mimi na wenzangu ndani ya Wizara. Kwa hakika uongozi wake, miongozo yake na maono yake yameleta ufanisi mkubwa katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninamshukuru Naibu Waziri mwezangu Mheshimiwa Wakili Msomi Mheshimiwa Stephen Byabato (Mbunge) ni Waziri ambaye anashughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Pia, Makatibu Wakuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara yetu, bila ya kuwasahau Mabalozi wetu ambao wanafanya kazi kubwa ya kutuwakilisha katika sehemu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu napenda pia kuishukuru familia yangu kwa upendo na uvumilivu wao na kuendelea kuniunga mkono wakati ninapotekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nichangie hoja, lakini naomba nianze kuchangia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanadiplomasia namba moja ya nchi yetu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuipaisha Diplomasia ya Tanzania na kuitangaza nchi yetu Kimataifa. Chini ya uongozi wake na kwa kipindi kifupi tu nchi yetu imeshuhudia mageuzi makubwa katika historia ya diplomasia ya nchi yetu. Sifa ya Tanzania, heshima ya Tanzania na hadhi ya Tanzania imeongezeka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa hili ni mialiko mingi ya Kimataifa ambayo amekuwa akiipokea na maombi mengi ya viongozi wa nje ya kutaka kufanya ziara hapa nchini kwetu. Pia, kukubali mialiko ya Mheshimiwa Rais wetu. Muhimu zaidi ni kwamba, hii imepelekea kukuwa kwa uchumi wetu, pia, kuongezeka kwa wawekezaji, kuongezeka kwa watalii na kuongezeka kwa mitaji kutoka nje *(Foreign Direct Investment)*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nieleze masuala ambayo baadhi ya Waheshimiwa wameyachangia hapa. Kwanza, ni suala la mchakato wa hadhi maalumu kwa *diaspora,* hili amelichangia vizuri hapa dada yangu Mheshimiwa Mbunge wa Arusha wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Catherine Magige.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kama tulivyoeleza hapo mwanzo ni kwamba, tayari Serikali imekamilisha maandalizi ya kutoa hadhi maalumu kwa

raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania *(Tanzania non-citizen diaspora)*. Tunategemea kwamba, hivi karibuni Muswada utawasilishwa wa marekebisho madogo ya Sheria ya Uhamiaji Sura Namba 54 na Sheria ya Ardhi Sura 113, ili hii hadhi maalumu ili iweze kuanza utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kukufahamisha kwamba, hadhi maalumu itakayotolewa imezingatia maombi ambayo yaliwasilisha na *diaspora* wenyewe. Maeneo hayo ambayo waliyaomba ni fursa ya kuingia, kukaa na kutoka nchi bila kikomo wala kutozwa *Visa*.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kurithi mali na kurithisha mali, haki ya kununua na kumiliki ardhi. Pia, haki ya kupewa, haki ya kuwa Wanachama katika Mifuko ya Hifadhi ya Taifa na kupata faida ambazo zinatokana na uwanachama wa mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa ni kwamba Serikali inategemea kupata faida nyingi kutokana na kutoa hadhi maalumu. Faida hizo ni pamoja na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kupitia fedha zitakazotumwa hapa nchini. Pia, kuongezeka kwa uwekezaji kupitia hisa na upatikanaji wa takwimu za *diaspora* ili kuwezasha nchi yetu kufanya maamuzi ya kisera.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja. Malizia Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** …Pia ni kutangaza utalii na upatikanaji wa teknolojia na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilizungumzwa hapa ni suala la uendelezaji wa viwanja vyetu katika Balozi zetu mbalimbali. Ninaomba kulifahamisha Bunge kwamba, kama alivyosema hapa Mheshimiwa Waziri ni kwamba tayari Wizara imeweka mkakati mahususi wa kuhakikisha kwamba Balozi zetu au viwanja vyetu vinajengwa huko nje na Balozi zetu zinakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, ilitajwa hapa kuhusiana na *issue* ya Ubalozi wetu ulipo Addis Ababa, Ethiopia; Mwezi Februari mwaka huu Wizara yetu ilitangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho na tayari taratibu za ndani zinaendelea na karibuni huo ujenzi utaanza. Pia, ilielezewa hapa…

**SPIKA:** Kengele ilishagonga Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. BALOZI MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, basi ninamalizia tu kutoa taarifa kwamba ilielezewa hapa pango kubwa tunalotoa au tunalolipa katika nchi za Abu Dhabi, Urusi pamoja na *Seoul.* Ninaomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, tayari Serikali ya *UAE* imekabidhi kiwanja kwa Ubalozi wetu na hivi karibuni taratibu za ujenzi zitaanza na hivyo kulipunguzia Taifa kodi kubwa ambayo inatoka huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mtoa hoja, kuja kuhitimisha hoja yake. Yupo mgeni wa Mheshimiwa Byabato, ambaye anaitwa John Joseph Mugangu, huyu ni mmoja wapo wa Watunzi wa Wimbo wa Afrika Mashariki, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa January Makamba, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki: Wakurugenzi na Maafisa kutoka Wizara ya Mambo Nje na Ushirikiako wa Afrika Mashariki na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Bumbuli, karibuni sana. *(Makofi)*

Wadau wa Wizara kutoka Benki za *NMB*, *CRDB* na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, karibuni sana. *(Makofi)*

Wakurugenzi na Wanafunzi kutoka Chuo cha Diplomasia cha Dr. Salim Ahmed Salim, karibuni sana. *(Makofi)*

Wawakilishi wa Jumuiya za Kikanda wanaowakilisha vijana kutoka sehemu mbalimbali na Ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Anna Lupembe, ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni watatu kutoka *General Hospital* ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo la wageni sasa nimwite Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini pia ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja hii imechangiwa na wachangiaji 13, waliozungumza tisa na waliochangia kwa maandishi wanne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wote, niishukuru Kamati kwa umahsusi kwa taarifa yake nzuri ambayo kama ilivyo kawaida imetupa mambo mengi mazuri ambayo tutafanyia kazi. Pia ninawashukuru Wabunge wote waliochangia kwa kututia moyo, kutupongeza na kutupa ushauri ambao kwa hakika kabisa tutaufanyia kazi na utaleta tija na manufaa katika utekelezaji wa kazi zetu na katika kuipaisha diplomasia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba tumepokea na yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaeleza tutayatolea majibu ya maandishi. Kwa hiyo, kabla ya Bunge hili kuahirishwa kila Mbunge ambaye amechangia kwa maandishi au kwa kuzungumza atapata maandishi ya majibu ya hoja ambazo ametoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nitumie muda huu kuzungumzia mambo machache tu ambayo nadhani ni muhimu kuyaweka vizuri na nashukuru sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri Mheshimiwa Mbarouk na Mheshimiwa Byabato wameelezea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala hili la *KPI* (upimaji wa utendaji kwa matokeo). Tumepokea ushauri wa Kamati, ushauri wa Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mheshimiwa Chumi kuhusu haja ya kuliweka vizuri hili, kwa sababu ni kweli na ni dhahiri kwamba vituo vinatofautiana. Balozi aliyepo Malawi huwezi kumpa malengo au vipimo sawa na aliyepo Beijing. Katika utaratibu tuliouweka tumezingatia hilo pia, tumefanya uchambuzi wa kina na kujua mambo gani kila kituo na kila Balozi apewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi tumewapa kazi mabalozi wenyewe watuletee ni aina gani ya vipimo na malengo wanavyotaka tuwapime navyo. Hili siyo zoezi ambalo limetoka Wizarani tu kwamba jamani mtafanya hiki, pia wao watueleze kwa mwaka wawekezaji ambao wanaweza kuwavutia Tanzania, *scholarship*, biashara na kadhalika. Kwa hiyo, tumepokea yale maoni yao na sisi tutachanganya na uchambuzi wetu na tutatoa, lakini tunaelewa na tumepokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba Balozi peke yake bila ufanisi wa makao makuu, bila nyenzo, hivi vitu havitafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata katika kuweka malengo tumezingatia changamoto zilizopo na tumezingatia vikwazo vilivyopo. Kwa hiyo, malengo yamewekwa kulingana na mambo yote hayo. Tunadhani ni utaratibu mzuri ambao unaanza kujenga utamaduni wa kupimana na kupitia Bunge hili Kamati itajulishwa kuhusu mwenendo wa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la Mheshimiwa Maimuna kuhusu uwakilishi katika mwenendo huo huo wa *KPI*. Ni kweli kutokana na rasilimali nchi yetu, Balozi unamuweka pale Abuja, mnamwambia unatuwakilisha kwenye nchi nyingine 14 kwa sababu hatuna uwezo wa kuweka Balozi kwenye kila nchi, hiyo ni kazi kubwa kwa sababu nchi 14 za Afrika Magharibi ni

nyingi, kwa hiyo lazima Balozi awe na uwezo na watu wa kutosha kuweza kutuwakilisha kwa ufanisi kwenye nchi zote hizo 13 au 14.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hivyo tulifanya uchambuzi hivi karibuni wa mtawanyo wa uwakilishi duniani na kupanga upya maeneo ya uwakilishi. Vilevile Waheshimiwa Mabalozi wametakiwa watuletee uchambuzi wa fursa zilizopo kwenye kila kituo ikiwemo kile ambacho ni mwenyeji na kile ambacho anawakilisha akitokea kituo kingine ili ionekane haja na uharaka wa kumpa barua ya utambulisho ili aende kule akajitambulishe na aweze kutuwakilisha. Kwa hiyo, kazi hiyo inafanyika hivi tunavyoongea na mabalozi wanatuletea maoni yao na uchambuzi wao kuhusu kule ambako wanahitaji wapewe hizi *credentials* ili waende. Kwa hiyo, hilo tuliona tuliweke hivyo ni zao la kazi mpya ambayo tumeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumziwa suala la watumishi. Tunashukuru sana kwa *support* kubwa tunayopata kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi wakiongozwa na Waziri Mheshimiwa Simbachawene hasa pia na Katibu Mkuu wa Utumishi. Kwa kweli tulipopeleka mahitaji pamoja na changamoto zilizopo waliyazingatia na bado kazi ipo ya kujaza vituo vyetu kwa wanadiplomasia ambao ni mahiri.

Mheshimiwa Spika, katika hilo Mheshimiwa Rais aliridhia tuanzishe utaratibu mpya unaitwa *Presidential Foreign Service Fellowship*. Huu ni mpango mahsusi wa Rais wa kutafuta vijana wenye vipaji vya juu kabisa katika jamii yetu ambao watakubali kuchukua miaka mitatu wakilipwa vizuri na baada ya kutahiniwa kwa viwango vya juu sana vya kimataifa, waje kutumika Wizarani na kwenye Balozi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama watafuzu katika hicho kipindi cha miaka mitatu basi watapewa fursa ya kuajiriwa. Tunatarajia wale wanaotoka shuleni, lakini hata wale waliopo kwenye *private sector* mfano mtu anafanya kazi benki labda *Standard Charter* au wapi, Mtanzania ana miaka 40 ameona abadilishe upepo aingie Serikalini kwenye diplomasia anaruhusiwa kuja kwa utaratibu huu maalumu ambao utakuwa na mtihani mahsusi wa kupima kila kitu, maarifa yote ya lugha, kuandika na kujieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imani yetu ni kwamba tukifanya hii programu kwa miaka mitano au sita tutakuwa tumeshehenisha Wizara yetu na diplomasia mahiri wakiwemo watu kwenye sekta binafsi ambao wanaweza kufanya kazi hii ya diplomasia na kuisaidia nchi yetu. Kwa hiyo, mpango huo tutauanza katika mwaka ujao wa fedha na tumeuandika kwenye hotuba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine limezungumzwa ni suala la miradi ya ujenzi. Ni kweli sisi ni wanadiplomasia, lakini tunalazimika kujenga majengo na kusimamia ujenzi, tulisaidiwa na wenzetu wa utumishi kupewa wahandisi. Ilibainika kwamba kuna tatizo, wanaohitajika siyo wahandisi, wanaohitajika ni watu wanaojua biashara ya nyumba na majengo na siyo tu nchini, ni duniani kote. Kwa sababu ukimchukua mtu anayejua kuweka paa vizuri wakati huo unataka kufanya biashara ya nyumba ama jengo pale Kinshasa huyo mtu hatakusaidia.

Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba sasa maarifa na ujuzi tutakaouomba kutoka Serikalini uwe ni watu wanaojua *real estate business* duniani, kwa sababu tuna viwanja na majengo 109 dunia nzima, ni utajiri mkubwa sana na lazima utupe manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uwekezaji na aina ya uwekezaji na ubia lazima utokane na ujuzi na utaalamu katika biashara hiyo. Kwa hiyo, tunashukuru kupitia Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi tumepewa msaada huo na kuna Kamati maalum na kuna kampuni ambayo itapewa kazi ambayo ndiyo kazi yake hiyo, kufanya uchambuzi wa kila kiwanja, kila jengo tulilonalo duniani na linaweza kutuingizia pesa kwa namna gani na uwekezaji wa namna gani unahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na Waheshimiwa Wabunge hapa wamezungumza, kwa kweli wapo sahihi kwamba hali ya baadhi ya majengo yetu haiendani na heshima ya nchi yetu na hilo lazima tulibadilishe kabisa. Mtu ambaye hajafika Tanzania akienda Washington DC pale kwenye Ubalozi wetu ile ndiyo Tanzania. Kwa hiyo, akiingia mapokezi lazima taswira ya nchi yetu ionekane pale mapokezi. Kwa hiyo, kama panavuja,

kama fanicha zimechakaa ile ndiyo sura ya nchi anaipata. Kwa hiyo tumekubaliana tubadilishe hiyo hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka tunatumia shilingi bilioni 29 kulipa pango kwenye Balozi zetu na kwenye Ofisi za Ubalozi, shilingi bilioni 29.6 kwa mwaka. Sasa katika viwanja vyote tulivyonavyo ambavyo tunataka kuweka vitega uchumi, tukipata shilingi bilioni 692 kwa ajili ya huo uwekezaji, mapato tutakayoyapata ni shilingi bilioni 36.3. Naomba nirudie, tukiweza kupata shilingi bilioni 692 kufanya uwekezaji tutapata mapato kila mwezi kutokana na pango shilingi bilioni 36. Maana yake ni zaidi ya tunazolipa sasa hivi kwa pango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine ambapo hata ile kodi ya mwezi ingeweza kuwa *mortgage* na baada ya miaka 20 lile jengo linakuwa la kwenu kama alivyosema Mheshimiwa Wakili Tadayo pale. Kwa hiyo, tumependekeza na tumekubaliwa na nadhani italetwa mabadiliko kwamba badala ya kulipa kodi ile kodi ndiyo iwe *mortgage* na lile jengo baadae unalimiliki wewe kuliko kulipa kodi kwa hela hiyo hiyo ambayo ungelipa *mortgage*. Kwa hiyo, hilo linaendelea na tunashukuru sana Serikali kuturuhusu kuingia katika utaratibu huo mpya ambao utatusaidia tuwe na majengo, maofisi na nyumba ambazo zinaendana na hadhi na heshima ya nchi yetu. Kwa hiyo, kilio cha Waheshimiwa Wabunge tumekipokea na wapo sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la sekta binafsi tumeanza na wenzetu wa *NSSF* kama washirika wetu angalau kwa sehemu mbili Kinshasa, Nairobi na tunazungumza kuhusu Kampala. Kwa hiyo, inawezekana tukafanya nao katika maeneo mbalimbali ili tuweze kumaliza hili jambo.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema kwamba kama nilivyosema katika hotuba yetu, kila nchi ina kiwango tofauti cha ushawishi, ushawishi ndiyo unawawezesha mpate mnayoyataka. Naomba nirudie, ushawishi ndiyo unawawezesha mpate mnayoyataka, nyenzo za ushawishi zipo nyingi. Nyenzo ya kwanza ni umahiri wa wanadiplomasia wenu, uwezo na maarifa yao na vitendea kazi vyao.

Mheshimiwa Spika, ni lazima muwe na utaratibu wa kupata wanadiplomasia mahiri ili waweze kutetea maslahi ya nchi. Nyenzo nyingine ya ushawishi ni misimamo sahihi kwenye mambo sahihi. Moja ya urithi wa nchi yetu kiasi kwamba tunaheshimika mpaka sasa ni hayo mawili. Tulikuwa na historia ya wanadiplomasia mahiri lakini pia tuna historia ya misimamo sahihi katika mambo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu ni kwamba turudi kule ambapo nchi yetu ilikuwa inasikilizwa, inaheshimika, inasifika na inapata inayoyataka. Kwa maana hiyo lazima turudi kwenye kujenga wanadiplomasia mahiri na kuwawezesha kufanya hiyo kazi lakini turudi kwenye kusimamamia mambo sahihi katika jumuiya ya Kimataifa, hiyo kazi ndiyo mwanzo huu na tunashukuru sana kwamba Bunge lako lipo pamoja na sisi katika mwelekeo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo tunayotaka wote tunayajua ambayo yanahitaji ushawishi, uwekezaji nchi zinashindana kuvutia uwekezaji, misaada na mikopo, nchi zinashindana kuvutia misaada na mikopo, fursa za ajira kwa Watanzania nje na vilevile biashara na masoko.

Mheshimiwa Spika, nchi tunazopakana tunazalisha bidhaa zinazofanana na masoko tunayagombania huko duniani. Wanadiplomasia na umahiri wa wanadiplomasia wetu unaweza kutusaidia kufungua masoko ya bidhaa ambazo tunaziuza. Nitatoa mfano mimi. Nchi ya India inanunua sana mbaazi, Lindi na Mtwara wanalima mbaazi na Mikoa mingine. India inatoa *quarter* ya mbaazi kwamba kila mwaka kwa sababu kule pia wanalima, kuna kiwango inachoruhusu cha mbaazi kutoka nje kuuzwa mle nchini na ukiingia kwenye lile soko bei ni kubwa. Kilichotokea ni kwamba kutokana na ushawishi wa diplomasia ya Tanzania ikiongozwa na Rais wetu badala ya kuuza tani 50,000 kwa mwaka mnapewa mpaka tani 200,000 - 250,000 - 300,000. Hayo ndiyo yaliyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni nini? Kutokana na ushawishi wa diplomasia bei ya mbaazi inakuwa kubwa kwa sababu soko lipo. Kwa hiyo, nimalize kwa kusema Wizara yetu hii na Diplomasia

ya Tanzania ina mchango kwenye kila eneo la maisha na ustawi wa nchi yetu. Kuanzia ulinzi na usalama, na sote Watanzania tunaposafiri nje tunawezeshwaje kwa urahisi wa kusafiri.

Mheshimiwa Spika, kama nchi yenu inaheshimika, inaaminika ni rahisi hata ninyi Watanzania mmoja mmoja huko duniani kupata fursa na kusifika na kuheshimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango na niseme kwamba kazi hii tumepewa na tutaifanya kwa weledi na maarifa makubwa kwa sababu kazi hii tunaipenda na Waheshimiwa nilionao pale kuanzia Makatibu Wakuu na Menejimenti nzima na Mabalozi wetu huko duniani wanaipenda na wanaifanya kwa maarifa na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa kweli nitoe pongezi na shukrani mahsusi kwa Mabalozi wetu walioko nje ya Tanzania kwa kuifanya kazi hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kifungu 1001– *Administration and Human Resources Management*…………………….....…..Sh. 18,937,898,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……….. Sh. 2,825,518,244
Kifungu 1003 – *Foreign Affairs Office Zanzibar*……..Sh. 1,537,908,000
Kifungu 1004 – *Policy and Planning Unit* ……………Sh. 3,557,987,300
Kifungu 1005 – *International Cooperation*………… Sh. 1,585,676,000
Kifungu 1006 – *Europe and America* ………………..Sh. 3,249,106,001
Kifungu 1007– *Asia and Australia*…………………… Sh. 7,229,791,114
Kifungu 1008 – *Africa*…………………………………...Sh. 4,275,547,933
Kifungu 1009 – *Regional Cooperation*……………....Sh. 1,807,652,000
Kifungu 1010 – *Protocol*…………………………………Sh. 5,891,381,052
Kifungu 1011 – *Legal Services Unit*…………………....Sh. 2,671,196,850
Kifungu 1012 – *Government Communication Unit*… Sh. 961,001,400
Kifungu 1013 – *Middle East Division*………………….. Sh. 1,732,865,000
Kifungu 1014 – *Internal Audit Unit*……………………....Sh. 766,902,797
Kifungu 1015 – *Procurement Management Unit* …... Sh. 729,366,085
Kifungu 1016 – *Information and Communication Technology Unit*..................................Sh. 1,026,697,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 123(2) iwapo zimesalia dakika 10 kabla ya kumaliza muda ulioongezwa chini ya fasili ya kwanza ambayo nilishaongeza, Kamati inaweza kupitisha mafungu yote. Kwa hiyo, katibu tusomee mafungu. *(Makofi)*

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kifungu 1017– *Diaspora Engagement And Opportunity*.................................Sh. 987,922,080
Kifungu 1018 – *Economic Infrastructure and Social Support Service Division*....... Sh. 1,175,428,000
Kifungu 1019 – *Political, Defence and Security Affairs*…………......................................... Sh. 1,144,612,000
Kifungu *1020 – Trade, Investment and Productive Sector Division*………..……………….... Sh. 1,331,482,000
Kifungu 1021 – *Economic Diplomacy Division*…….Sh. 1,083,191,000
Kifungu 1022 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 650,013,000
Kifungu 2001 – *Embassy of Tanzania-Addis Ababa* Sh. 3,282,752,341
Kifungu 2002 – *Embassy of Tanzania – Berlin*……….Sh. 4,535,525,051
Kifungu 2003 – *Embassy of Tanzania – Cairo*……….Sh. 3,765,693,132
Kifungu 2004 – *Embassy of Tanzania – Kinshasa*….Sh. 4,321,446,023
Kifungu 2005–*High Commission of Tanzania Abuja*.Sh. 4,295,295,635
Kifungu2006 – *High Commission of Tanzania – London*...........................Sh. 5,553,776,075
Kifungu 2007 – *High Commission of Tanzania – Lusaka*...........................Sh. 2,305,181,289
Kifungu 2008 – *High Commission of Tanzania – Maputo*.........................Sh. 2,259,522,735
Kifungu 2009 – *Embassy of Tanzania – Moscow*…Sh. 3,974,749,832
Kifungu 2010 – *High Commission of Tanzania – New Delhi*.....................Sh. 4,242,726,577
Kifungu 2011 – *Permanent Mission to The UN – New York*.........................Sh. 5,388,107,136
Kifungu 2012 – *High Commission of Tanzania – Ottawa*.......................Sh. 3,078,275,287
Kifungu 2013 – *Embassy of Tanzania – Paris*………Sh. 3,714,683,578
Kifungu 2014 – *Embassy of Tanzania – Beijing*…….Sh. 4,512,509,453
Kifungu 2015 – *Embassy of Tanzania – Rome*…….....Sh. 4,422,260,268
Kifungu 2016 – *Embassy of Tanzania – Stockholm*...Sh. 5,189,454,422
Kifungu 2017 – *Embassy of Tanzania – Tokyo*……...Sh. 4,482,825,666
Kifungu 2018 –*Embassy of Tanzania–Washington*...Sh. 4,666,971,213
Kifungu 2019 – *Embassy of Tanzania – Brussels*…….Sh. 4,791,608,141

Kifungu 2020–*Permanent Mission to The UN – Geneva*..............................Sh. 6,101,496,746
Kifungu 2021 – *High Commission of Tanzania – Kampala*........................Sh. 2,373,807,730
Kifungu 2022 – *High Commission of Tanzania – Harare*...........................Sh. 2,149,630,858
Kifungu 2023 – *High Commission of Tanzania – Nairobi*...........................Sh. 4,536,491,299
Kifungu 2024 – *Embassy of Tanzania – Riyadh*……..…Sh. 3,434,007,545
Kifungu 2025 – *High Commission of Tanzania – Pretoria*...........................Sh. 3,419,776,697
Kifungu 2026 – *Embassy of Tanzania - Kigali* ….……Sh. 2,052,064,436
Kifungu 2027 – *Embassy of Tanzania - Abu-Dhabi*…Sh. 5,276,941,999
Kifungu 2028 – *Embassy of Tanzania– Bujumbura*…Sh. 2,008,276,322
Kifungu 2029 – *Embassy of Tanzania - Muscat*……..Sh. 2,717,545,958
Kifungu 2030 – *High Commission of Tanzania – Lilongwe*........................Sh. 2,261,722,061
Kifungu 2031– *Embassy of Tanzania – Brasilia*………Sh. 3,529,676,597
Kifungu 2032 – *High Commission of Tanzania - Kuala Lumpur*...............................................Sh. 2,611,279,436
Kifungu 2033 – *Embassy of Tanzania - The Hague*...Sh. 3,559,578,979
Kifungu 2034 – *Embassy of Tanzania – Moroni*…......Sh. 2,878,728,177
Kifungu 2035 – *Embassy of Tanzania - Kuwait* …..…Sh. 2,289,216,745
Kifungu 2036 – *Embassy of Tanzania – Algiers*…..……Sh. 2,747,126,447
Kifungu 2037 – *Embassy of Tanzania – Ankara*…….Sh. 3,714,802,963
Kifungu 2038 – *Embassy of Tanzania -Khartoum* ….Sh. 1,550,893,712
Kifungu 2039 – *Embassy of Tanzania - Seoul* …….....Sh. 6,144,591,894
Kifungu 2040 – *Embassy of Tanzania - Tel-Aviv* ……Sh. 3,838,139,114
Kifungu 2041 – *Embassy of Tanzania – Doha*………Sh. 3,213,966,643
Kifungu 2042 – *Embassy of Tanzania - Havana* …...Sh. 3,084,022,703
Kifungu 2043 – *Embassy of Tanzania – Windhoek*...Sh. 2,952,664,513
Kifungu 2044 – *Embassy of Tanzania - Jarkata* ……Sh. 2,746,448,197
Kifungu 2045 – *Permanent Mission to The UN – Vienna*................................Sh. 4,300,451,519

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kifungu 1004 - *Policy and Planning Unit* …………Sh. 11,633,376,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana na sasa nitawahoji hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji na ninyi kuafiki, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa Makadirio yao ya Mapato na Matumizi na Bunge. Tunawatakiwa kila la heri kwenye kutekeleza yale ambayo mmeahidi kupitia Hotuba yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo nitumie fursa hii kuwashukuru sana Kamati yetu, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii, mnafanya kazi nzuri ya kuisimamia Wizara hii. Tunawashukuru sana kwa kufanya kazi hii vizuri na kwa uadilifu mkubwa sana. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nanyi nyote tunawashukuru wale ambao mmepata nafasi ya kuchangia na ambao hamjapata nafasi ya kuchangia. Ushauri mnaotoa mara kwa mara kupitia maswali yenu hapa Bungeni, lakini pia wakati mwingine kuwaona Naibu Mawaziri ambao ndiyo wapo hapa mara nyingi na Mheshimiwa Waziri, basi yanasaidia kuboresha.

Pia Wabunge mbalimbali ambao mnatuwakilisha huko katika vyombo mbalimbali vya kimataifa huko mnakoenda, baadhi yenu mmetoa ushauri hapa kwa uzoefu mlioupata katika hayo maeneo mliyoenda kutembelea. Bila shaka Mheshimiwa Waziri ataendelea kuufanyia kazi na huko anakozunguka na yeye

basi maadamu anazunguka na Mheshimiwa Rais, basi wanazitafuta wote fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii na tunaamini maendeleo ni pamoja na balozi zetu kuwa katika hali nzuri kama Mheshimiwa Waziri alivyosema. Tunawatakia kila la heri katika hayo pia. *(Makofi)*

Mambo mawili; la kwanza nimeletewa ujumbe hapa, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati akihitimisha hoja yake jana alizungumza kuhusu marekebisho ambayo yamefanywa ama mapitio yaliyofanywa kwenye Sera ya Ardhi.

Leo wakati Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki akiwasilisha hoja yake alisema kwamba tunayo sasa Sera mpya ya Ardhi. Kwa hiyo, haijajulikana kama Sera ya Ardhi ni mpya au ni sera ile ile, lakini imehuishwa. *(Makofi)*

Sasa wakati mwingine haya mambo yanaweza kuwa yanachanganya kidogo kwa sababu sera siyo sheria kwamba itaitwa kile kipindi chake halafu, yaani sera huwezi kuwa na nakala mbili lakini Sheria unaweza kuwa na nakala mbili. Kwa maana ya kwamba, ile sheria ya kwanza halafu na yale marekebisho yake lakini sera huwa inatoka hata mabadiliko yakifanyika madogo lazima ichapwe mpya na lazima iitwe hivyo.

Hata hivyo kwa maelezo ya ujumla upande wa Serikali kwa matumizi ya haya maneno kwamba ni sera mpya ama ni sera iliyokuwepo ambayo imepitiwa? Nadhani mchakato wa kutengeneza sera mpya ni tofauti na mchakato wa kuhuisha sera. Kwa hiyo, hilo ndilo linaloleta changamoto. *(Makofi)*

Hivyo, kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameshahitimisha hoja yake, ninyi kati ya hayo mawili Bunge litapaswa kujua ni lipi kati ya hayo. Kama ni sera mpya ama ni sera ile, lakini mmefanya mapitio pamoja na kwamba mwisho wa haya lazima itakuwa ni moja kwa sababu hauwezi kuwa na sera hii lakini ina marekebisho haya. Kwa hiyo, mkishawasiliana kuhusu hilo mtaweza kutupa taarifa ili tuwe na hakika ni lipi kati hayo mawili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho ni tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mara baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge basi Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya semina ambayo itatolewa kuhusu Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori Wakali na Waharibifu itakayotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa kwenye semina hiyo. *(Makofi)*

Sasa naona miguno mingi, sina hakika kama kuna wanyama wakali kule Msekwa. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi kwamba mtawakuta sasa wanyama wakali kule, hapana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana kwa uvumilivu wenu maana tumeongeza muda kidogo, lakini nawashukuru sana. *(Makofi)*

Tunaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.28 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 29 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*